# KUTESWA KWA AJILI YA KRISTO



# KUTESWA KWA AJILI YA KRISTO

# Tortured For Christ

## Swahili Edition

Copyright 2015 Voice Media

info@VM1.global
Web home: www.VM1.global

All rights reserved. No part of the publication may be reproduced, distributed or transmitted in any form or by any means, including photocopying, recording, or other electronic, or mechanical methods, without the prior written permission of the publisher, except in the case of brief quotations embodied in critical reviews and certain other noncommercial uses permitted by copyright law. For permission requests, email the publisher, addressed "Attention: Permission Coordinator," at the address above.

This publication **may not be sold, and is for free distribution** only.

# YALIYOMO


UTANGULIZI
KUHUSU MWANDISHI

| Sura | | Ukurasa |
|---|---|---|
| 1 | KANISA LA SIRI, Sehemu ya I | 13 |
| | Kuongoka<br>Lugha Mbili Zafanana<br>Warusi Wana Roho za Kiu<br>Kuhubiri Katika Kambi za Warusi<br>Kanisa la Siri Lilivyotenda Kazi Wazi | |
| 2 | MATESO NA KUOSHWA AKILI | 41 |
| | Mateso Yasiyosemeka<br>Maana ya Kuoshwa akili<br>"Sisi Tuhubiri, Wao Watupige?"<br>Yaliyowapata Mke na Mtoto Wangu | |
| 3 | UHURU WA MASHARTI | 61 |
| | Sababu ya Kutoka Nchini Rumania | |
| 4 | HATARI YA UKOMUNISTI | 66 |
| | Tulivyofurahi Gerezani<br>Kushambulia Ukomunisti Kiroho<br>Funzo la Historia ya Dunia<br>Mateso Baada ya Kufunguliwa | |
| 5 | KANISA LA SIRI, Sehemu ya II | 105 |
| | Kutumia Vitabu vya Kikomunisti<br>Wakomunisti Waweza Kuokolewa<br>Makundi Maalum ya Kanisa la Siri | |
| 6 | MAGAZETI YA KIKOMUNISTI | 129 |
| | Ushuhuda wa Magazeti<br>Barua Maalum | |
| 7 | UJUMBE KUTOKA KANISA LA SIRI | 156 |
| | Wajibu wa Wakristo Huru | |

# Utangulizi

Ulikuwa mwezi Desemba, mwaka 1964 nilipoingia katika nchi ya Rumania kwa mara yangu ya kwanza. Mapema baada ya kufika Albania, Rumania peke yake ndiyo ilikuwa nchi niliyokuwa sijafika bado katika Ulaya. Kwa muda wa miezi kadhaa, Mungu alikuwa amenidhihirishia wazi kwamba nifike. Hivyo nilivuka mpaka wa nchi ya Hungary nikaingia Rumania nikiwa katika msafara wa Mchungaji John Moseley.

Mara moja tulitambua kwamba tulikuwa katika nchi ya Kikomunisti ambapo watawala walituchunguza kwa uangalifu sana. Hata hivyo, waamini walitupokea kwa shangwe. Basi, Jumapili jioni, ikiwa ndiyo Jumapili ya kwanza ya majuma manne kabla ya siku ya Kuzaliwa kwake Kristo, tulikwenda kusali katika Kanisa la 'German Baptist' mjini Bucharest. Ndugu walituomba kila mmoja wetu atoe salamu na ushuhuda. Baada ya mkutano, baadhi ya watu walizungumza nasi, na miongoni mwao palikuwa na mtu mrefu mwenye shauku iliyochanganyika na huzuni kidogo. Ndugu huyu alitusihi tuzungumze naye, ndipo alijitoa kutukaribisha nyumbani kwake. Hivyo usiku ule kama saa nne tulikwenda katika nyumba ambayo Richard Wurmbrand na mkewe Sabina, pamoja na mtoto wao Mihai waliishi – chumba kidogo katika orofa ya juu.

Tuliingia kimya! Ndipo Pasta ambaye habari zake zilivuma mno katika sehemu za Magharibi, alifunua siri ya visa vya kushangaza wakati alipokuwa amefungwa gerezani muda wa miaka kumi na minne. Kwanza mtoto wao Mihai alitoka nje kuchunguza. Ndipo Sabina mkewe naye alifuata. Wote walileta habari kusema, nyumba

ilikuwa imezungukwa na polisi waliongojewa na motakaa upande mwingine wa nyumba jirani iliyokabili yetu.

Mioyo yetu ilitudunda vibaya vifuani!Je, wataichunga nyumba ile mpaka lini? Tena, matokeo yake yatakuwaje? Richard Wurmbrand alimaliza masimulizi ya visa vyake, sote tukaomba. Ule ulikuwa mkutano wa maombi ya kukumbukwa kwa vile tulivyotoa dua zetu na kumsihi Mungu awalinde watumishi wake. Wakati tulipoona makovu na alama za mateso katika mwili wake, tulitambua uovu na hofu kuu ya kutisha mno ya wakati ule. Walakini nuru ya utukufu wa upendo iliingia katika visa vile vya mateso ya kifungo gerezani. Mungu alisikia dua zetu. Maana tulipotoka nje barabarani, wale askari polisi walikuwa wametoweka.

Nasi kwa mara ya kwanza tulikuwa tumekutana na jamaa ya Mungu, jamaa yenye ushuhuda wa kishujaa kwa ajili ya Yesu Kristo. Sote tulijisikia kubadilika wala siyo kudumu vile vile tulivyokuwa. Kwa hiyo naona heshima kuu kuandika UTANGULIZI wa kitabu hiki. Nami naandika kwa moyo nikimwomba Mungu aamshe mioyo ya watu wengi ili wawapende watu wa Ulaya ya Mashariki kusudi matokeo ya huruma kuu yalete misaada kwa watu wale wateswao kwa ajili ya Jina la Yesu Kristo, ili kukamilisha mateso ya Kristo miilini mwao kwa ajili ya Mwili wa Kristo, ambalo ni Kanisa.

– – – – –

# Kuhusu Mwandishi

Mchungaji Richard Wurmbrand ni Pasta wa Injili ambaye alikaa miaka kumi na minne katika gereza la Kikomunisti nchini kwake Rumania. Yeye ni mmojawapo wa Warumania Wakristo viongozi, wandishi na walimu.

Mwaka 1945 Wakomunisti walipovamia nchi ya Rumania na kutawala makanisa yote kwa makusudi yao, Richard Wurmbrand alianzisha "huduma ya siri" kwa askari wa Kirusi na wafungwa wao. Huduma hii ilifanikiwa, mwishowe yeye pamoja na mke wake Sabina walikamatwa. Mkewe alitumikishwa kazi za kipagazi muda wa miaka mitatu, lakini Pasta Wurmbrand kwa miaka mitatu alifungiwa katika chumba cha pekee bila kuonana na mtu ye yote isipokuwa watesi wake tu. Baada ya miaka hiyo mitatu, alipelekwa katika gereza la jumuia ambako aliteswa miaka mitano zaidi.

Kwa ajili ya kujulikana sana kama kiongozi Mkristo, mabalozi wa nchi za nje waliomba serikali ya Kikomunisti imfungue. Lakini walijibiwa kwamba Wurmbrand alikwisha toroka Rumania. Polisi wa siri wakijifanya kama wafungwa wenzake, nao walimwambia mkewe kuwa waliwahi kuhudhuria mazishi yake katika makaburi ya gereza. Jamaa na rafiki zake Rumania na penginepo ng'ambo waliambiwa wasahau habari zake.

Baada ya miaka minane, Richard Wurmbrand alifunguliwa tena. Ndipo mara moja aliendelea na huduma ya Kanisa la Siri. Baada ya miaka miwili, yaani mwaka 1959, alikamatwa tena na kuhukumiwa kifungo cha miaka ishirini na mitano.

Alifunguliwa tena kutokana na msamaha wa wafungwa mwaka 1964. Lakini tena alirudia huduma yake ya

tayarisha kwa ajili ya huduma ya jinsi hii. Hivyo mimi na mke wangu tulikamatwa mara nyingi, tulipigwa na kuburutwa hata mbele ya mahakimu wa Kinazi. Vitisho vya enzi za Nazi vilikuwa vikuu mno. Lakini huu ulikuwa mwanzc tu wa mateso ya kuogofya chini ya serikali ya Kikomunisti. Mwanangu Mihai aliitwa jina lisilo la Kiyahudi kusudi asiuawe.

Walakini, enzi hizi za Nazi zilikuwa na faida moja kuu. Zilitufundisha kwamba mapigo ya mwili yaweza kuvumiliwa, tena kwamba kwa msaada wa Mungu, roho ya binadamu yaweza kusalimika katika mateso mabaya. Zaidi tulifundishwa ujuzi wa siri ya kazi ya Kikristo, ambayo yalikuwa ni matayarisho maalum kwa ajili ya mateso maovu – mateso yaliyokuwa mbele yetu.

**Huduma Yangu kwa Warusi.**

Kutokana na majuto ya kuwa mtu amkanaye Mungu, nilipata uchu wa kupenda kuwashuhudia Warusi tangu siku ya kwanza ya kuokolewa kwangu. Warusi ni watu wanaofundishwa kuwa hakuna Mungu tangu utoto. Hivyo nia yangu kuu ya kuwahubiri Warusi ilikuwa imetimizwa. Nia hii ilitimizwa hata wakati wa enzi za Nazi, sababu katika nchi ya Rumania palikuwa na maelfu ya Warusi mateka wa vita, nasi tuliweza kufanya shughuli za Kikristo miongoni mwao.

Hii ilikuwa kazi ya shani na ya kusisimua. Wala sitasahau kamwe mara yangu ya kwanza kupambana na mfungwa Mrusi. Aliniambia alikuwa fundi-mitambo. Nami pale pale nilimwuliza iwapo alimwamini Mungu. Kama angejibu "hapana" nisingejali zaidi. Kwani ni haki kwa kila mtu kuamini au kutokuamini. Lakini Mrusi yule nilipomwuliza iwapo alimwamini Mungu, yeye alinikazia macho pasipo kufahamu lile nililosema, ndipo akajibu, "Sina amri ya kijeshi ya namna hiyo. Nikipewa amri kama hiyo nitaamini."

Niliposikia vile machozi yalinidondoka! Nilijisikia moyo wangu umeraruriwa vipande vipande! Kwani mbele

yangu alisimama binadamu ambaye mawazo yake yalikuwa yamekufa. Mtu ambaye alikuwa amepoteza karama kuu iliyotolewa na Mungu kwa binadamu, yaani kila binadamu awe mtu kamili bi nafsi. Lakini huyu akili zake zililemazwa na mafunzo ya Kikomunisti, kwamba hata kuamini au kutokuamini ilikuwa sharti angojee sheria. Hakuwa tena mtu wa kutegemea mawazo yake mwenyewe. Hivyo ndivyo walivyo Warusi wa kawaida baada ya kutawaliwa na Ukomunisti muda wa miaka mingi. Baada ya fadhaa kuu ya kuona vile ukomunisti unavyowatendea binadamu, nilimwahidi Mungu kwamba nitatoa maisha yangu wakf kwa ajili ya watu hawa ili kuwarudishia ubinadamu wao, na kuwafanya wamwamini Mungu na Kristo.

Haikuwa lazima niende Urusi kusudi kuwahubiri Warusi. Maana tangu tarehe 23 Agosti 1944, askari milioni moja wa Kirusi waliingia katika nchi ya Rumania. Na baada ya muda mfupi, Wakomunisti waliitawala nchi yetu Rumania. Mara moja yalianza mateso makali kuzidi yale ya enzi za Nazi!

Wakati ule nchi ya Rumania ilikuwa na watu milioni kumi na nane, lakini chama cha Kikomunisti kilikuwa na wanachama kumi elfu tu. Lakini Waziri wa Urusi wa Mambo ya Nje, Bwana Vishinsky, alishambulia ofisi ya Mfalme wetu mpendwa, Mfalme Michael I. Bwana Vinshinsky aligongagonga mezani kwa ngumi hali akimngurumia Mfalme Michael, "Ni lazima Wakomunisti wawekwe katika shughuli za serikali!" Jeshi letu na polisi walinyang'anywa silaha. Hivyo kwa nguvu, tena wakichukiwa na kila mtu, Wakomunisti walitawala Rumania.

Watu wanahusika mbele za Mungu kwa ajili ya dhambi zao mmoja mmoja bi nafsi, na tena wanahusika kwa ajili ya dhambi za taifa lao zima vile vile. Ndivyo hata mioyo ya Wakristo Waafrika, Waamerika, Waingereza, Waasia inavyohusika na Msiba wa mataifa yaliyotekwa na ukomunisti. Wakristo wote duniani ni lazima

kujidhabihu ili kuwaleta wafungwa hawa katika nuru ya Kristo.

**Lugha ya Upendo yafanana na Lugha ya Kushawishi.**

Mara baada ya Wakomunisti kutawala, kwa ujanja mwingi walitumia maneno ya kushawishi kanisa. Kweli lugha ya upendo yafanana na lugha ya kushawishi! Mvulana atakaye kuposa msichana wa ndoa, na yule atakaye msichana kwa usiku mmoja tu ndipo baadaye amtupilie mbali, wote husema, "Ninakupenda sana dada!"

Yesu Kristo ametufundisha kupambanua baina ya lugha ya upendo na lugha ya kushawishi. Vile vile ametufundisha kupambanua baina ya mbwa-mwitu waliovaa ngozi za kondoo na kondoo halisi.

Lakini wakati Wakomunisti walipotawala, maelfu ya mashemasi, makasisi, wachungaji na Maaskofu hawakupambanua tofauti baina ya sauti zile mbili.

Wakomunisti waliitisha mkutano wa Wakristo wa madhehebu yote katika jumba la Bunge la nchi yetu. Waliohudhuria walikuwa watu elfu nne, mashemasi, makasisi, maaskofu na wengineo toka madhehebu ya nchi nzima. Mapasta na Maaskofu wale elfu nne walimchagua Mkuu wa Urusi wa wakati ule, Bwana Joseph Stalin, kuwa Raisi wa Heshima wa mkutano ule. Kumbe wakati ule Joseph Stalin alikuwa Raisi wa Chama cha Watu Wasiomcha Mungu Duniani, na hivyo kiongozi wa mauaji ya Wakristo. Kila mmoja wa Mapasta na maaskofu wale elfu nne alisimama katika jengo la Bunge akitangaza kwamba ukomunisti na Ukristo kwa asili ni sawa, na yote mawili yaweza kushirikishwa! Kila mmoja wa Makasisi waliohudhuria alisimama akisifu ukomunisti, na kuhakikisha utii wa kanisa kwa serikali mpya.

Mimi na mke wangu tulihudhuria mkutano ule. Mara moja mke wangu aliyekuwa ameketi kando yangu alininong'onezea, "Richard! Simama uoshe aibu hii toka

usoni mwa Kristo! Wanamtemea mate Kristo usoni!

Nilimjibu mke wangu, "Nikifanya vile, utapoteza mumeo!"

Pale pale alinikazia macho, akiwa kimya kwanza, ndipo akasema. "Sipendi mtu mwoga kuwa mume wangu!"

Ndipo nilisimama na kuhutubia mkutano huu. Sikuwasifu wauaji wa Wakristo, bali nilimsifu Kristo na Mungu nikikaza kwamba, ni lazima kumtii Mungu kwanza. Hotuba zote katika mkutano huu zilikuwa zikitangazwa katika redio pale pale. Hivyo nchi yote, watu waliweza kusikia ujumbe huu wa Kristo kutoka katika mimbara ya Bunge la Kikomunisti. Naam! Ingawaje baadaye niliteswa vibaya kwa ajili ya ujumbe huu, lakini yalikuwa malipo yaliyostahili.

Viongozi wa madhehebu mengi walijitahidi kushindana, kila mmoja akionyesha vile alivyojitoa kufuata ukomunisti. Askofu mmoja aliweka alama ya nyundo na mundu katika joho lake, tena akawakataza Mapasta wake kumwita "Mheshimiwa Askofu", bali wamwite "rafiki (komredi) Askofu."

Siku moja nilihudhuria mkutano wa Viongozi wa Makanisa ya Kibaptisti katika mji wa Resta. Mkutano ulifanyika chini ya bendera nyekundu ya kikomunisti, ikipepea. Tena wimbo wa taifa wa Kirusi ulipigwa, kila mtu amesimama. Raisi wa Makanisa ya Kibaptisti alitangaza kwamba Stalin hakufanya jambo jingine lo lote isipokuwa kutimiza amri za Mungu! Alimsifu Stalin kuwa mwalimu mkuu wa Biblia!

Makasisi Patrascoiu na Rosianu walijitoa zaidi hata wakawa maofisa katika kikosi cha polisi wa siri. Askofu Rapp, Makamu wa Askofu wa Kanisa la Kiluteri katika Rumania alianza kufundisha katika Seminari kwamba Mungu ametoa ufunuo mara tatu. Ufunuo wa kwanza ulitolewa kwa Musa. Ufunuo wa pili ulitolewa kwa Yesu. Na ufunuo wa tatu ulitolewa kwa Stalin,

na huo wa Stalin unazidi ufunuo huu mwingine uliotangulia!

Lakini ni lazima ifahamike wazi kwamba baadhi ya ya Wabaptisti halisi hawakukubaliana na mafunzo haya. Bali walikaa waaminifu kwa Kristo, wakiteseka sana. Walakini, Wakomunisti huwachagulia viongozi wa makanisa yao, na Wabaptisti hawa hawana sauti isipokuwa kuwakubali wale viongozi wachaguliwao.

Wale viongozi na Wakristo wanaokuwa watumishi wa ukomunisti badala ya kumtumikia Kristo, huwasuta na kuwashtaki ndugu zao Wakristo wasiowafuata.

Kama vile Wakristo Warusi walivyoanza Kanisa la Siri baada ya mapinduzi ya Kirusi, vivyo hivyo viongozi wa Kanisa katika Rumania walilazimika kuanzisha Kanisa la Siri baada ya Ukomunisti kuingia nchini. Kanisa la Siri lilikuwa na shabaha maalum, yaani *kuhubiri Injili halisi ya Kristo, kwa uaminifu, na kuleta watoto kwa Kristo.* Wakomunisti walizuia mambo haya. Hata kanisa la kawaida lililoruhusiwa lilikubaliana na sheria hiyo ya kupinga.

Mimi pamoja na wengine tulishirikiana kuanzisha Kanisa la Siri. Kwa sababu kwa nje mimi niliheshimiwa, hivyo heshima hiyo ilinikinga vyema na shughuli zangu za Kanisa la Siri. Mimi nilikuwa Pasta wa Kanisa la Kiluteri la Norway, tena niliwakirisha Umoja wa Makanisa ya Dunia (World Council of Churches) nchini Rumania. (Katika nchi ya Rumania hatukufahamu io lote kwamba Umoja wa Makanisa ya Dunia uliunganika na Wakomunisti). Hivyo vyeo hivi viwili vilinikinga vizuri mbele ya watawala ambao hawakufahamu kazi zangu za siri.

Shughuli za Kanisa la Siri zilikuwa za namna mbili hasa.

Kwanza, utumishi wetu wa siri ulikuwa miongoni mwa askari milioni moja wa Kirusi waliokuwa Rumania.

Pili, utumishi wetu wa siri ulikuwa miongoni mwa wafungwa mateka wa Kirumania.

**Warusi ni Watu Wenye Roho za Kiu.**

Kwangu mimi, kuwahubiri Warusi ni furaha kuu ya mbinguni. Ingawa nilikwisha kuhubiri Injili kwa watu wa mataifa mengi mbali mbali, lakini nilikuwa sijapata kuona watu wenye roho za kiu ya Injili kama Warusi. Kweli wana roho za kiu hasa, na wanakunywa Injili.

Siku moja rafiki yangu Pasta Mkristo halisi alinipigia simu kwamba afisa mmoja Mrusi alifika kwake kutubu. Rafiki yangu Pasta hakufahamu Kirusi, hivyo alimpa anwani yangu maana alifahamu kuwa nakielewa. Ndipo keshoye, yule ofisa wa Kirusi alifika kwangu. Ofisa huyu alionekana kumpenda Mungu, alimtafuta Mungu; lakini alikuwa bado hajaona Biblia! Tena alikuwa bado hajahudhuria ibada yo yote ya Kikristo, maana katika Urusi, kanisa ni haba mno. Hakuwa na mafunzo yo yote ya Neno la Mungu. Ofisa huyu wa Kirusi alimpenda Mungu pasipo kumfahamu.
Mungu pasipo kumfahamu.

Mara moja nilianza kumsomea Mahubiri ya Mlimani na Mifano ya Bwana Yesu. Alipoyasikia maneno yale, alirukaruka chumbani akiwa katika furaha ya ajabu!

"Mbona maneno haya ni mema ajabu! Je, niliwezaje kuishi pasipo kumfahamu huyu Kristo?" Ofisa alisema hali akiendelea kufurahi.

Hii kwangu ilikuwa mara ya kwanza kumwona mtu amejaa furaha kuu katika Kristo. Ndipo bila kujua nilifanya kosa moja! Nilimsomea habari za mateso na kusulibiwa kwa Kristo kabla sijamtayarisha kupokea neno hili. Ofisa huyu hakutumaini kusikia vile. Mara aliposikia jinsi Kristo alivyopigwa, alivyosulibiwa mpaka akafa, ghafula alilia machozi kitini mwake! Huyu ofisa alikuwa amemwamini Mwokozi, kumbe Mwokozi wake sasa amekufa!

Afrika ya Kati. Hivyo lugha yao haina neno "theluji." Kwa hiyo aya ile ilitafsiriwa hivi:

"Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama tui la nazi."

Hivyo nasi ilitubidi kutafsiri Injili katika lugha ya Kikomunisti kusudi waelewe. Sisi peke yetu hatukuwa na uwezo wa kufanya neno kama hili, bali Roho Mtakatifu alifanya kazi yake kwa kututumia.

Yule Kapteni na ofisa mwanamke waliokolewa siku ile ile. Nao baadaye walikuwa msaada mkuu kwetu katika shughuli za kuwahubiri Warusi kwa siri.

Kwa siri tulichapa na kueneza maelfu ya Injili na vijitabu vingi vya Kikristo katika sehemu za Warusi. Kwa siri tuliweza kuingiza Biblia na vitabu vingine katika nchi ya Urusi kwa njia ya msaada wa askari wa Kirusi waliompokea Kristo.

Vile vile tulitumia njia nyingine ya kuwapa Warusi vitabu vingi vya Neno la Mungu. Askari wa Kirusi walikuwa wakipigana kwa miaka mingi nje ya nchi yao. Na wengi wao walikuwa wameacha watoto wao nyumbani kwa muda huu wote. (Kweli Warusi huwapenda sana watoto.)

Hivyo mwanagu Mihai pamoja na watoto wengine wengi waliokuwa chini ya umri wa miaka kumi waliwatembelea askari wa Kirusi po pote. Watoto hawa walichukua Biblia, Injili na vitabu vingine katika mifuko yao. Kwa vile askari hawa waliwapenda watoto, waliwakumbatia na kuwabembeleza wakiwapigapiga vichwani, wakizungumza nao kwa upendo, waliwapa vyakula kama pipi na vitu vingine, wakikumbuka watoto wao waliowaacha nyumbani. Ndipo watoto hawa nao walitoa Biblia au Injili na kuwapa hawa askari Warusi. Mara nyingi tendo lile lililokuwa hatari kwetu kutenda wazi wazi, watoto wetu walilitenda kwa usalama kamili. Watoto hawa walikuwa wamissionari vijana kwa Warusi.

Matokeo yake yalikuwa mazuri ajabu. Askari wengi wa Kirusi walipokea Injili kwa njia hii wakati njia nyingine yo yote iliposhindwa kufaulu.

## Kuhubiri katika Kambi za Jeshi la Kirusi.

Hatukufanya kazi miongoni mwa Warusi kwa kushuhudia mtu mmoja mmoja tu, bali tuliweza kukutanika katika vikundi vidogo vidogo pia.

Warusi walipenda sana saa. Waliiba na kunyang'anya saa toka kila mtu waliyekutana naye barabarani. Ungewaona Warusi wakiwa na saa kadhaa mikononi. Ungeweza kuwaona ofisa wanawake Warusi wamening'niza shingoni mwao saa kubwa za mezani. Wengi wao walikuwa hawajapata kuwa na saa, wala wasingepata za kuwatosha. Warumania waliotaka saa waliingia katika kambi za askari Warusi na kununua zile zilizoibiwa, mara nyingine walinunua saa zao tena. Hivyo ilikuwa kawaida kwa Warumania kuingia kambi za askari wa Kirusi. Hata sisi watumishi wa Kanisa la Siri tulikuwa na udhuru maalum "kununua saa" kusudi kuingia kambini.

Kwa mara yangu ya kwanza nilichagua kuhubiri ikiwa siku kuu ya Watakatifu Paulo na Petro. Hivyo niliingia katika kituo cha jeshi kwa kujifanya kwamba nataka kununua saa. Nilijisingizia kusema kwamba saa moja ilikuwa ghali sana, na nyingine ilikuwa ndogo mno na nyingine ati ilikuwa kubwa kupita kiasi. Askari wachache walinizunguka, na kila mmoja akinionyesha kitu cha kununua. Ndipo kwa namna ya mzaha niliwauliza, "Je pana mmoja wenu hapa anayeitwa Paulo au Petro?"

"Ndiyo!" Waliitikia kwamba walikuwapo akina Paulo na Petro.

Nilizidi kuwauliza tena, "Je, mwajua kuwa leo ni

siku ambayo kanisa lenu lawakumbuka Watakatifu Paulo na Petro?"

Baadhi ya Warusi wazee walielewa neno hili wazi. Ndipo tena niliuliza, "Je, mwawafahamu hawa Watakatifu Paulo na Petro ni akina nani?"

Hapakupatikana mtu aliyejibu swali hili. Mara nilianza kuwaeleza habari za Paulo na Petro.

Ghafula, mmoja wa wale askari wazee wa Kirusi alinikata kauli: "Wewe hukuja kununua saa! Umekuja kutuambia habari za imani yako. Basi, njoo, kaa chini hapa pamoja nasi utuambie! Lakini jihadhari! Sisi tunawafahamu watu walio hatari ambao yakupasa ujihadhari nao. Hawa wanaokuzunguka wote ni wema. Lakini kila nikushikapo goti kwa mkono wangu, zungumza habari za saa. Na wakati nikiondoa mkono, endelea na mahubiri yako tena."

Muda si mwingi nilijiona nimezungukwa na kundi kubwa la watu. Nami niliendelea kuwaambia habari za Paulo na Petro, habari za Kristo ambaye Paulo na Petro walikufa kwa ajili yake. Mara moja mtu ye yote wasiyemwamini aliposogea, yule askari alinishika goti, nami pale pale niligeuza mahubiri yangu na kuanza kuzungumza habari za kununua saa. Mtu yule akienda zake, ndipo ninarudia tena kuhubiri habari za Kristo. Mtido huu wa kuhubiri uliendelea mara nyingi kwa msaada wa askari Warusi Wakristo. Kwa njia hiyo, ndugu zao wengi walimwamini Kristo. Tena vijitabu vingi vya Injili viligawiwa kwa siri.

Baadhi ya ndugu na dada zetu wa Kanisa la Siri walishikwa na kupigwa sana kwa sababu hii, walakini hawakusaliti chama chetu.

Katika kazi tulikuwa na shangwe ya kuonana na ndugu zetu wa Kanisa la Siri la Urusi. Tulifurahi mno kusikia habari na matendo yao. Kwanza walionekana kuwa kama watakatifu wakuu. Kwa muda wa miaka

mingi walikuwa wamepita katika mafunzo ya Kikomunisti. Baadhi yao walikuwa wameingia hata katika vyuo vikuu vya Kikomunisti. Lakini kama vile samaki aishivyo katika bahari ya chumvi pasipo kupoteza ladha yake, Wakristo hawa pia walifunzwa katika shule za Kikomunisti, lakini walitunza roho zao safi na takatifu katika Kristo.

Wakristo hawa wa Kirusi walikuwa na roho safi ajabu! Walisema, "Twafahamu wazi nyota hii na nyundo pamoja na mundu vilivyo kwenye kofia zetu ni alama ya mpinga-Kristo!" Haya waliyasema kwa masikitiko makuu. Na hawa ndio waliotusaidia sana kueneza Injili kwa askari wengine wa Kirusi.

Mimi naweza kusema hawa Wakristo Warusi walikuwa na nguvu zote za Kikristo, kasoro furaha tu! Furaha waliipata wakati wa mazungumzo tu, ndipo ilitoweka baada ya mazungumzo. Neno hili lilinishangaza sana! Hata mwishowe nilimwuliza Mkristo wa Kibaptisti, "Mbona huna furaha kamili?"

Naye pasipo kusita alinijibu, "Je, yawezekanaje niwe mwenye furaha kamili maadam ninamwogopa hata Pasta wa kanisa yangu asigundue kuwa mimi ni Mkristo mwaminifu, niombaye na kuhubiri wengine Injili ya Kristo? Maana Pasta ni askari wa siri wa polisi. Tunapelelezwa mno kila mmoja, na Wachungaji ndio wasaliti wa kundi! Sisi tunayo furaha kuu ya Wokovu ndani yetu, lakini furaha hii ya nje uliyo nayo wewe, sisi hatuwezi kuipata.

"Kwetu sisi Ukristo limekuwa jambo la shani limpatalo mtu. Wakati ninyi Wakristo mnapomleta mtu kwa Kristo, mtu yule huingia katika Kanisa hai na tulivu. Bali sisi tunapomleta mtu kwa Kristo, tunafahamu kuwa atatupwa gerezani, tena kwamba watoto wake watabaki yatima. Hivyo shangwe ya kumleta mtu kwa Kristo imechanganyika na mawazo kwamba kila mara pana gharama kubwa ya kulipwa!"

Naam! Tulikuwa tumekutana na namna mpya ya Wakristo – Wakristo wa Kanisa la Siri. Tulishangazwa mno! Kama vile watu wengi wanavyojidhani kwamba ni Wakristo, kumbe kwa kweli sivyo; ndivyo sisi tulivyoona kuwa miongoni mwa Warusi pana wale wanaojifikiri kwamba sio Wakristo, kumbe kwa kweli ni Wakristo.

Siku moja nilikutana na watu wawili, mume na mke, wote fundi wa kuchonga sanaa. Wakati nilipozungumza nao habari za Mungu, nilipata majibu ya ajabu!

"Hasha! Hakuna Mungu! Sisi tu 'Bezboshniki'–tusio na Mungu. Lakini tutakusimulia kisa kimoja cha kushangaza tulichokiona siku moja.

"Wakati fulani tulikuwa tukichonga sanamu ya Stalin. Ndipo wakati ule wa kazi, mke wangu aliniuliza: 'Mume wangu, wafikirije juu ya kidole gumba? Kama tusingekuwa na kidole gumba, au tuseme, kama vidole vya miguu ndivyo vingekuwa vidole vya mikono, ni wazi tusingeweza kushika nyundo, kifaa cho chote, kitabu, wala hata kipande cha mkate. Pasipo kidole gumba, maisha ya binadamu yangekuwa ya shida kuu. Sasa ni nani aliyeumba kidole gumba? Wakumbuka sote tulijifunza shuleni elimu ya Kikomunisti kwamba mbingu na nchi zilizuka zenyewe vivi hivi tu, kwamba havikuumbwa na Mungu. Sote tulijifunza vile, na twaamini vile. Hata kama Mungu hakuumba mbingu na dunia, bali aliumba kidole gumba, basi ni lazima atukuzwe kwa ajili ya hiki kidole gumba kidogo.

" 'Tunamsifu Edison kwa sababu ya kugundua nguvu ya umeme. Twamheshimu Bell kwa kugundua simu. Twamshangilia na kumsifu Stephenson kwa ajili ya kugundua gari moshi. Mbona basi hatumtukuzi aliyeumba kidole gumba? Kama Edison asingekuwa na kidole gumba, bila shaka asingevumbua cho chote. Ni haki tupu kumwabudu Mungu aliyeumba kidole gumba.' "

Mumewe alikasirika ajabu baada ya kusikia hekima bora ya mkewe. Hivi ndivyo wanaume wengi wafanyavyo baada ya wake zao kuwaambia mambo ya hekima.

"Usiseme upumbavu hapa! Umejifunza kwamba hakuna Mungu. Huwezi kujua kama mji wetu hautavurugwa, na kama hatutakuwa katika matata. Milele, zingatia tena akilini mwako kwamba hakuna Mungu. Mbinguni hakuna ye yote!"

Naye mkewe alijibu, "Huu ni upeo wa miujiza! Kama mbinguni palikuwa na Mwenyezi Mungu ambaye babu zetu walimwamini kwa upumbavu, hivyo ni neno la kawaida kwetu kuwa na vidole gumba. Lakini Mwenyezi Mungu aweza kufanya kila neno, kwa hiyo aliweza kuumba hata kidole gumba. Na kama mbinguni hakuna ye yote, mimi kwa upande wangu nimekata shauri kwa moyo wangu wote kumwabudu huyu "Hakuna ye yote" kwa maana aliumba kidole gumba.

Hivyo wote wawili mume na mke walimwabudu huyu "Hakuna ye yote." Imani yao katika Mungu huyu "Hana ye yote" iliongezeka zaidi, wakiamini kuwa ndiye aliyeumba kidole gumba, nyota, maua, watoto na vitu vingine vyema duniani.

Neno hili lilikuwa kama lile la zamani katika mji wa Athene wakati Mtume Paulo alipowakuta watu wakimwabudu "Mungu Asiyejulikana."

Watu hawa wawili mume na mke walifurahi sana kusikia nikiwaeleza vile imani yao ilivyokuwa ya kweli. Maana mbinguni "Hakuna ye yote," bali kuna Mungu aliye Roho. Nilizidi kuwaambia vile Mungu alivyo Roho wa upendo na hekima, Roho wa kweli na nguvu ambaye aliwapenda upeo hata akamtuma Mwanawe kujitoa kafara msalabani kwa ajili yao.

Ndugu hawa walimwamini Mungu pasipo kufahamu. Mimi nilikuwa na majaliwa kuwasogeza mbele hatua moja, nayo ni kutambua wokovu na kuokolewa.

Siku moja nilikutana barabarani na Ofisa mwanamke Mrusi. Nilisogea karibu na kumwomba radhi nikisema, "Naelewa siyo heshima bora kumsalimia bibi usiye-

mfahamu, hasa ikiwa ni barabarani kama hivi. Lakini mimi ni Pasta, na nia yangu ni njema, nayo ni kukwambia habari za Kristo."

Naye pale pale aliniuliza, "Kweli unampenda Kristo?"

"Ndiyo! Nampenda Kristo kwa moyo wangu wote."

Ghafula, yule bibi aliruka akanikumbatia na kunibusu tena na tena. Ilikuwa hali ya kushangaza sana mwanamke kumbusu Pasta barabarani. Hivyo hata mimi nilimbusu vile vile nikitumaini kwamba watu watafikiri ni jamaa yangu.

Yule ofisa mwanamke alisema kwa kuchangamka mno. "Hata mimi nampenda Kristo vile vile."

Mara moja nilimkaribisha nyumbani kwetu. Ndipo baadaye niligundua kuwa hakufahamu habari yo yote juu ya Kristo, kusema kweli hakujua lo lote! isipokuwa jina tu! Walakini alimpenda! Mwanamke huyu ofisa hakufahamu Mafundisho ya Kristo, wala maisha na utumishi wake. Jambo hili liliamsha silika yangu ya upelelezi. Je, yawezekanaje kumpenda mtu fulani kwa kufahamu jina lake tu?

Nilipozidi kupeleleza, huyu bibi alinitobolea siri yote. Alisema, "Nilipokuwa mtoto mchanga nilijifunza kusoma picha. Mahali pa neno 'kiti', palikuwa na picha ya kiti. Na mahali pa neno 'chatu', palikuwa na picha ya chatu. Mahali pa neno "saa', palikuwa na picha ya saa. Na mahali pa neno 'bata', palikuwa na picha ya bata, na kuendelea vivyo.

"Hata wakati nilipoingia katika shule za juu, nilifundishwa kwamba wajibu wetu mtukufu.ni kuilinda nchi ya babu zetu ya Kikomunisti. Nilifunzwa maadili ya kikomunist. Lakini sikufahamu sura ya 'wajibu mtukufu' wala 'maadili.'

"Mimi sasa nafahamu kuwa babu zetu walikuwa na picha kwa kila neno zuri lenye thamani na manufaa

maishani. Nyanya yangu alikuwa akipiga magoti mbele ya sanamu moja akisema kwamba ilikuwa picha ya mtu aliyeitwa Kristo. Mimi nilipenda jina hili peke yake maana lilijitokeza kuwa kitu halisi machoni pangu. Maana yake ni kwamba jina hili lampa mtu furaha kuu."

Wakati nilipokuwa nikimsikiliza, nilikumbuka habari iliyoandikwa katika Wafilipi, kwamba kwa jina lake kila goti litakunjwa. Pengine kwa muda mfupi tu, Mpinga-Kristo ataweza kuondolea mbali elimu ya kumfahamu Mungu. Lakini hata hivyo kuna nguvu tele katika Jina Hili la Kristo. Na nguvu hii itaongoza mpaka katika nuru ya utambuzi

Ofisa huyu mwanamke, kwa furaha isiyokadirika alimpokea Kristo pale pale nyumbani kwetu. Sasa jina ambalo alilipenda lakaa ndani yake katika nafsi kamili ya Kristo.

Hivyo kwangu kila wakati niliokaa na Warusi, ulikuwa tamasha iliyojaa utenzi na maana kuu.

Kwa mfano. Dada mmoja aliyekuwa akieneza Injili katika kituo cha gari la moshi alimpa Ofisa fulani anwani yangu.

Ndipo siku moja jioni, Ofisa yule alifika nyumbani kwetu. Alikuwa kijana Mrusi, mrefu na malidadi kweli, tena mwenye cheo cha juu jeshini, (Lieutenant.)

Baada ya kusalimiana naye na kuketi, nilimwuliza, "Je, naweza kukusaidia kwa njia gani?"

Ofisa yule alijibu, "Nimekuja ili kupata nuru."

Pale pale nilianza kumsomea vifungu maalum katika Maandiko Matakatifu. Ndipo Ofisa huyu alinishika mkono na kusema, "Tafadhali nakusihi kwa moyo wangu wote usinipotoshe. Mimi ni mmoja wa watu walio gizani. Niambie tafadhali, je hili ni Neno la Mungu kweli?"

Mara moja nilimhakikishia kuwa kweli hili ni Neno la Mungu. Naye alisikiliza muda mrefu, na baadaye akamwamini Kristo.

Kwa jumla, Warusi hawashughuliki na mambo ya dini kwa juu juu tu. Warusi hutia nia yao yote katika shughuli yo yote, iwe ni kupigana kupinga dini, au kuipenda dini na kumtafuta Kristo. Ndiyo sababu katika Urusi, kila Mkristo ni mwinjilisti atafutaye kuokoa roho za watu. Na hii tena ndiyo sababu nchi ya urusi iko tayari kupokea Injili. Warusi ni baadhi ya miongoni mwa watu wachukuao dini kuwa jambo la asili. Kutatokea badiliko kuu duniani kama tutawapa warusi Injili kwa juhudi kuu.

Ni jambo la msiba mkuu kuona kwamba watu wengi wamefuta mawazoni utumishi wa Injili kwa Wakomunisti. Kumbe nchi ya Urusi na watu wake wana njaa kuu ya Neno la Mungu.

Siku moja nilipokuwa nikisafiri katika gari la moshi, Ofisa Mrusi aliketi mbele yangu. Nilizungumza naye habari ya Kristo muda wa dakika chache. Ndipo yeye alipinga vikali akidondoa maneno ya kupinga Biblia yaliyotumiwa na Marx, Stalin, Voltaire, Darwin na wengineo. Hakunipa hata dakika moja ya kuzungumza kwa ajili ya wingi wa maneno ya kupinga yaliyomtiririka kama maji ya mto. Ofisa huyu alifuliza mazungumzo muda wa saa nzima akinishawishi niamini kuwa hakuna Mungu.

Wakati aliponyamaza ndipo nilipata nafasi ya kumwuliza swali. "Kama hakuna Mungu, mbona huwa unaomba wakati unapokuwa katika shida?"

"Je, wajuaje kuwa huwa ninaomba?" Aliniuliza akijaribu kukwepa swali.

"Kwanza jibu swali langu. Mimi nilikuuliza kwanza, kwa nini waomba? Tafadhali nijibu!" Nilisisitiza sana kusudi asiepuke swali langu.

"Ndiyo! Tulipokuwa tumezungukwa na Wajerumani vitani, sote tuliomba! Hatukujua jinsi ya kuomba, lakini tuliomba. Sote tulisema, 'Mungu na roho ya mama... !"

Kwa kweli hii ni sala nzuri ya maombi machoni pa Yule atazamaye mioyo ya watu.

Utumishi wetu miongoni mwa Warusi umetoa mazao mengi zaidi. Nakumbuka kijana mmoja ajulikanaye kwa jina la Petro. Hapana mtu afahamuye kijana huyu alikufa katika gereza gani la Kirusi. Alikuwa kijana mdogo wa miaka kama ishirini hivi. Kijana Petro aliingia nchini Rumania akiwa katika jeshi la Kirusi. Wakati alipookolewa na Kristo katika mkutano mmoja wa siri, ndipo aliniomba nimbatize.

Baada ya ubatizo, nilimsihi atueleze kifungu cha Maandiko katika Biblia kilichomchoma zaidi na kumleta kwa Kristo.

Kijana Petro alisema kwamba siku moja katika mkutano wa siri alinisikiliza kwa makini sana wakati niliposoma katika Injili ya Luka Sura 24. Habari yenyewe ilikuwa hadithi ya Yesu alipokuta wanafunzi wawili wakisafiri kwenda Emmau. Wakati walipokaribia kijiji, Yesu alionekana kama alitaka kuendelea mbele.

Petro alizidi kueleza, "Nilishangaa kwa nini Yesu alisema maneno haya! Kweli alitaka kukaa na Wanafunzi wake! Mbona basi yasemekana kuwa alitaka kuendelea mbele?"

Maelezo yangu yakuwali kwamba Yesu ni mpole. Alitaka sana kuhakikisha kwamba walimhitaji. Na wakati alipoona kuwa walimkaribisha, aliingia nao nyumbani kwa furaha. Wakomunisti sio wapole. Wao huingia kwa nguvu na ukali katika mioyo na akili zetu. Wanatulazimisha tuwasikilize wao tu tangu asubuhi hadi usiku. Wanafanya hivyo katika shule, redio, magazeti, matangazo, senema, katika mikutano ya kupinga na mahali po pote. Utake usitake, ni lazima kila mara usikilize maenezi ya maneno yao yamkanayo Mungu.

"Lakini Yesu huheshimimu uhuru wetu. Yeye hugonga mlangoni kwa utulivu sana. Yesu Kristo alinivuta kwake kwa njia ya heshima na upole wake," Petro alikaza usemi wake kwa mafafanusi ya aya hizo.

Petro hakuwa Mrusi pekee aliyevutwa sana na tabia hii katika maisha ya Yesu. (Mimi nikiwa Pasta, nilikuwa bado sijafikiri neno hili jinsi hii.)

Baada ya kuokolewa kwake, Petro alijitoamaisha yake mara nyingi kusafirisha kwa siri Biblia na misaada mingine ya Kanisa la Siri kutoka Rumania kuingia Urusi. Mwishowe alikamatwa. Nafahamu mwaka 1959 alikuwa angali bado gerezani. Kama amekwisha kufa na kwenda mbinguni, au kama bado apigana vita yake bora hapa dunianі, mimi sijui. Ni Mungu pekee ndiye ajuaye mahali alipo Petro leo hii.

Pana watu wengi kama Petro ambao hawakutulia baada ya kuamini. Kuleta roho kwa Kristo sio mwisho wa kazi. Hii ni sehemu tu ya kazi. Kila roho iletwayo kwa Kristo ni lazima nayo ifunzwe jinsi ya kuleta roho nyingine kwa Kristo. Warusi hawakuamini tu, bali walikuwa wajumbe wa kutangaza Injili katika Kanisa la Siri. Tena walikuwa hodari na shupavu kwa ajili ya Kristo, kila mara wakisema kwamba hata huduma yao hiyo ilikuwa ndogo mno kulinganisha na vile Kristo alivyokufa kwa ajili yao.

**Huduma Yetu Ya Siri Katika Taifa Lililotekwa.**

Sehemu nyingine ya kazi yetu ya ujumbe wa siri wa Injili ilikuwa miongoni mwa Warumania wenyewe.

Baada ya muda mfupi tu Wakomunisti walivivua vinyago vyao na kudhihirisha tabia yao wazi wazi. Mwanzoni waliwashawishi Waongozi wa Makanisa ili wawe upande wao. Lakini mara moja hofu kuu ilitukia. Maelfu ya watu walikamatwa. Hata sisi pia tuliona ni tamasha kuu kumleta mtu kwa Kristo kama vile ilivyokuwa kwa Warusi wenyewe.

Mimi mwenyewe mwishowe nilitupwa gerezani pamoja na watu wale ambao Mungu alikuwa amenisaidia kuwaleta kwa Kristo. Nilikuwa gerezani katika kijumba pamoja na mtu mmoja aliyeacha mkewe na watoto wake

sita. Sasa alikuwa amefungwa gerezani kwa ajili ya imani yake katika Kristo. Mkewe na watoto walikuwa wakifa kwa njaa. Pengine hatawaona tena! Ndipo nilimwuliza, "Je, wanichukia kwa sababu nilikuleta kwa Kristo, na kwa ajili hiyo jamaa yako yateseka?"

Naye alijibu, "Sina maneno yawezayo kutosha kukushukuru vile ulivyonileta kwa Mwokozi huyu wa ajabu. Maana yake isingaliwezekana kwa njia nyingine."

Haikuwa rahisi kumhubiri Kristo katika hali ya dhiki kama hii. Kweli tulifaulu kuchapisha vijitabu vya Neno la Mungu kwa shida, hata hivyo baada ya kuchunguzwa kwa uangalifu mwingi na Wakomunisti. Tulimpa Mkomunisti mchunguzaji wa maandishi, vijitabu vilivyokuwa na picha ya Karl Marx, yule mwanzishaji wa ukomunisti. Vitabu hivi viliitwa DINI NI BANGI YA WATU na majina mengine. Mchunguzi huyu alividhania kuwa vitabu vya Kikomunisti, akavipiga mhuri na kuviruhusu vitumike. Kurasa chache za kwanza za vitabu hivi zilikuwa na maneno yaliyotamkwa na Marx, Lenin na Stalin ambayo yalimfurahisha mchunguzi. Lakini katika kurasa nyingine vyingi tulihubiri ujumbe wa Kristo.

Kanisa la Siri lafanya kazi, sehemu kwa siri na sehemu kwa wazi. Ni kama gogo lielealo majini, sehemu hutokeza nje, na sehemu huzama majini. Tulikwenda kuona maonyesho ya Kikomunisti na kugawa hivi vijitabu vya "kikomunisti". Wakomunisti walipoona picha ya marx katika jalada, kila mtu alipigana kukinunua. Wakati waliposoma kufikia ukurasa wa kumi ndipo kugundua kwamba kitabu chote kilieleza habari ya Mungu na Yesu, sisi tulikuwa tumefika mbali sana kutoweka.

Kuhubiri Neno la Mungu katika hali kama hii siyo rahisi kamwe. Watu wetu waliteswa vibaya. Wakomunisti walimnyang'anya mtu ye yote, kitu cho chote kile. Mkulima alinyang'anywa shamba na mifugo. Kinyozi au

fundi mshonaji alinyang'anywa duka lake. Siyo kwamba ni tajiri tu ndio walioonewa hivi, la, hata fukara waliteswa vibaya ajabu! Karibu kila jamaa ilikuwa na mtu aliyetupwa gerezani, isitoshe, ufukara ulikuwa wa kutisha! Hata baadhi ya watu hujiuliza, "Inakuwaje Mungu mwenye upendo kuruhusu uovu huu kufaulu?"

Wala isengalikuwa rahisi kwa mitume wa kwanza kuhubiri habari ya Kristo siku ile ya Ijumaa Kuu, wakati ule Yesu alipokufa msalabani, akilia kwa sauti, "Mungu Wangu! Mungu Wangu! Mbona umeniacha!"

Lakini kwa kuwa kazi ile ilifanyika, ni wazi kwamba huu ulikuwa uwezo wa Mungu wala sio wetu. Imani ya Kikristo tu peke yake ndiyo iwezayo kujibu maswali ya jinsi hiyo.

Bwana Yesu alisimulia habari za maskini Lazaro alivyoteseka wakati ule, (kama vile sisi tulivyoteswa), njaa, vidonda vyake vikilambwa na mbwa, kifo; lakini mwishoni malaika walimpeleka kifuani mwa Ibrahim.

## Jinsi Kwa Sehemu Kanisa La Siri Lilivyotenda Kazi Wazi.

Kanisa la Siri lilikutanika faraghani katika nyumba, vyumba vya chini, mistuni na kila mahali palipowezekana. Katika mikutano ile ya siri, kazi za wazi zilipangwa na kutayarishwa. Chini ya Wakomunisti, tulibuni mpango wa kuhubiri mabarabarani, ingawaje baadaye ilikuwa hatari kuu. Lakini hiyo ilikuwa njia pekee na maalum ya kuwapata wengi ambao wasingesikia.

Mke wangu, Sabena, alikuwa hodari mno katika mpango huu. Baadhi ya Wakristo walikutanika kimya barabarani pembeni, na kuanza kuimba. Ndipo watu walikusanyika kusikiliza zile nyimbo tamu tamu. Halafu mke wangu akahubiri ujumbe wa Kristo haraka, mwisho sote tunaondoka upesi kabla polisi hawajafika.

Alasiri moja mimi nilipokuwa nikishughulika mahali

pengine, mke wangu alikuwa akihubiri maelfu ya wafanya kazi katika lango la kiwanda "MALAXA" mjini Bucharest. Bibi huyu aliwahubiri wafanya kazi hawa habari za Mungu na wokovu mkuu. Keshoye wafanya kazi wengi katika kiwanda kile walipigwa risasi kwa kuasi dhuluma ya Wakomunisti Ajabu kuu Kwani walikuwa wamesikia ujumbe wa Kristo katika wakati uliofaa sana.

Kweli sisi tulikuwa Kanisa la Siri. Lakini kama vile Yohana Mbatizaji, tulihubiri watawala na watu wengine wazi wazi.

Siku moja katika ngazi za kuingilia jengo la serikali yetu, Wakristo wawili walijipenyeza mpaka kumfikia Waziri Mkuu wetu Gheoghiu Dej. Muda ule mfupi waliopata, walimshuhudia na kumhubiri habari ya Kristo, wakimsihi atubu dhambi zake na mateso yale makuu. Waziri Mkuu aliamuru watu wale watupwe gerezani kwa ajili ya ushuhuda wao wa kijasiri.

Baada ya miaka kadhaa, yule yule Waziri Mkuu, Georghiu Dej, aliugua. Ndipo mbegu zile za Injili zilizopandwa ndani yake, na ambazo kwazo wale wapandaji waliteswa, zilizaa matunda. Waziri Mkuu huyu alikumbuka yale maneno aliyohubiriwa. Kama Biblia isemavyo, maneno haya yalikuwa "hai, yenye nguvu, na makali kuliko upanga ukatao kuwili."

Yalikata ule ugumu uliokuwa katika moyo wake mpaka akajitoa kwa Kristo. Aliungama dhambi zake na kumpokea Mwokozi, akaanza kumtumikia hata wakati alipokuwa mgonjwa. Ingawa alikufa baada ya muda mfupi, lakini alikwenda kuonana na Mwokozi wake aliyemwokoa. Hili lilitukia kwa sababu Wakristo wawili walijitoa maisha yao kwa lo lote ambalo lingetokea. Hili ni tendo la kawaida tu la baadhi ya Wakristo wengi walio katika nchi za Kikomunisti leo hii.

Hivyo Kanisa la Siri halikuwa na mikutano wala shughuli za siri tu, bali kwa ujasiri, tena wazi wazi,

lilitangaza Injili ya Kristo katika barabara za Kikomunisti na kwa watawala wa Kikomunisti. Palikuwa na gharama kuu, lakini tulikuwa tayari kabisa kuilipa. Hata leo hii Kanisa la Siri li tayari kulipa gharama yo yote ile.

Askari wapelelezi walilitesa sana Kanisa la Siri, maana walifahamu peupe kwamba hiyo ndiyo njia peke ya kupinga ukomunisti. Kweli hii ni aina maalum ya upingaji, tena upingaji wa kiroho, ambao kama ukiachwa pasipo kuzuiwa, utadhoofisha nguvu yao ya kumkana Mungu. Kama vile Shetani ajuavyo, ndivyo hata Wakomunisti walivyong'amua. Na mara matisho makali yalianza! Walifahamu wazi kwamba mtu anapomwamini Kristo, hapungukiwi tena fahamu hata kuweza kuwa rahisi kudanganywadanganywa. Walijua peupe kwamba waliweza kuwafunga binadamu gerezani, lakini hawakuweza kuifunga imani yao katika Mungu. Hivyo walipigana juu chini ili kukomesha Kanisa la Siri.

Lakini Kanisa la Siri lilikuwa na watu walioli-hurumia, hata serikali ya Kikomunisti na askari polisi wa siri nao vile vile walilihurumia.

Hali kadhalika nasi tuliwafundisha Wakristo kujiunga na kikosi cha siri cha askari polisi. Wakristo hawa walivaa mavazi yale rasmi ya askari, ambayo yalichukiwa vibaya katika nchi nzima. Kazi yao hasa ilikuwa kuchunguza matendo ya askari halisi wa siri, ndipo kutoa taarifa kwa Kanisa la Siri. Baadhi ya ndugu wa Kanisa la Siri walijiunga na kikosi hiki, wakificha imani yao. Siyo rahisi kudharauliwa na jamaa pamoja na rafiki katika nchi yako kwa sababu ya kuvaa mavazi ya Kikomunisti pasipo kuwambia ujumbe wako kamili. Lakini walifanya, walakini walimpenda Kristo sana.

Wakati nilipochukuliwa kwa nguvu barabarani na kulindwa kwa ulinzi mkali, nikiwa mahali pa siri muda wa miaka mingi, Daktari Mkristo aliingia katika kikosi

cha askari wa siri ndipo akanigundua mahali nilipofichwa. Kwa kuwa alikuwa daktari, tena askari wa siri, aliruhusiwa kuingia katika vyumba vya wafungwa wote. Nia na tumaini lake vilikuwa mpaka anigundue. Rafikize wote walimzomea na kumdharau, kuwa amekuwa Mukomunisti Kwa kweli kuzunguka huko na huko katika mavazi ya watesi ni kujitoa dhabihu kuu kwa ajili ya Kristo kuliko kuvaa mavazi ya kifungwa.

Daktari huyu alinigundua nimefichwa katika kichumba cha giza kuu, ndipo akatuma habari kuwa nilikuwa hai bado! Yeye ndiye alikuwa rafiki yangu wa kwanza kunigundua baada ya kuwa kifungoni miaka minane na nusu.

Ilitokana na kujitolea kwa huyu Daktari, kwamba habari zilienea kuwa nilikuwa hai bado. Wakati wafungwa wengi walipofunguliwa kutokana na ruhusa ya Eisenhower pamoja na Khruschev mwaka 1956, Wakristo nao walidai hata mimi niachiwe vile vile. Kweli nilifunguliwa kwa muda Mfupi.

Kama asingekuwa huyu Daktari Mkristo, kuingia kikosi cha polisi wa siri kusudi anitafute, bila shaka nisingefunguliwa. Huenda ningekuwa bado gerezani, au ningekuwa kaburini wakati huu.

Ndugu zetu wa Kanisa la Siri walipokuwa askari wapelelezi, walitumia madaraka yao ili kutuonya. Hivyo walikuwa msaada mkuu mno kwetu. Mpaka hivi leo Kanisa la Siri linao askari katika kikosi cha siri cha polisi ambao huwaonya Wakristo na hatari yo yote ijayo. Baadhi ya askari hawa ni watu wakuu mno katika shughuli za Kikomunisti, bali wanayo imani kuu katika Kristo, nao hutusaidia sana. Siku moja mbinguni watamtangaza wazi Kristo ambaye sasa wanamtumikia kwa siri.

Hata hivyo ndugu wengi wa Kanisa la Siri waligunduliwa na kufungwa. Wapo akina "Yuda Iskariote" ambao hutusaliti kwa askari polisi wa siri. Kwa njia za mapigo, kuburutwa, kutishwa na rushwa, Wakomunisti waliwapata mapasta na Wakristo ili kuwasaliti ndugu zao.

\- - - - - -

SURA YA PILI

# Mateso Na Kuoshwa Akili

Nilifanya kazi zote za siri na za wazi mpaka tarehe 15 Februari, mwaka 1948. Siku hiyo ilikuwa Jumapili – Jumapili bora ajabu ambayo polisi wa siri walinichukua kwa nguvù barabarani wakati nikienda kanisani.

Mara kwa mara nilikuwa nikistaajabia maana ya "kuiba watu," neno ambalo latajwa mara kadhaa katika Biblia. Kumbe ukomunisti umetufundisha maana yake.

Watu wengi watwaliwa kwa nguvu, au kuibwa jinsi hii. Motakae ya polisi wa siri ilisimama mbele yangù. Ndipo watu wanne waliruka nje na kunisukumia ndani! Nilikuwa mateka muda mrefu, zaidi ya miaka minane, wala hapakuwa na mtu aliyefahamu kama nilikuwa hai ama maiti! Polisi wa siri walifika nyumbani kwa mke wangu wakijifanya wafungwa waliofunguliwa. Nao walimwambia kwamba nilikwisha kufa, nao walihudhuria mazishi yangu. Hivyo hata mke wangu alivunjika moyo kweli!

Wakati ule maelfu ya watu toka kanisa nyingi za madhehebu mbalimbali walitupwa gerezani. Waliofungwa gerezani hawakuwa mapasta peke yao, bali hata Wakristo wa kawaida, wavulana kwa wasichana wenye kushuhudia imani yao. Hivyo magereza yote yalijaa. Kufungwa katika gereza za nchi ya Rumania, au nchi yo yote ya Kikomunisti, maana yake ni mateso makali.

Mateso yenyewe yalikuwa ya kutisha mno. Sipendelei sana kueleza mateso yale niliyoyapitia. Wakati niyaelezapo silali usiku. Ni maumivu makali mno!

**Mateso Yasiyosemeka.**

Mchungaji mmoja ajulikanaye kwa jina, Pasta Florescu aliteswa kwa visu na vyuma vilivyochomwa motoni mpaka kuwa vyekundu. Alipigwa mapigo mabaya mno. Ndipo mapanya wenye njaa kali waliongozwa chumbani kwa bomba kubwa la chuma. Hakuweza kulala isipokuwa kujilinda asigugunwe na mapanya hawa. Kiasi cha kusinzia kidogo tu, mapanya walimshambulia.

Alilazimishwa kusimama muda wa majuma mawili mchana na usiku. Wakomunisti walikuwa wakimlazimisha awasaliti ndugu zake, lakini yeye alipinga.

Mwishowe walimleta mwanawe wa kiume mwenye umri wa miaka kumi na minne, na kuanza kumpiga mbele ya babaye. Wakomunisti wale walisema wataendelea kumpiga yule mtoto mpaka pasta, baba yake, aseme yale waliyoyataka. Maskini Pasta Florescu alikuwa nusu maiti. Alivumilia kwa uchungu mwingi kadiri alivyoweza. Na wakati alipoona hawezi kuvumilia zaidi, alimlilia mwanawe aliyekuwa akiteswa.

"Alexander! Ni lazima niseme vile watakavyo! Siwezi kuvumilia zaidi kuona unavyopigwa hivi!"

Yule mtoto alijibu kwa unyonge, "Babangu! Tafadhali usinifedheheshe kwa kuwa mzazi msaliti! Pinga neno hili! Kama wataniua, basi nitakufa na maneno, 'Yesu na nchi ya Baba yangu!"

Wakomunisti walijaa hasira na kumwangukia kijana huyu kwa mapigo mpaka akafa, damu ikiwa imetapakaa kwenye kuta zote chumbani. Mvulana Alexander alikufa akimsifu Mungu. Ndugu yetu mpendwa Florescu alipoona hili limetukia, alithibitika upya katika imani, wala hakudumu vile alivyokuwa.

Zile pigu tulizofungwa mikononi zilikuwa na misumari mikali kwa ndani. Wakati tulipokuwa tumetulizana kimya, misumari ile haikutukatakata. Lakini katika

vyumba vya baridi kali, kila tulipojitikisa kwa kujikunyata, mikono yetu ilichanwachanwa na misumari ile.

Wakristo walifungwa miguu kwa kamba nzito, ndipo wakaning'inizwa vichwa chini. Halafu walipigwa mapigo makali madam miili ikipembea huko na huko.

Wakristo walifungiwa katika masanduku ya barafu na vyumba vya barafu vilivyokuwa baridi kweli. Mimi mwenyewe niliwahi kutumbukizwa katika chumba kimojawapo nikiwa na nguo nyepesi ajabu. Madaktari wa magereza walikaa wakichungulia ndani kwa tundu ili kuona dalili za kuganda mpaka kiasi cha kufa. Mara moja walitoa ishara kwa walinzi ambao huingia ndani kuwatoa na kuwapasha moto.

Baada ya kupata joto, wale Wakristo, mateka wafungwa, hurudishwa tena katika barafu mpaka wagande. Ndipo huondolewa haraka na kupashwa joto. Halafu hurudishwa tena. Ndipo hutolewa ili kupashwa joto. Halafu hurudishwa tena! Tendo hili hurudiwa tena na tena pasipo kikomo. Mpaka leo hii mimi sidiriki kufungua mashine ya barafu!

Sisi Wakristo tuliingizwa katika masanduku ya mbao membamba sana, yakizidi ukubwa wetu kiasi kidogo mno. Wala haikupatikana nafasi yo yote ya kujongea. Ndipo misumari mikubwa yenye ncha kali ilipigiliwa pande zote za sanduku. Ncha kali za misumari hii zilitokeza kwa ndani. Tuliposimama kimya kwa kutulizana, hapakuwa na shida kubwa. Lakini kwa vile tulilazimishwa kusimama katika masanduku haya muda mrefu tulichoka na kuyumba huku na huku kwa kuangukaanguka. Hapo ndipo ile misumari mikali ilituchoma miilini. Tulipojijongeza au kutikisa tu mwili, pale pale misumari mibaya ile ilituingia vibaya miilini!

Mateso na maovu ambayo Wakomunisti wamewatendea, na wanawatendea Wakristo yanazidi mafikara ya binadamu kwa mbali!

Niliwaona Wakomunisti wengi kwa nyuso za shangwe na furaha wakiwatesa Wakristo. Watesaji kwa kutabasamu waliwaambia Wakristo, "Sisi ndio ibilisi!"

Kumbe, kushindana kwetu si kwa mwili na damu, bali twashindana na mamlaka na nguvu za yule mwovu. Nasi tuliona kwamba Ukomunisti haukutoka kwa wanadamu, bali umetoka kwa yule mwovu. Ukomunisti ni nguvu ya yule roho mwovu, nayo yaweza tu kupambana na nguvu ya Roho wa Mungu ambaye ana nguvu kuliko mwovu.

Mara kwa mara niliwauliza wale watesaji, "Mbona hamna huruma mioyoni mwenu?"

Nao kama kawaida walinijibu kwa kutumia maneno ya Lenin. "Huwezi kukaanga yai pasipo kupasua ganda lake. Wala huwezi kukata mti pasipo kurusha vigeregenja."

Ndipo nilijibu tena, "Naam, hata mimi nafahamu huo usemi wa Lenin. Lakini pana tofauti kubwa. Wakati mti ukatwapo, hausikii maumivu. Lakini hapa mwawatesa binadamu. Kila pigo laleta maumivu makali, isitoshe pana mama waombolezao." Maelezo haya yote yalikuwa ni kupoteza wakati tu. Wao ni watu wasadikio kwamba hakuna roho wala ulimwengu usioonekana. Kwao binadamu ni mnyama tu asiye na roho, hivyo alingana kama gogo au gamba la yai! Kwa ajili ya imani hiyo, Wakomunisti hutumbukia katika kina kirefu cha ukatili usio mfano.

Ukatili wa mtu asadikiye kwamba hakuna Mungu ni wa kushangaza mno! Wakati mtu akoswapo imani kwamba matendo mema yana thawabu yake, na matendo maovu yana adhabu yake, ndio wakati mtu huyo hafai kuwa binadamu. Maana hana kizuizi cha maovu yaliyomo ndani yake.

Kila mara Wakomunisti watesaji walisema, "Hakuna Mungu, hakuna maisha ya baadaye, wala hakuna adhabu ya maovu! Tunaweza kufanya tupendavyo."

Hata niliwahi kumsikia mmoja wa watesaji akisema, "Namshukuru Mungu nisiyeamini, kwamba nimeishi mpaka saa hii ili niweze kuonyesha maovu yote yaliyo moyoni mwangu."

Kweli aliyaonyesha maovu yake kwa ukatili usio kifani wa kuwatesa wafungwa.

Huwa jambo la kusikitisha sana kusikia kwamba mamba amemla mtu. Lakini mamba hakaripiwi wala kulaumiwa, kwa sababu hana akili ya kutambua mema na mabaya kama vile binadamu alivyo. Hali kadhalika Wakomunisti hawatakaripiwa wala kulaumiwa kwa ajili ya ukatili wao. Ukomunisti umeharibu akili yao ya kutambua mema na mabaya. Ndiyo maana walijitapa kuwa hawakuwa na chembe ya huruma mioyoni mwao.

Nao hili lilikuwa fundisho kuu mno kwangu. Kwa kuwa Wakomunisti hawakumpa Yesu nafasi yo yote mioyoni mwao, hata mimi nilikata shauri kutompa Shetani nafasi yo yote katika moyo wangu.

Nilikwisha kueleza wazi matendo maovu ya Wakomunisti katika Kamati ya Usalama ya Baraza Kuu la Amerika. Nilisimulia vile Wakristo wafungwavyo misalabani kwa siku nne mchana na usiku. Ndipo misalaba ile hulazwa chini hali Wakristo bado wamefungwa pale. Halafu mamia ya wafungwa hushurutishwa kunya na kuwakojolea nyusoni na miili yote. Mwisho, misalaba ile husimikwa tena. Na Wakomunisti huwadhihaki kwa dharau kuu:

"Mtazameni Kristo wenu! Lo yu malidadi mbona! Ebu yanuseni manukato anayoleta kutoka mbinguni!"

Tena nilieleza vile Pasta mmoja baada ya kuteswa mpaka kiasi cha kuwa mwenda wazimu, alilazimishwa kutumia choo na mkojo kama Ushirika Mtakatifu, aki-

shirikisha Wakristo wafungwa. Tendo hili lilitukia katika gereza la Pitesti nchini Rumania.

Baadaye nilimwuliza Mchungaji yule kwa nini hakuchagua kufa badala ya kushiriki kutenda kufuru mbaya kama ile. Alinijibu hivi, "Tafadhali sana usinihukumu! Mimi nimekwisha kuteseka zaidi ya Kristo!"

Mateso yaliyo katika magereza ya Kikomunisti hayalinganishwi na vile Biblia ielezavyo maumivu ya jahanum.

Kwa kifupi haya ni maelezo ya mambo machache tu miongoni mwa yale yaliyotukia Jumapili moja katika gereza la Pitesti. Mambo mengine hayasemeki. Ningezimia kama nikiyasimulia tena na tena. Yanatisha mno, tena ni machafu kabisa hata kuyaandika. Lakini, hivyo ndivyo vitendo watendewavyo hata sasa ndugu zako katika Kristo.

Mmoja wa mashujaa hodari katika imani alikuwa Pasta Milan Haimovici. Kwa vile magereza yalijaa wafungwa, hivyo walinzi hawakutufahamu majina. Kila mara walipoitwa wafungwa ambao walipaswa kutandikwa viboko ishirini na vitano kwa kuvunja amri za jela, Pasta Milan Haimovici alijitokeza kupigwa badala mfungwa fulani. Alifanya hivi mara nyingi mno, na hivyo wafungwa wengine walimheshimu na kumtukuza Kristo Bwana wake.

Sitakuwa na mwisho kama nikiendelea kusimulia mateso ya Kikomunisti na vile Wakristo walivyojitoa kafara. Kwani siyo mateso pekee yaliyojulikana. Matendo ya ujasiri mkuu yalijulikana vile vile. Matendo ya kijasiri katika magereza yalikuwa mifano ya kutia moyo Wakristo waliokuwa bado huru.

Mmojawapo wa ndugu zetu wafanya kazi katika Kanisa la Siri alikuwa msichana mdogo. Polisi Wakomunisti walikwisha gundua kwamba msichana huyu alieneza Injili na kuwafunza watoto habari ya Kristo.

Walikata shauri kumkamata. Lakini ili kutaka kukamatwa kwake kulete maombolezo na maumivu makali, waliahirisha mpaka siku ya kuolewa kwake. Hivyo siku ile ya arusi yake, msichana alivalia vazi maalum la ndoa. Na kama ilivyo, siku kama hii huwa siku ya shangwe na furaha kuu katika maisha ya msichana. Ndipo ghafula, milango ilisukumwa kwa nguvu, na polisi wa siri walijazana ndani!

Wakati bibi arusi alipoona askari polisi, aliwapa mikono yote miwili wamtie pingu. Nao kwa fujo walimkaza pingu mikono yote miwili. Yule bibi arusi alimtazama mpendwa wake, bwana arusi, halafu alibusu pingu zile akasema, "Ninamshukuru Bwana Arusi wangu wa mbinguni kwa ajili ya lulu aliyonitunukia siku hii ya ndoa yangu. Namshukuru kwamba nastahili kuteswa kwa ajili yake!"

Askari walimburuta huyu bibi arusi akawaacha bwana arusi na rafiki zake Wakristo wakimwombolezea. Walijua matendo maovu na ya aibu ambayo askari walinzi Wakomunisti huwatendea wasichana Wakristo.

Msichana huyu alifunguliwa baada ya miaka mitano akiwa ameharibiwa vibaya, amevunjwa moyo, tena akionekana mzee wa miaka thelathini. Bwana arusi wake alikuwa akimngoja muda huu wote. Baada ya kuonana tena, bibi arusi alisema kwamba hiyo ilikuwa kazi kidogo aliyofanya kwa ajili ya Kristo. Wakristo wema na hodari jinsi hiyo wamo katika Kanisa la Siri.

## Kuoshwa Akili Maana Yake Ni Nini?

Neno "Kuoshwa Akili" limejulikana pote tangu vita ya Korea mpaka vita ya Vietnam. Mimi mwenyewe nimekwisha kupitia hatua za "kuoshwa akili." Hili ni teso baya na la kutisha kuliko mateso yote.

Kwa miaka mingi, kila siku tukikaa kiasi cha saa kumi na saba kusikiliza:

Ukomunisti ni Mwema!
Ukomunisti ni Mwema!
Ukomunisti ni Mwema!
Ukomunisti ni Mwema!
Ukristo ni upumbavu!
Ukristo ni upumbavu!
Ukristo ni upumbavu!
Uacheni!
Uacheni!
Uacheni!
Uacheni!

Naam! Kusikiliza mambo yaya haya tu yakirudiwa-rudiwa muda wa saa kumi na saba kila siku, kwa majuma, miezi na miaka!

Wakristo wengi wamewahi kuniuliza jinsi tulivyoepuka kuoshwa akili. Kuna njia moja ya kuzuia "kuoshwa akili", nayo ni kupinga "kuoshwa moyo". Kama moyo umesafishwa na upendo wa Kristo Yesu, na kama moyo wampenda Kristo kweli, unaweza kupinga mateso ya namna yo yote. Je, bwana arusi anaweza kushindwa jambo gani kwa ajili ya bibi arusi ampendaye? Hivyo kama wampenda Kristo kiasi kile Mariam alivyompenda alipokuwa mtoto mchanga mikononi mwake, na kama wampenda Yesu kama vile bwana arusi ampendavyo bibi arusi, basi unaweza kuzuia mateso kama yale.

Mungu atatuhukumu kwa kadiri ya wingi wa upendo wetu, wala siyo kwa kadiri ya kiasi tulichovumilia. Mimi nashuhudia katika magereza ya Kikomunisti kusudi wawe na upendo, yaani wampende Mungu na watu.

Mateso na ukatili viliendelea pasipo kizuizi. Mimi mwenyewe niliteswa kwa mapigo mabaya. Wakati nilipopigwa mpaka kuzirai au kupata mzumbao hata watesi wangu wakatambua kuwa hakuna tumaini la kujitolea kwangu, ndipo hunirudisha kijumbani. Huachwa humo

hoi, nusu mfu, bila uangalizi, nikirudia uhai pole pole kusudi watesi wangu waje tena kufanya kazi yao. Watu wengi mno walikufa katika hatua hii. Lakini kwa namna ya ajabu, mimi nguvu zangu zilinirudia kila mara. Kwa mfuatano wa miaka katika magereza tofauti, walinivunja mifupa yangu minne ya mgogo, na mingineyo. Baadhi ya mifupa ilipindwa mahali kumi na mbili mbali mbali Walinichoma moto na kutoboa matundu kumi na manane mwilini mwangu!

Madaktari katika mji wa Oslo walipoona majeraha yote haya pamoja na makovu yaliyokuwa katika mapafu yangu kwa ajili ya kifua kikuu, walisema wazi kwamba kuishi kwangu ulikuwa ni mwujiza mtupu! Kwa kufuata vitabu vyao vya udaktari ningekuwa nimekufa miaka mingi. Hata mimi mwenyewe najua wazi wazi kuwa kuishi kwangu ulikuwa mwujiza! Kweli, Mungu ni Mungu wa miujiza.

Ninaamini Mungu alifanya mwujiza huu kusudi mweze kusikia sauti yangu ikipaaza kwa niaba ya Kanisa la Siri lililo katika Ngome ya Chuma. Mungu kwa ajabu alimsalimisha mtu mmoja kusudi atangaze ujumbe kutoka kwa ndugu zenu waaminifu wanaoteswa.

**Uhuru Wa Muda Ndipo Kufungwa Tena.**

Mwaka 1956 ulifika. Mimi nilikuwa nimekwisha kukaa gerezani miaka minane na nusu. Nilikuwa nime-konda sana hata kupata magamba mabaya. Nilikuwa nimepigwa vibaya kikatili, nimekanyagwa na kupigwa mateke, nimedhihakiwa, nimenyimwa chakula, nime-kandamizwa, nimesailiwa mpaka kiasi cha kuchukizwa, nimetishwa na kutupiliwa mbali! Hakuna mojawapo la mateso haya lililowapa watesi wangu jawabu waliloli-taka. Hivyo walikata tamaa na kuniachia huru. Isitoshe watu wengi mno walilalamika kuhusu kufungwa kwangu.

Niliruhusiwa kurudia kazi zangu muda wa juma moja tu. Nilipata kuhubiri mara mbili, ndipo niliitwa na ku-katazwa nisiendelee kuhubiri wala kujiingiza katika

shughuli zo zote za dini. Je, nilikuwa nimesema nini baya? Nilikuwa nimewashauri Wakristo wa shirika langu wazidi kuwa "wavumilivu, wawe na uvumilivu zaidi." Askari polisi Wakomunisti walinizomea kwamba niliwaambia watu, "Mvumilie mpaka Waamerika watakapokuja kuwaokoa."

Vile vile nilikuwa nimewaambia kwamba upepo wavuma, na mabadiliko yaja. Neno hili askari wale walilifasiri, "Unawaambia kuwa Wakomunisti hawataendelea kutawala! Haya ni mapinduzi ya uwongo," walininguruma vikali. Hivyo huo ndio ulikuwa mwisho wa huduma yangu ya wazi.

Pengine watawala wangedhania kuwa ningeogopa kuendelea na mahubiri yangu ya siri. Kumbe walikuwa wamekosea vibaya. Kwa siri nilishika tena kazi niliyokuwa nikifanya zamani. Isitoshe jamaa yangu walinisaidia mno.

Zaidi tena nilishuhudia vikundi vingi vya siri kwa uhuru mwingi nikitoka na kuingia kama kizuka katika himaya yake. Safari hii nilikuwa na makovu na vidonda vingi vya kuthibitisha ushuhuda wangu wa matendo ya kikatili ya watu wasiomwamini Mungu. Hivyo Wakristo wengi waliokwisha kuzimia roho walihuishwa na kuzidi kumtumaini Mungu kwa ushujaa mkuu. Niliongoza kikosi cha wainjilisti waliosaidiana wao kwa wao kueneza Injili machoni pa Wakomunisti waliopigwa upofu kwa namna ya mwujiza wa ajabu. Kweli kama mtu atapofuka kiasi cha kutoona mkono wa Mungu ukifanya kazi, hataweza kuona mkono wa mwinjilisti ukitenda kazi vile vile.

Mwishowe jitihada isiyokoma ya askari polisi, wakinitafuta na kupeleleza shughuli zangu mchana na usiku, ilifanikiwa vizuri. Niligunduliwa na kukamatwa tena. Kwa ajili ya sababu zisizojulikana, safari hii hawakufunga jamaa yangu. Nafikiri pengine ni kwa sababu ya kujulikana kwangu, lakini sijui barabara.

Nilikuwa nimefungwa gerezani muda wa miaka minane na nusu, ndipo nikapata miaka mitatu ya uhuru wenye masharti. Sasa itakuwa lazima nifungwe tena miaka mitano na nusu.

Kwa namna nyingi, kifungo changu cha pili kilikuwa kibaya zaidi kuliko kile cha kwanza. Nilijua wazi yaliyonikabili. Tena afya ya mwili wangu ilidhoofu haraka mno. Walakini tulizidi kufanya kazi za siri katika Kanisa la Siri, katikati ya magereza ya siri ya Kikomunisti.

**Tulifanya Mkataba – Sisi Tuhubiri, Wao Watupige.**

Ilikuwa mwiko kabisa kuhubiri wafungwa wengine gerezani. Tena ilifahamika wazi kwamba, ye yote atakayeonekana akihubiri atapigwa vibaya. Baadhi yetu wengi tulikata shauri kupokea mapigo yale makali kwa ajili ya kutaka kuhubiri. Hivyo tulikubali mkataba wao. Mkataba ulikuwa: *Sisi Tuhubiri, Wao Watupige.* Sisi tulifurahia kuhubiri, na walinzi walifurahia kutupiga. Hivyo kila mmoja alifurahi.

Tamasha kama hili ifuatayo ilitukia mara nyingi mno nisizoweza kukumbuka.

Ndugu mmoja alikuwa akihubiri wafungwa wenzake wakati walinzi walipomfumania ghafula na kumkata kauli. Walimburuta kupitia ukumbini hadi katika chumba cha kupigia. Baada ya mapigo makali yasiyo na kikomo, walimleta tena na kumtupa sakafuni, akiwa amejaa damu na machubuko. Pole pole aliyanyanyua magofu ya ya mwili wake uliogongwagongwa, na kwa kujikalifu sana aliyanyosha mavazi yake akasema, "Sasa ndugu zangu, nilikuwa nimefika wapi nilipokatwa kauli?" Alizidi kuendelea na ujumbe wake wa Injili.

Naam! Nilipata kuona mambo mema ajabu! Mara nyingi wahubiri walikuwa watu wa kawaida tu. Watu wa kawaida walioongozwa na Roho Mtakatifu walihubiri vizuri kweli. Mioyo yao ilikuwa katika maneno yao, na kweli kuhubiri katika hali ya kuadhibiwa vile siyo

mzaha hata kidogo. Ndipo walinzi hufika kumkokota mhubiri na kumpiga nusura kufa.

Katika gereza ya Gherla, Mkristo mmoja aliyeitwa Grecu alihukumiwa kupigwa mpaka kufa. Mfululizo wa mapigo ulichukua majuma kadhaa wa kadhaa. Alikuwa akipigwa pole pole sana. Aliweza kupigwa pigo moja la nguvu katika nyayo kwa kutumia rungu la mpira mgumu, ndipo akaachwa muda. Baada ya dakika chache alipigwa tena, halafu akaachwa, ndipo akapigwa tena, na vivi hivi. Alikuwa akipigwa hata mapumbu. Ndipo daktari humdunga sindano. Na baada ya kuhuika tena, alipewa chakula kizuri kusudi apate nguvu, ndipo alipigwa tena vivyo hivyo mpaka akafa kwa ajili ya mapigo yale ya pole pole. Mtu mmoja aliyeongoza mateso haya alikuwa mjumbe katika Kamati Kuu ya Kikomunisti, naye aliitwa Reck.

Hata wakati fulani fulani, Reck naye alisikiwa akisema maneno ambayo Wakomunisti walizoea kuwaambia Wakristo:

"Mwajua! Mimi ni Mungu! Ninazo nguvu za uzima na kifo juu yenu. Yule aliye juu mbinguni hana mamlaka juu ya maisha yenu. Kila jambo limo mikononi mwangu. Kama nikitaka mwaweza kuishi! Tena nikitaka mwaweza kufa! Mwaona! Mimi ni Mungu!"

Hivyo ndivyo walivyowadhihaki Wakristo.

Katika hali hii ya mateso makuu, ndugu Grecu alimpa Reck jibu zuri ajabu ambalo Reck mwenyewe alipata kunisimulia. Grecu alisema:

"Hujui ukuu wa neno ulilosema. Wewe kweli ni mungu. Maana kila yai la nzi huanguliwa likawa nzi mzima kama likipitia hatua zote bila hitilafu. Hata wewe hukuumbwa kusudi uwe mtesaji na mwuaji. Uliumbwa kusudi uwe mfano wa Mungu. Yesu aliwaambia Wayahudi wakati ule, 'Ninyi ni mungu.' Uzima wa Mungu umo mioyoni mwenu. Watu wengi ambao walikuwa

kama wewe, watesaji kama Paulo, walipata kugundua kuwa ilikuwa aibu kuu kwa binadamu kutenda ukatili mbaya hivi, badala ya kutenda mema. Hivyo watu hao wameitwaa hali ya utakatifu na kuwa watu wema. Bwana Reck, amini ninayosema kwamba wito wako ni kuwa kama Mungu, yaani ufanane na Mungu, wala siyo kuwa mtesaji na mwuaji!"

Kwa wakati ule, Bwana Reck hakujali hayo maneno ya mateka wake. Ni sawa na Saulo wa Tarsus ambavyo naye hakujali ushuhuda mwema wa Stefano alipouawa machoni pake. Bali maneno yale yalifanya kazi moyoni mwake. Ndivyo hata Reck naye baadaye alitambua wazi kwamba huo ndio ulikuwa wito wake kweli.

Mapigo, mateso na mauaji ya Wakomunisti yalileta fundisho moja kuu kwamba *roho hutawala mwili.* Kila mara tulipoteswa, tulijisikia kama roho ameyaondolea mbali mateso na kuyazika katika utukufu wa Kristo uliokuwa mbele yetu.

Wakati tulipopewa kipande kimoja cha mkate kila juma, na mchuzi mchafu kila siku, hata hivyo tulikata shauri kutoa zaka kwa uaminifu. Kila juma la kumi tulitoa zaka kile kipande cha mkate kwa kumpa mmoja-wapo wa ndugu zetu aliyekuwa amedhoofika vibaya.

Mkristo mmoja alihukumiwa kufa. Lakini kabla ya kunyongwa aliruhusiwakumwona mkewe. Na wosia wake kwa mkewe ulikuwa hivi:

*"Mke wangu! Sharti ufahamu kwamba nitakufa nikiwapenda wauaji wangu. Maana hawajui watendalo! Na ombi langu la mwisho kwako ni kwamba, hata wewe nakuomba uwapende vile vile. Usiwe na uchungu moyoni mwako kwa kuwa wanamwua mpendwa wako. Tutakutana mbinguni!"*

Maneno haya yalimchoma sana ofisa aliyekuwapo wakati wa mazungumzo. Na ni ofisa yule yule ndiye aliniambia hadithi hii tukiwa gerezani pamoja, hata yeye akiwa amefungwa kwa sababu ya kuwa Mkristo.

Katika gereza la Tirgu-Ocna, palikuwa na mfungwa kijana aliyeitwa Matchevici Kijana huyu alifungwa akiwa na umri wa miaka kumi na minane. Kwa sababu ya mateso mabaya alipata ugonjwa wa kifua kikuu. Jamaa yake walipogundua afya ya kijana huyu kuwa katika hatari, walimtumia chupa mia moja za dawa itwayo *Streoptomycin* ili kuokoa maisha yake.

Ofisa wa Siasa gerezani alimwita kijana Matchevici akamwonyesha kifurushi kile cha dawa, na kusema:

"Hapa pana dawa ya kuokoa maisha yako. Lakini sheria yakataza mfungwa awaye yote asipokee kifurushi kutoka kwa jamaa zake. Ingawa ni hivyo, lakini mimi mwenyewe napenda sana kukusaidia. Maana wewe u kijana mdogo bado. Wala sipendi kukuona unakufa mumu humu gerezani. Basi, nisaidie, ili nikusaidie vile vile! Nipe habari za wafungwa wenzako. Na hii itakuwa sababu ya kutosha nitakayotoa kwa wakubwa wangu kuonyesha kwamba ilikuwa haki upokee kifurushi chako."

Kijana Matchevici alijibu mara moja. "Sitaki kuishi nikiwa mwenye fedheha wakati nijitazamapo katika kioo na kuuona uso wangu ukiwa wa msaliti. Sitaweza kukubali mkataba huo! *Mimi nachagua kufa!*"

Yule ofisa wa polisi wa siri alimshika mkono kijana Matchevici na kumpongeza mno:

"Nakupongeza mno! Sikutumaini kupata jibu tofauti na hili kutoka kwako. Walakini napenda kutoa shauri jingine. Sikia, baadhi ya wafungwa hutuletea habari. Wanajiita Wakomunisti, lakini wanawakana ninyi. Wanashika pande mbili. Wala sisi hatuwaamini kamwe. Hivyo tungependa kufahamu juu ya uaminifu wao. Kwenu, watu hao ni wasaliti wazi, maana wanawatendea maovu kwa kutuelezea habari, maneno na matendo yenu. Nafahamu wazi kuwa wewe usingependa kumsaliti nduguyo. Lakini, ebu tupe habari za watu

hawa ambao ni kinyume chenu, nawe utaokoa maisha yako!"

Matchevici alijibu upesi kama vile kwanza, alisema:

"Mimi ni mwanafunzi wa Kristo. Na Kristo ametufundisha kuwapenda hata adui zetu. Kweli hawa wanaotusaliti wanatutendea maovu, lakini mimi sitalipiza ovu kwa ovu. Ninawahurumia mno, ninawaombea kila mara, wala sipendi kuhusubiana na Wakomunisti."

Kijana Matchevici alirudi chumbani bila dawa yake, baada ya kuhojiana na ofisa wa polisi. Na baada ya muda mfupi, Matchevici alifariki katika chumba kile kile nilichokuwa nimefungwa. Saa ya kufa kwake nilikuwapo, *alikufa akimtukuza na kumsifu Mungu.* Upendo hushinda hata tamaa kuu ya maisha.

Hata fukara akiwa anapenda muziki na michezo, hulipa shilingi yake moja ya mwisho kusudi ahudhurie michezo na tamasha la muziki. Hubaki bila pesa, lakini hajuti wala kusikitika, kwa sababu amesikia na kuona mambo mema ya kumstarehesha na kumtumbuiza.

Hali kadhalika mimi sijuti kuona nimepoteza miaka mingi nikiwa gerezani. Nimeona mambo mema ajabu! Mimi mwenyewe nimekuwa miongoni mwa watu dhaifu na duni katika gereza, lakini nilijaliwa kuwa gerezani pamoja na watakatifu wakuu, mashujaa wa imani sawa sawa na Wakristo wa karne ya kwanza. Kwa furaha kuu walikufa kwa ajili ya Kristo. Wema wa roho za watakatifu na mashujaa hao hauwezi kuelezeka.

Mambo ninayoyaeleza hayahitilafiani na yale ya Wakristo wa kale. Mambo na matendo yasiyo ya kawaida yamekuwa ya kawaida kwa Wakristo wa Kanisa la Siri. Kanisa hili la Siri limekuwa kanisa lililorudia upendo wa kwanza.

Nilipokuwa sijaingia gerezani nilimpenda Kristo sana. Lakini sasa, baada ya kuingia gerezani na kumwona "Bwana Arusi Kristo" katika mwili wake wa

kiroho, naweza kusema kuwa napenda Kanisa la Siri kama vile nimpendavyo Kristo. Nimeona wema wa kanisa hili na roho yake ya kujitoa kafara.

**Yaliyowapata Mke na Mtoto Wangu.**

Nilikuwa nimetengwa mbali na mke wangu. Wala sikujua yaliyompata baada ya kukamatwa kwangu. Ilikuwa baada ya kupita miaka mingi ndipo nilisikia kuwa hata yeye pia alipata kufungwa. Wakristo wanawake huteswa vibaya mno gerezani kuliko wanaume. Walinzi wakatili wale huwashika kwa nguvu wasichana kwa wanawake na kulala nao. Dhihaka na uchafu watendewao wanawake vyatisha mno!

Wanawake walilazimishwa kufanya kazi ngumu kama vibarua wakichimba mfereji wa maji uliokuwa ukijengwa. Nao iliwapasa kutimiza kipande sawa na wanaume. Walichimbishwa mchanga nje hata wakati wa baridi. Wafungwa kahaba ndio waliofanywa wasimamizi, nao walishindana kuwatesa wenzao waliokuwa waaminifu. Mke wangu aliwahi kula majani kama ng'ombe ili apate kuishi. Wafungwa wenye njaa kali walikula panya na nyoka wakati wakichimba mfereji huo.

Mojawapo ya tafrija za askari walinzi kila siku ya Jumapili ilikuwa kuwatosa wanawake katika mto Danube, na kuwavua tena. Askari walidhihaki na kuchekelea walipoona miili ya wanawake hawa waliotota maji. Ndipo waliwatupa majini tena, na kuwavua vivyo hivyo. Mke wangu naye aliwahi kutoswa hivyo katika mto Danube.

Mwanangu Mihai aliachwa atangetange ovyo barabarani wakati wazazi wake tulipokamatwa. Lakini Mihai tangu utoto wake alikuwa mtu wa dini, tena alivutwa mno na habari za imani. Wakati babaye na mamaye walipokamatwa, yeye akiwa na umri wa miaka tisa, mtoto huyu alipitia maisha ya hatari kubwa. Alichukia na kuishuku mno dini yake. Yeye alikumbana

na matatizo magumu mno mapema kuliko yale yawapatayo watoto wa umri wake. Ilikuwa lazima afikirie njia za kufanya kazi kusudi apate kuishi.

Lilikuwa kosa la kuvunja sheria kwa mtu ye yote aliyesaidia mtoto wa Mkristo mfungwa. Wanawake wawili waliopatikana wakimsaidia Mihai walikamatwa baadaye na kupigwa vibaya, na mpaka sasa ni vilema, ingawaje imepita miaka kumi na mitano. Bibi mmoja aliyejitolea kumchukua Mihai nyumbani mwake alihukumiwa kifungo cha miaka minane kwa kosa la kumsaidia mtoto wa mfungwa. Bibi huyu aling'olewa meno yote! Mifupa yake kadha ilivunjwa wala hataweza kufanya kazi tena. Hata yeye naye atakuwa kilema wa maisha!

## "Mihai, Mwamini Yesu!"

Mihai alianza kufanya kazi ya kibarua alipokuwa na umri wa miaka kumi na mmoja. Mateso makali yalikuwa yameteteresha imani yake. Lakini, miaka miwili baada ya kufungwa kwa mamaye, Mihai aliruhusiwa kwenda gerezani kumwona. Ndipo aliingia katika gereza ya Kikomunisti na kumwona Mamaye ndani ya ngome ya vyuma. Mamaye alikuwa amekonda, mchafu, mwenye mikono iliyochubuka, akiwa amevaa mavazi machafu ya kifungwa.

Mamaye alipomwona alimsalimu kwa maneno, "Mihai, Mwamini Yesu!"

Kwa hasira kali, walinzi walimsukumia mbali yule mama. Mihai alilia machozi wakati alipoona Mamaye akiburutwa vibaya na askari. Kumbe! Dakika hii ilikuwa ni dakika ya kuongoka kwake. Alijua wazi kwamba kama Kristo anaweza kupendwa hata katika hali kama hiyo, basi, Yeye ni Mwokozi kweli. Baadaye alisema, "Hata kama kuna mambo mengine mema zaidi katika Ukristo, si kitu: *Mimi imani ya Mamangu yanitosha!*" Hiyo ilikuwa ndiyo siku aliyompokea Kristo moyoni mwake.

Hata shuleni, mwanangu Mihai alikuwa na vita. Yeye alikuwa mwanafunzi mwema, hivyo alipewa tuzo ya tai nyekundu ya kuvaa shingoni. Hii ndiyo ilikuwa alama ya kikosi cha vijana Wakomunisti.

Lakini Mihai alikataa akisema, "Sitavaa alama ya watu ambao wamewafunga Mama na Baba gerezani!"

Pale pale alifukuzwa shuleni kwa sababu hii. Baada ya kupoteza mwaka mmoja bila masomo, aliingia shuleni tena. Safari hii alijificha kwamba hakuwa mtoto wa mfungwa Mkristo.

Baadaye katika darasa lao walitakiwa kuandika insha ndefu ya kupinga Biblia. Mihai aliandika maneno haya katika insha yake:

"Hoja za kupinga Biblia ni duni, tena hata yale madondoo ya kupinga Biblia ni uwongo mtupu. Ni wazi kuwa hata Profesa (mwalimu mkuu chuoni) hajapata kusoma Biblia. Biblia inakubaliana kabisa na sayansi."

*Alifukuzwa tena shuleni!* Safari hii alipoteza miaka miwili bila masomo.

Mwishowe aliruhusiwa kwenda kusoma katika seminari. Mafundisho yote ya shule hii yalikuwa elimu ya Marx, na kila neno lilielezwa kufuata mtindo wa Karl Marx. Mihai alipinga hili wazi wazi darasani, hata wanafunzi wengine nao walimwunga mkono. Matokeo yake yalikuwa kwamba alifukuzwa mapema bila kumaliza mafunzo yake ya Seminari.

Mihai alipokuwa angali shuleni, ndipo mwalimu afundishe habari za kumpinga Mungu, mwanangu husimama na kukanusha kwa nguvu. Kila mara aliwaambia walimu wa jinsi hiyo wajibu wao kama watawapotosha vijana jinsi hiyo. Mara nyingi darasa zima lilimwunga mkono. Ilikuwa lazima kwamba mtu mmoja sharti apate ujasiri wa kusimama na kusema. Ndipo wengine wote walimwunga mkono. Kwa ajili ya hamu ya elimu, ilikuwa

lazima Mihai afiche kwamba hakuwa mtoto wa Wurmbrand, yule mfungwa Mkristo. Lakini kila walipogundua, Mkuu wa chuo alimwita ofisini na kumfukuza shuleni. Hili lilikuwa ndilo jawabu la kawaida.

Mihai naye aliteseka mno kwa njaa. Jamaa wa wafungwa Wakristo katika nchi za Kikomunisti, huachwa wafe kwa njaa. Ni jinaya kuu kuwasaidia.

Sasa nitawasimulia kisa kimoja cha mateso ya jamaa ambao niliwafahamu mno. Ndugu mmoja alifungwa gerezani kwa sababu ya kazi yake katika Kanisa la Siri. Alimwacha mkewe na watoto sita nyumbani. Binti zake wawili, wenye miaka kumi na tisa na kumi na saba hawakuweza kupata kazi. Ni taifa peke yake ndilo huajili kazi katika nchi za Kikomunisti. Hivyo watoto wa "wahalifu", yaani Wakristo, hawapati kazi. Tafadhali sana nakuomba usihukumu kisa hiki kufuatana na kanuni ya tabia na uadilifu. Walakini kubali kisa chenyewe na habari zake kamili!

Hawa binti wawili Wakristo, tena watoto wa Mkristo mfungwa, waliingia umalaya kusudi kupata fedha za kulisha wadogo zao na mama yao mgonjwa. Kaka yao mdogo alipoona haya alipatwa kichaa, akapelekwa katika kambi ya wenda wazimu.

Baada ya miaka, baba yao alifunguliwa. Alipofika nyumbani kuona haya, alimwomba Mungu, "Mungu, nirudishe tena gerezani.Siwezi kuvumilia kuona matendo haya yote!"

Maombi yake yalisikiwa. Naye kwa sasa yumo gerezani kwa kosa la kuwashuhudia watoto wake habari za Kristo. Binti zake sasa sio malaya tena. Wamepatiwa kazi baada ya kukubaliana na madai ya polisi wa siri. Binti hawa sasa hutoa habari kwa askari polisi. Kwa kuwa wao ni watoto wa Mkristo mfungwa, hivyo hupokelewa kwa heshima sana katika kila nyumba. Husikiliza, ndipo hutoa taarifa ya kila neno kwa askari polisi.

Usilaumu jambo hili kwa kusema kuwa ni upotovu na uovu mkuu. Kweli yaonekana hivyo. Lakini jiulize iwapo uovu huu siyo dhambi yako kwamba mikasa yote hii yatokea! Mbona jamaa wa Kikristo kama hao watupwa tu ovyo pasipo kusaidiwa na wewe uliye huru?

SURA YA TATU

# Uhuru Wa Masharti

Jumla ya miaka kumi na minne ilipita nikiwa gerezani. Muda huu wote sikupata kuona Biblia au kitabu kingine cho chote. Nilisahau hata kuandika! Kutokana na njaa kuu, dawa mbaya za kulevya na mateso makali, nilisahau hata Maandiko Matakatifu! Lakini siku ile niliyotimiza miaka kumi na minne kamili, katika usahaulifu ule wote, aya moja ilirejea ubongoni mwangu:

"Yakobo alimtumikia Raheli miaka kumi na minne, *nayo ikawa machoni pake kama siku chache tu kwa vile alivyompenda.*"

Muda mfupi baada ya haya nilifunguliwa kutokana na msamaha uliotolewa kwa wafungwa katika nchi yetu. Msamaha huu ulikuja baada ya mashauri na mawazo ya Waamerika wengi.

Nilionana tena na mke wangu aliyekuwa akinisubiri kwa uaminifu muda wa miaka kumi na minne. Sote tulianza tena maisha katika ufukara mkuu, maana wakati mtu afungwapo, mali yake yote huchukuliwa.

Mapasta waliofunguliwa waliweza kupata kanisa ndogo ndogo. Mimi nilipata kanisa moja katika mji wa Orsova. Wizara ya Dini ya Kikomunisti ilinieleza kwamba kanisa yangu ilikuwa na watu thelathini na watano, halafu nilionywa wasiwe thelathini na sita. Tena niliambiwa niwe mtumishi wa polisi wa siri, nikiwapelekea habari za Wakristo, wala tena nisikaribishe watoto na vijana kanisani! Hivi ndivyo Wakomunisti watumiavyo makanisa kama chombo cha kutawala matakwa yao.

Nilijua wazi wazi kama nikihubiri, lazima tu watu wengi wafike kusikiliza. Kwa hiyo sikujaribu kuhubiri hata katika kanisa langu. Bali nilijiunga tena na Kanisa la Siri, nikishiriki mema yote na hatari za kazi hii.

Muda wa miaka ile niliyokaa kifungoni, Mungu alikuwa ametenda kazi ajabu. Kanisa la Siri lilikuwa bado halijaachwa wala kusahauliwa. Waamerika na Wakristo wengine walikuwa wameanza kutusaidia na kutuombea.

Siku moja katika mji mkuu wa mkoa nilikuwa nikipumzika kidogo katika nyumba ya ndugu mmoja. Mara moja niliamshwa na sauti kusema, "Ndugu kutoka ng'ambo wamekuja." Kule Magharibi palikuwa na ndugu ambao walikuwa hawajatutupa wala kutusahau.

Wakristo wakubwa kwa wadogo walifanya mpango wa siri wa kusaidia jamaa za Wakristo wafungwa na wafia dini. Hata kwa siri waliingiza vitabu vya Kikristo.

Katika chumba kingine nilikuta ndugu sita waliokuja kufanya kazi hii. Tulizungumza mengi mno pamoja. Baadaye waliniambia kuwa waliwahi kusikia habari za mtu mmoja aliyekaa gerezani miaka kumi na minne na kwa anwani ya mji ule wangepata kuonana naye. Ndipo niliwaambia kwamba mtu huyo ni mimi.

Kwa kushangaa sana walijibu, "Sisi tulitazamia kumwona akiwa mtu mwenye huzuni na uchungu mwingi! Haiwezekani kamwe kuwa wewe! Mbona una furaha ya ajabu hivi? !"

Pale pale nilizidi kuwahakikishia kwamba ni mimi niliyekuwa mfungwa, na kufika kwao kulikuwa ndiyo asili ya furaha yangu. Maana nafahamu sasa kwamba hatukusahaulika kamwe. Pole pole, kwa uthabiti na utaratibu maalum, msaada ulifika mara kwa mara kwa Kanisa la Siri. Kupitia katika mifereji au njia za siri, tulipata Biblia na vitabu vingi vya Kikristo. Hata msaada kwa jamaa za Wakristo wafungwa na wafia dini ulifika vile vile. Sasa kwa msaada huo, sisi Wakristo

wa Kanisa la Siri tuliweza kufanya kazi vizuri.

Kweli ndugu hawa walituletea msaada wa Neno la Mungu na vifaa vinginevyo, lakini sisi tulijiona kuwa tunapendwa mno. Ndugu hawa walionyesha upendo, ambalo ni neno kuu la kutufariji mno.

Katika muda ule wa "kuoshwa akili" tulikuwa tukisikia:

"Hakuna mtu ye yote anayewapenda tena! Hakuna mtu ye yote anayewapenda tena! Hakuna mtu ye yote anayewapenda tena!"

Lakini sasa tunawaona Wakristo Waamerika na Waingereza wanatoa maisha yao ili kutuonyesha wanavyotupenda. Baada yao kupata maarifa kutoka kwetu, walibuni maarifa ya kazi ya siri. Mara nyingi waliweza kujipenyeza katika nyumba zilizozungukwa na askari polisi pasipo polisi kuwa na habari vile walivyoingia.

Haiwezekani kueleza manufaa ya Biblia zilizoingizwa kwa siri namna hii. Wala hata Wakristo Waamerika na Waingereza wanaoziingiza hawawezi kuyaelewa.

Mimi na jamaa yangu tusingeweza kuishi bila msaada wa vifaa kutoka kwa Wakristo wa ng'ambo waliokuwa wakiomba vile vile. Hili lilikuwa kweli hata kwa jamaa za wafungwa na wafia dini wengine. Ninaweza kuthibitisha wazi kwa kisa kimoja cha msaada wa vifaa na mambo mengine makuu tuliyopata kutoka kwa Wakristo wa Uingereza. Kwetu sisi wajumbe wao walikuwa kama malaika waliotumwa na Mungu!

Kwa sababu ya kuhuishwa tena kwa kazi za Kanisa la Siri, mimi mwenyewe nilikuwa katika hatari ya kukamatwa mara nyingine. Wakati huu vyama viwili vya Kikristo vililipa fidia ya Shs. 50,000 kwa ajili yangu. Hivyo nilipata kuruhusiwa kutoka nchini Rumania.

## Sababu Ya Kutoka Nchini Rumania.

Mimi mwenyewe nisingeondoka nchini Rumania,

licha ya kuwako mateso na hatari zote hizo. Lakini Viongozi wa Kanisa la Siri waliniagiza nitumie muda huu, nitoke, niwe Sauti ya Kanisa la Siri katika Ulimwengu Huru. Waliniomba kwa niaba yao niwaelezee ndugu wa Magharibi mateso na mahitaji ya Kanisa la Siri. Ingawaje ninakwenda katika nchi za Magharibi, lakini moyo wangu wabakia pamoja nao. Kama nisingetambua haja kuu ya watu kutaka kusikia mateso na ujasiri wa kazi za Kanisa la Siri, nisingelitoka nchini Rumania. Hivyo basi, huu ndio ujumbe wangu.

Askari polisi wa siri waliniita mara mbili kabla sijatoka nchini Rumania. Kwanza waliniambia – kwamba fedha za fidia yangu zilikwisha pokelewa. (Maana Rumania huuza raia wake kwa fedha sababu ya shida kuu ya uchumi iliyoletwa nchini na ukomunisti.) Ndipo baadaye walinikanya:

"Enenda kule Magharibi ukahubiri Kristo kwa nguvu uwezavyo. Lakini jihadhari usituguse! Usiseme neno lo lote kutusuta! Tutakwambia wazi mpango uliopo kama hutasikia! Kwa kiasi cha Shs. 3,000 tu, tutaweza kupata haramia atakayekuulia mbali, au kukuiba na kukuleta kwetu."

Hapa nilikumbuka wazi, maana mimi mwenyewe nilifungwa gerezani na Askofu Vasile Leul ambaye aliibwa toka Austria mpaka akaletwa Rumania. Kucha zake zote ziling'olewa! Tena nilikuwa na wengine walioibwa toka Berlin nchini Ujerumani. Karibu, Warumania wengine waliibwa toka Italia na Ufaransa.

Halafu mara ya pili waliendelea kuniambia, "Tunaweza kuharibu sifa yako kwa kukusingizia kwamba ulizini na msichana, au wizi, au dhambi zako za ujana. Wale watu wa Magharibi, hasa Waamerika ni wepesi mno kudanganywa na kurubuni!"

Baada ya kutishwa vile, ndipo waliniruhusu niondoke nchini Rumania. Waliamini kabisa hatua zile za "kuoshwa akili" nilizopitia kwamba zimefaulu. Maana kule

Magharibi walikuwako watu wengine wengi waliopitia hatua zile zote kama mimi, nao walikuwa kimya. Baadhi yao huusifu ukomunisti, hata baada ya kuteswa na Wakomunisti. Hivyo Wakomunisti walikuwa na hakika kwamba hata mimi pia nitakuwa kimya.

Kwa hiyo katika mwezi Desemba, mwaka 1965, mimi na jamaa yangu tuliondoka nchini Rumania.

Tendo langu la mwisho kabla ya kuondoka Rumania, nilikwenda kwa kaburi la ofisa aliyetoa amri ya kukamatwa kwangu, na ambaye aliongoza mateso yangu miaka yote. Niliweka maua katika kaburi lile. Kwa tendo hili nilijitoa wakf maisha yangu ili kuwapa Wakomunisti furaha ya Kristo ambayo hawakuwa nayo.

Mimi nachukia siasa ya Kikomunisti, bali watu ninawapenda. Nachukia dhambi, lakini nampenda mwenye dhambi. Hivyo nawapenda Wakomunisti kwa moyo wangu wote. Wakomunisti wanaweza kuua Wakristo, walakini hawawezi kuua upendo wa Wakristo wale. Mimi mwenyewe sina hata chembe ndogo ya uchungu wala chuki kwa Wakomunisti, au watesi wangu.

SURA YA NNE

# Hatari Ya Ukomunisti

Wayahudi wana hadithi kwamba, wakati babu zao walipokombolewa kutoka utumwani Misri, halafu Wamisri walipokufa maji katika Bahari ya Sham, malaika mbinguni nao waliimba wimbo wa ushindi pamoja na Waisraeli. Ndipo Mungu aliwaambia wale malaika:

"Wayahudi ni watu, hivyo wanaweza kushangilia wokovu wao. Lakini ninyi natumaini mwafahamu zaidi. Je, Wamisri sio viumbe wangu? Mwadhani kuwa mimi siwapendi hata wao? Mbona hamwezi kutambua huzuni niliyo nayo kwa sababu ya msiba wao?"

Wakati Yoshua alipokuwa karibu na mji wa Yeriko, aliinua macho yake, na tazama palikuwa na mtu amesimama na upanga wazi mkononi, kumpinga. Yoshua alimwendea akasema, "Je, wewe u upande wetu, au upande wa adui zetu?" Yoshua 5:13.

Kama mtu yule aliyekutana na Yoshua angekuwa binadamu, jibu la swali lile lingekuwa, "Niko upande wenu," au "Niko upande wa adui zenu," au "Sina upande." Haya ndiyo majibu ya kibinadamu yawezayo kujibu swali kama lile. Lakini Yule ambaye Yoshua aliona alikuwa ametoka katika ulimwengu tofauti. Hivyo Yoshua alipomwuliza kama alikuwa upande wao, au upande wa adui zao, jibu lililotolewa lilikuwa gumu kufahamika, tena lisilotumainiwa: "La!" Nini maana ya neno "La?"

Yeye alikuwa amekuja kutoka katika ulimwengu ambao watu wake hawapendelewi wala kupingwa. Huo ni ulimwengu ambao kila mtu na kila kitu hufahamika na kuangaliwa kwa huruma na upendo pamoja na moto.

Pana usawa wa binadamu kule. Na kwa usawa ule sharti ukomunisti upingwe. Kwa usawa huu, lazima kuwapinga Wakomunisti vile vile, maana ndio waungao mkono mawazo haya ya kinyama na ukatili mbaya.

Lakini Wakristo ni zaidi ya watu wa kawaida. Wao ni watoto wa Mungu na washiriki wa ile asili takatifu.

Hivyo basi, yale mateso niliyopita katika gereza za Kikomunisti hayakunifanya niwachukie Wakomunisti. Maana hata wao ni viumbe wa Mungu. Nawezaje basi kuwachukia? Wala tena siwezi kuwa rafiki yao. Kwa sababu, urafiki maana yake ni kuwa na roho mbili katika kifua kimoja. Lakini mimi sina roho moja na Wakomunisti. Wao humchukia Mungu. Mimi nampenda Mungu. Hivyo ni wazi hatuwezi kuwa marafiki.

Kama ningeulizwa swali: "Je, wewe u upande wa Wakomunisti, au wawapinga?"

Bila shaka jibu langu lingekuwa na mambo mengi. Ukomunisti waleta hatari kuu sana kwa binadamu. Hivyo mimi ninaupinga kabisa. Tena ningependa kupambana nao mpaka ushindwe na kutoweka!

Lakini katika roho naketi mbinguni pamoja na Yesu. Naketi katika ule ulimwengu wa "La." Ulimwengu ambao Wakomunisti na makosa yao wanafahamika na kupendwa. Huu ni ulimwengu ambao malaika wanasaidia kila mtu apate maisha ya kibinadamu yaliyo kama ya Kristo. Kwa hiyo shabaha yangu ni kuhubiri Injili kwa Wakomunisti na kuwapa Habari Njema ya uzima wa milele."

Kristo aliye Bwana wangu anawapenda Wakomunisti. Yeye Kristo alisema kwamba ampenda kila mtu, na kwamba yu tayari kuacha wenye haki tisaini na tisa kuliko kumwacha mmoja apotee na kuangamia. Mitume wake pamoja na walimu wakuu wa Ukristo wamefundisha upendo huu wa jumla katika Jina lake.

Mtakatifu Macary alisema zamani, "Kama mtu anawapenda sana watu wote, ndipo aseme kwamba pana mtu mmoja ambaye hawezi kumpenda, basi mtu mwenye upendo wa jinsi ile siye Mkristo, kwa sababu upendo wake unabagua!"

Vile vile Mtakatifu Agustine alifundisha, "Kama binadamu wote wangekuwa wenye haki kasoro mtu mmoja tu ndiye awe mwenye dhambi, hata hivyo Kristo angekuja kufa msalabani kwa ajili ya mtu yule, maana Kristo ampenda kila mmoja!"

Mafundisho ya Kikristo yako wazi. Wakomunisti ni binadamu, na Yesu Kristo anawapenda vile vile. Hivyo ndivyo inavyompasa mtu yule aliye na nia ya Kristo kufanya. Twawapenda wenye dhambi ingawa twachukia dhambi. Twafahamu upendo wa Kristo kwa Wakomunisti jinsi ulivyo kutokana na vile sisi tunavyowapenda.

Mimi mwenyewe katika magereza ya Kikomunisti nilikwisha kuona wafungwa Wakristo wakiwa na ratli 50 za minyororo miguuni wakiteswa kwa kuunguzwa kwa vyuma vya moto vyekundu, wakilazimishwa kumeza vijiko vya chumvi bila maji, halafu wananyimwa chakula, wanapigwa na kuteswa kwa baridi. Lakini wafungwa wale wale waliwaombea Wakomunisti kwa bidii mno. Katika hali ya kibinadamu, neno kama hili haliwezekani kamwe. Ni upendo wa Kristo tu uliomiminwa mioyoni mwetu ndio uwezao neno kama hili.

Baada ya muda, Wakomunisti wale waliotutesa nao walifungwa gerezani. Katika hali ya ukomunisti, hata Wakomunisti au watawala wao, wote hutupwa gerezani mara kwa mara sawa kama wapinzani wao Wakristo. Ndipo watesaji na wateswaji wote walikuwa katika gereza moja. Wakati wafungwa wengine walipowachukia hawa wafungwa watesi wao hata kuwapiga, Wakristo waliwatetea, ingawa walilaumiwa kuwa nao wameshiriki ukomunisti. Niliwahi kuwaona Wakristo wafungwa wakitoa sehemu zao za mikate, (tulipata kipande kimoja

kwa juma), pamoja na dawa ambazo zingelilinda maisha yao, na kuwapa wale Wakomunisti watesaji waliofungwa.

Maneno ya mwisho ya Bwana Iuliu Maniu, Waziri Mkuu wa Rumania, Mkristo, aliyefia gerezani yalikuwa:

"Kama Wakomunisti wakipinduliwa katika nchi yetu hii, wajib mtakatifu wa kila Mkristo ni kwenda barabarani kuwalinda Wakomunisti kutokana na hasira kali ya haki ya watu wale waliowatesa."

Siku chache baada ya kumwamini Kristo, nilidhani sitaishi zaidi. Kila mara nilipotembea barabarani, nilisikia maumivu kama niliyechomwa kisu kikali moyoni kwa ajili ya swali kama wale watu nikutanao nao wamekwisha kuokoka ama sivyo. Kama Mkristo wa kanisa yetu akianguka dhambini, nilimlilia machozi muda wa saa nyingi. Shauku ya wokovu wa kila roho ilidumu moyoni mwangu, wala sitawabagua Wakomunisti.

Katika vyumba vile vidogo vya mtu kufungwa pekee, hatukuomba tena kama kwanza. Tulikuwa na njaa kali mno, isitoshe yale madawa ya kulevya tuliyopewa yalitufanya wajinga kupindukia! Tulikonda na kukondeana mpaka kuwa magofu ya watu – mifupa mitupu! Hata Sala ya Bwana ilitushinda kusema, ilikuwa ndefu mno! Licha ya urefu, hatukuweza kuikariri barabara. Maombi yangu mafupi niliyorudia tena na tena yalikuwa, "Yesu, ninakupenda!"

Ndipo siku moja tukufu nilipata jibu kutoka kwa Yesu, "Unanipenda? Sasa nitakuonyesha jinsi mimi ninavyokupenda wewe!"

Pale pale nilisikia mwali wa moto ukiwaka moyoni mwangu. Wale wanafunzi waliokuwa wakirudi toka Emmau walisema mioyo yao iliwaka moto wakati Yesu alipozungumza nao. Hata mimi nilikuwa vile. Nilifahamu upendo wa mmoja ambaye alitoa maisha yake msalabani kwa ajili yetu sote. Upendo kama ule hautabagua Wakomunisti hata kama dhambi zao ni nyingi kiasi gani!

Wakomunisti wametenda, na mpaka sasa wanatenda maovu makuu, lakini, "maji mengi hayawezi kuzima upendo, wala mafuriko ya maji kuugharikisha. Upendo una nguvu mithili ya kifo. Lakini chuki ina ukatili sawa na kaburi!"

Kama vile kaburi inavyowameza watu wote, tajiri kwa fukara, mzee kwa kijana, watu wa rangi zote wanaume kwa wanawake, watawala na wanasiasa, waadilifu kwa wakosaji; hali kadhalika upendo nao hujumlisha wote. Upendo wa utu wa Kristo hautakoma mpaka Wakomunisti nao wameokolewa.

Pasta mmoja alitupwa katika chumba chetu gerezani akiwa nusu mfu. Damu ilimtiririka vibaya usoni na mwili mzima. Alikuwa amepigwa vibaya mno. Tulimwosha majeraha yake. Baadhi ya wafungwa walianza kuwalaani Wakomunisti. Pasta yule hali akikoroma alisema, "Tafadhali msiwalaani! Nyamazeni! Nataka kuwaombea!"

## Tulivyoweza Kufurahi Hata Gerezani.

Wakati nitazamapo ile miaka kumi na minne niliyokaa gerezani, pengine huona kwamba ulikuwa ni wakati wa furaha. Wafungwa wengine hata na walinzi mara nyingi walishangaa sana kuona vile Wakristo walivyoweza kufurahi hata katika hali ya mateso mabaya. Haikuwezekana kukatazwa kuimba, ingawaje tulipigwa mara kwa mara tulipoimba. Mimi nafikiri chiriku angeimba tu hata kama anajua baada ya wimbo awezakuuawa. Wakristo wafungwa waliimba na kucheza kwa furaha gerezani! Je, iliwezekanaje wafurahi hivyo katika hatari mbaya ya kutisha namna hiyo?

Kila mara gerezani nilitafakari mno maneno ambayo Yesu aliwambia wanafunzi wake. "Heri macho yaonayo mambo yale mnayoyaona."

Yesu alisema maneno haya baada ya ziara ya Palestine pamoja na wanafunzi wake. Nao walikuwa wame-

ona mambo ya kutisha na kuogofya. Palestine ilikuwa nchi ya mateso wakati huo. Kila mahali palikuwa na hali mbaya ya huzuni wa watu walioteswa. Hivyo hata wanafunzi walikuwa wamepambana na maradhi, tauni, njaa na masikitiko ya kila aina.

Waliingia hata nyumba za wananchi waliokuwa wamekamatwa na kufungwa gerezani, hali wameacha wake na watoto wao katika maombolezo makuu. Huo haukuwa ulimwengu mwema kuangalia!

Hata hivyo Yesu alisema, "Heri macho yaonayo mambo yale mnayoyaona." Hii maana yake ilikuwa kwamba hawakuona mateso tu. Walikuwa wamemwona Mwokozi wa wote, na Mtimilizaji wa mambo mema yote, ambaye ni Lengo la Walimwengu wote. Tazama, muda mfupi wa kiangazi miti hupukutisha majani, nyasi hukauka, maua hayaonekani, ardhi huwa kavu na yenye vumbi. Lakini baada ya hayo, miti hupata majani mabichi mororo, nyasi mbichi kuchipuka, maua huchanua pote, ardhi hupendeza kutazama wala haina vumbi tena. Hivyo mateso ya muda huzaa furaha ya daima mbele za Mwenyezi Mungu.

Gerezani pande zote nilizungukwa na akina Ayubu wengi. Naam, wakiwa wanateseka zaidi ya Ayubu. Lakini nafahamu mwisho wa hadithi ya Ayubu ulivyokuwa. Alipata mara dufu ya mali ile aliyokuwa nayo kwanza.

Vile vile gerezani nilizungukwa na akina maskini Lazaro, wenye njaa na majeraha machafu yenye usaha. Lakini nafahamu malaika watawachukua mpaka kifuani mwa Ibrahim. Niliona vile watakavyokuwa baadaye. Wale wafia dini wanyonge na wachafu waliokuwa karibu nami niliwaona kuwa watakatifu wa kesho wakiwa wamevaa taji za utukufu.

Lakini kwa kufikiria watu hawa jinsi watakavyokuwa baadaye, pasipo kutazama hali yao ya sasa, niligundua akina Paulo wengi miongoni mwa watesaji wale kama

alivyokuwa Saulo wa Tarsus. Na baadhi yao walikwisha badilika hivyo. Maofisa polisi wa siri tuliowashuhudia waliokoka na kuwa Wakristo. Nao vile vile walitupwa gerezani pamoja nasi kwa ajili ya kumpokea Kristo wetu. Miongoni mwa walinzi wa gereza waliotupiga, tuliona uwezekano kama wa mlinzi wa gereza la Filipi, ambaye kwanza alimpiga Mtume Paulo, lakini akaamini baadaye. Tuliota ndoto kwamba karibuni nao watauliza, "Tufanye nini tupate kuokoka?" Miongoni mwa wale waliowadhihaki Wakristo waliopakwa mavi na mkojo hali wamefungwa misalabani, tuliona umati wa watu kule Golgotha ambao karibuni wangepigapiga vifua vyao kwa hofu kwamba wamekosa.

Ilikuwa gerezani tu ndipo tulipata tumaini la wokovu wa Wakomunisti. Sisi mle gerezani tulianzisha wazo la kuwa na wajibu mkuu kwao Kwa ajili ya kuteswa nao tulijifunza kuwapenda.

Jumla kubwa sana ya jamaa zangu waliuawa. *Lakini yule mwuaji wao aliamini Yesu akiwa nyumbani mwetu.* Na nafasi hiyo ndiyo ilifaa sana. Hivyo wazo la ujumbe wa Kristo kwa Wakomunisti lilizaliwa katika magereza ya kikomunisti.

Mungu huona mambo tofauti kabisa na vile tuonavyo sisi, ni sawa na tofauti baina ya kuona kwetu sisi na kule kwa sisimizi. Kwa mawazo ya kibinadamu, mtu kufungwa msalabani halafu kupakwa mavi na mkojo ni jambo ovu kuliko mpaka. Walakini Biblia huita mateso ya wafia dini kuwa ni "dhiki nyepesi." Vile vile kukaa gerezani miaka kumi na minne ni muda mrefu sana, bali Biblia yaita dhiki kama ile "muda kitambo, ambayo yatufanyia utukufu wa milele. . .!" Hili latupa haki kufikiri kwamba maovu haya ya Wakomunisti ambayo kwa hali ya kibinadamu siyo ya kusamehe, na tena kwa haki twayapinga vikali, machoni pa Mungu ni mepesi kuliko yalivyo machoni petu. Udhalimu wao ambao umedumu nusu karne kwa sasa, ni muda mfupi wa kupo-

toka tu mbele za Mungu ambaye kwake miaka elfu ni kama siku moja. Bado pana uwezekano wa kuokolewa kwao.

Mji Yerusalemu wa mbinguni ni kama mama, tena una upendo kama mama. Bado milango ya mbinguni haijafungwa ili Wakomunisti wasiingie. Wala taa zake bado hazijazimwa. Wakomunisti wanaweza kutubu sawa na mtu mwingine ye yote. Ni wajibu wetu tuwaite waje kutubu.

Upendo peke yake tu ndio uwezao kubadili Wakomunisti. Upendo huu sharti ubainike wazi pasipo kushiriki ukomunisti kama vile viongozi wengine wa makanisa kadha wafanyavyo. Chuki hupofusha. Hitler alipinga ukomunisti, bali alikuwa na chuki. Hivyo badala ya kuwashinda Wakomunisti, aliwasaidia kuteka theluthi ya dunia.

Kwa njia ya upendo mle gerezani tulipanga kazi za kuwahudumia Wakomunisti. Nasi pale pale tuliwafikiria watawala wa kikomunisti.

Wakurugenzi wa vyama vya kuhubiri Injili waonekana kufahamu machache sana kuhusu Historia ya Kanisa. Je, Ukristo uliingiaje katika nchi ya Norway? Mbona ilikuwa baada ya Mfalme wao Olaf kuamini! Kwanza, Urusi ilikuwa na Injili wakati Mfalme wao Vladimir alipoamini! Hungary nayo ilipata Injili baada ya kuamini Mfalme wao Mtakatifu Stefano! Hata katika nchi ya Poland mambo yalikuwa yale yale. Injili iliingia katika makabila mbalimbali ya Afrika wakati Watemi na Wafalme wao walipoamini. Sisi twapanga ujumbe wetu kwa watu wenye vyeo na wengine ambao huwa Wakristo hodari, bali hawana mvuto makali wa kuleta mabadiliko makubwa kwa nchi, kabila au taifa.

Sharti tuwahubiri watawala mpaka waamini. Wanasiasa, wakuu wa uchumi, watu wa sayansi, wataalamu wa kila namna, wote yafaa waamini. Maana watu kama hawa wanaweza kubadilisha mioyo ya watu haraka.

Watu wa jinsi hii hufinyanga mawazo na roho za watu haraka. Wakuu hawa wanapoamini, raia wao huamini haraka mno.

Kwa upande wa kazi za kuhubiri Injili kufuatana na mawazo ya jinsi hiyo, utaratibu wa Wakomunisti watoa njia rahisi mno. Serikali yao ina madaraka na uwezo mkuu mno!

Kama Raisi wa Amerika akiwa mfuasi wa dini ya Mormon, nchi nzima ya Amerika haiwezi kuwa chini ya dini ya Mormon. Maana Raisi wa Amerika hawezi kutoa amri kwa nchi nzima ikafuatwa na kila mtu. Lakini kama Mao Tse-Tung wa China akiamini na kuwa Mkristo, au hata Watawala wa Urusi wakiwa Wakristo, nchi zile zitahubiriwa Injili bila shida. Kwa sababu viongozi wale wana nguvu kuu katika nchi zao, tena wanao mvuto mkali sana kwa watu.

Je, kiongozi au mtawala wa Kikomunisti aweza kumwamini Yesu? Hakika yawezekana. Maana hata yeye hana furaha wala usalama, ni sawa na mateka wake. Karibu watawala wengi wa Urusi wametupwa gerezani au kupigwa risasi na wenzao (komredi). Hata Uchina ya kikomunisti mambo ni yale yale. Wale Mawaziri wa Mambo ya Ndani kama Iagoda, Iejov na Beria ambao walikuwa na uwezo wote mikononi, walitupwa kifungoni sawa kama watu wengine baki; mwishowe walipigwa risasi za shingo kama wenzao wa mapinduzi. Hivi karibuni Waziri wa Mambo ya Ndani wa Urusi, Bwana Shepelin, na yule wa Yugoslavia, Bwana Rankovic, wote wametupwa kama takataka na kusahaulika kabisa!

## Tuwezavyo Kushambulia Ukomunisti Kwa Njia Ya Kiroho.

Utawala wa Kikomunisti haumfurahishi ye yote. Hata wale wanaouendesha wana· hofu kuu kwamba usiku wo wote gari la askari wa siri laweza kuwazoa, kwamba maongozi ya chama yaenda tenge!

Mimi nafahamu viongozi wengi wa Kikomunisti ambao wana mzigo mzito. Ni Yesu peke yake awezaye kuwapumzisha.

Kuwaongoa watawala wa Kikomunisti mpaka kuamini, ni kuokoa ulimwengu mzima kutokana na kiini cha maangamizi mabaya. Tena ni kuokoa binadamu kutokana na njaa kuu inayokabili dunia nzima, maana fedha nyingi zatumika kutengeneza zana za vita. Hivyo kuamini kwa watawala wa Kikomunisti ni kutatua tatizo la mashaka ya dunia. Kuongoka na kuamini kwa watawala wa Kikomunisti ni kuwafurahisha Kristo na malaika wote. Huu waweza kuwa ushindi mkuu wa Kanisa la Kristo. Sehemu zile ambazo watumishi wa Mungu wataabika sana kuhubiri Injili zitafuata pasipo shida, kwa maana Ukristo utakuwa umepata mwenendo na nguvu mpya.

Mimi mwenyewe nawafahamu Wakomunisti waliomwamini Yesu. Isitoshe, hata mimi nilikuwa nikimkana Mungu kwanza katika ujana wangu. Mkomunisti na mtu amkanaye Mungu wanapotubu na kuokolewa, humpenda Kristo mno, sababu huwa wamefanya dhambi kuu mno mwanzoni.

Kazi za kutangaza Injili zahitaji mawazo ya busara. Kuhusu mawazo ya wokovu, roho zote zi sawa. Lakini kuhusu mawazo ya kazi za kuhubiri Injili, roho zi tofauti. Huleta maana kuu kama mtu mwenye mvuto mkali wa watu akiamini, maana ataleta watu wengine wengi kwa Kristo kuliko mtu mmoja tu kijijini akiamini na kuokoa roho yake. Hii ndiyo maana Yesu alichagua kumalizia huduma yake katika Yerusalemu, makao makuu ya kiroho, badala ya vijijini. Ni kwa sababu hii hii Paulo alipigana mpaka kufika katika mji wa Rumi.

Biblia yasema, "Uzao wa mwanamke utamponda nyoka kichwa." Bali sisi twamtekenya nyoka tumboni na kumfanya acheke. Kumbe kichwa cha nyoka kiko mahali fulani kati ya Moscow na Peking, wala siyo Tunis na Madagascar. Kanisa, Wakurugenzi wa Vyama vya ku-

hubiri Injili pamoja na kila Mkristo, wote wangehusika mno na ulimwengu wa Kikomunisti.

Sote tungetupilia mbali kawaida za kazi na taratibu za ofisini za kila siku. Imeandikwa, "Alaaniwe mtu yule afanyaye kazi ya Bwana kwa udanganyifu." Kanisa lapaswa kujitokeza mbele na kupambana na ukomunisti kwa njia ya kiroho.

Ushindi vitani hutokana na maarifa ya kushambulia wala siyo maarifa ya kujilinda. Katika shughuli za kupambana na ukomunisti, mpaka sasa Kanisa limekuwa likijilinda au kujitetea tu, hali likipoteza nchi moja moja na kuachia ukomunisti ustawi.

Kanisa yapaswa kubadilisha mwenendo huu upesi iwezekanavyo. Zaburi yasema kwamba Mungu huvunja-vunja vyuma. Kwa hiyo ile Ngome ya Chuma si kitu kwake.

Kanisa la kwanza lilifanya kazi kwa siri, tena pasipo ruhusa, lakini lilishinda. Hali kadhalika, yatupasa tena tujifunze jinsi ya kufanya kazi kwa njia ile ile.

Kabla ya Ukomunisti kuingia, sikufahamu kwa nini baadhi ya watu wa Agano Jipya walikuwa na majina ya fumbo kama: Simoni aliyeitwa Mweusi, Yohana aliyeitwa Marko, na mengineyo. Hata sisi kwa siri twatumia majina ya fumbo kazini mwetu katika nchi za Kikomunisti.

Nilikuwa sijatambua kwa nini Yesu alipotaka kula Pasaka ya mwisho hakuwapa jina na anwani kamili ya mtu yule, bali alisema, "Enendeni mjini, nanyi mtamwona mtu amebeba mtungi wa maji." Sasa ninafahamu maana yake. Hata sisi katika Kanisa la Siri twatumia alama maalum za siri kusudi kutambulisha.

Kama tukikubali kufanya kazi namna hii, yaani kutumia tena njia zile zilizotumiwa na Kanisa la

kwanza, tutafaulu kumtumikia Kristo katika nchi za Kikomunisti.

Lakini kila nikutanapo na Viongozi wa Makanisa katika nchi za Magharibi, badala ya kuwapenda Wakomunisti, neno ambalo lingeongoza shughuli za kuhubiri katika nchi za kikomunisti, naona mawazo tofauti kabisa kuhusu Wakomunisti. Sikuona huruma kama ya Msamaria Mwema kwa ajili ya roho zinazoangamia zilizo katika nyumba ya Karl Marx.

Kwa kweli mtu huamini mambo yale ambayo yu tayari kufa kwa ajili yake, wala siyo yale anayokariri katika imani yake.

Wakristo wa Kanisa la Siri walikwisha kuhakikisha kwamba wako tayari kufa kwa ajili ya imani yao. Mpaka sasa mimi mwenyewe naendelea na kazi ambayo yaweza kunifanya nifungwe tena katika nchi za Kikomunisti, niteswe zaidi mpaka kufa kwa sababu niliongoza ujumbe wa siri katika nchi hizo, nikiwa nimejitoa maisha yangu. Ninaamini mambo haya niyaandikayo.

Ninayo haki kuuliza, "Wale Viongozi wa Makanisa kule Ulaya, Amerika na Afrika ambao ni marafiki wa ukomunisti wako tayari kuacha vyeo vyao ili kuja kufa kwa ajili ya imani yao? Nani awazuiaye kuacha vyeo vyao hivyo ili kwenda kushika vyeo vya upasta katika nchi za Mashariki na kushirikiana na Wakomunisti huko? Uthibitisho wa imani hiyo bado haujapatikana kwa Kiongozi ye yote wa Kanisa kutoka pande za Magharibi ya Ulaya.

Maneno ya kibinadamu yaonyeshayo moyo wa kuhurumiana mtu na mwenzake hutokana na kufahamiana katika matendo ya pamoja kama biashara, uwindaji, uvuvi, na mambo mengine ya maisha. Walakini hakuna maneno ya kibinadamu yatoshayo kueleza mambo makuu ya kiroho ya Mwenyezi Mungu.

Hali kadhalika, hakuna maneno ya kibinadamu ya-

toshayo kueleza ukatili mbaya wa kishetani. Kwa mfano, mtu awezaje kueleza kwa maneno vile alivyojisikia mtu mwingine aliyekuwa karibu kutupwa katika tanuru wakati wa enzi za Nazi?

Au, wawezaje kueleza kwa maneno jinsi alivyojisikia mzazi ambaye aliona mtoto wake akitupwa katika tanuru?

Na ndivyo ilivyo kazi bure kujaribu kueleza kwa maneno mateso ambayo Wakristo waliteseka, na bado wanaendelea kuteseka katika nchi za Kikomunisti.

Nilikuwa gerezani na Bwana Lucretiu Patrascanu, mtu ambaye alisaidia Wakomunisti kutawala Rumania. Ndugu zake (komredi) walimlipa kwa kumtupa gerezani. Ingawa alikuwa mwenye akili timamu, lakini alifungwa katika hospitali ya wehu, mpaka naye akawa mwenda wazimu. Walifanya vile kwa Anna Pauker aliyekuwa Waziri wao wa Mambo ya Ndani. Wakristo hutendewa hivi mara kwa mara. Hupata kushtushwa kwa nguvu za umeme kila mara. Vile vile huzongwazongwa katika makoti magumu yasiyokunjika, nao hukaa wamenyoka hivyo tu muda mrefu.

Ulimwengu wote huogofishwa na matendo yatendekayo katika mabarabara ya Kichina. Katika mawazo ya kila mtu, wale Walinzi Wekundu huendesha vitisho vyao. Sasa fikiria yale yanayowapata Wakristo katika magereza ya Kichina ambako hakuna mtu aonaye.

Ushuhuda wa mwisho ni kwamba Mkristo maarufu wa dhehebu la "Chinese Evangelical" alikatwa mikono yake, miguu yake, pamoja na ulimi alipokataa kukana imani yake.

Kutesa na kuua watu silo ovu kuu kuliko yote watendayo Wakomunisti. Bali pia hudanganya mawazo ya watu na kutia sumu katika akili za vijana na watoto. Hutwaa Wakomunisti na kuwaweka katika madaraka kanisani ili waongoze Wakristo na kuharibu makanisa.

Vile vile huwafundisha vijana kutomwamini Mungu na Kristo, na kuyachukia majina hayo.

Je, ni maneno gani ya kibinadamu yawezayo kueleza msiba unaowapata Wakristo wateswao, halafu warudipo nyumbani wanakuta watoto wao wanawabeza vibaya baada ya kubadilika kuwa wamkanao Mungu.

*Kwa jumla kitabu hiki hakikuandikwa kwa wino tu, bali pia kimeandikwa kwa damu itiririkayo toka mioyo ya watu watesekao.*

Isipokuwa pana neno moja kuu. Kama vile ilivyokuwa wakati wa Daniel, wakati wale vijana watatu waliotupwa katika tanuru ya moto, walipotoka nje hawakunuka harufu ya moto. Ndivyo hivyo hata Wakristo ambao wamekuwa katika gereza za kikomunisti hawanuki harufu ya kuwachukia Wakomunisti.

Kama ukilikanyaga ua la waridi na kuliseta kwa mguu, litakuzawadisha manukato matamu matamu. Hali kadhalika, Wakristo walioteswa na Wakomunisti waliwatunukia watesaji wao na tunu ya upendo. Tuliwaleta wengi wa walinzi wetu kwa Kristo. Hivyo sisi twatawaliwa na neno moja kuu: kuwapa Wakomunisti waliotutesa, tunu kuu tuliyo nayo, yaani wokovu ambao wapatikana kwa Bwana wetu Yesu Kristo.

Mimi sikujaliwa kama baadhi ya ndugu zangu wengi walivyojaliwa, yaani kufia gerezani kwa ajili ya imani katika Kristo. Mimi nilifunguliwa toka gerezani na kuruhusiwa kutoka karika nchi ya Rumania mpaka nchi hizi za Magharibi.

Ajabu kuu ni kwamba katika nchi hizi za Magharibi nimekuta viongozi wa makanisa wakiwa na nia tofauti na ile inayotawala Kanisa la Siri katika nchi za kikomunisti. Wakristo wengi katika nchi za Magharibi hawana upendo wa Kikristo kwa Wakomunisti. Uthibitisho wa neno hili ni kwamba hakuna neno lo lote linalofanyika kuhusu wokovu wa watu wale walio katika

nchi za Kikomunisti. Makanisa mengi yana mipango ya kuhubiri Injili kwa Wayahudi, Waislamu na Wabuddha. Baadhi ya makanisa yana mipango ya kuhubiri na kuwashawishi Wakristo wa madhehebu mengine waingie katika dhehebu jingine. Walakini hakuna kazi za Mission kwa Wakomunisti. Ni dhahiri hawawapendi! La sivyo, wangekwisha unda kazi za mission kwa ajili ya Wakomunisti; kama vile Carey alivyowapenda Wahindi, na Hudson Taylor alivyowapenda Wachina hata wakaunda missioni zao.

Siyo kwamba Makanisa ya nchi za Magharibi hayafanya lo lote kuhusu wokovu wa Wakomunisti, bali kwa sababu ya utulivu na kutojali kwao, viongozi wa Makanisa haya huonekana kama wanawatia nguvu Wakomunisti kuendelea na udhalimu wa ukafiri wao. Wanawapa nafasi Wakomunisti kujidukiza katika makanisa ya Magharibi, kuwa waongozi makanisani na ulimwengu mzima. Maana Wakristo hawaamshwi kuiona hatari ya Wakomunisti.

Tendo hili la viongozi wa Makanisa ya nchi za Magharibi litaleta balaa la ukomunisti kung'oa Ukristo katika sehemu hizi vile vile.

## Fundisho Kutokana na Historia ya Dunia Limetupwa Mbali

Wakati wa karne ya kwanza, Ukristo ulikuwa na nguvu mno katika Afrika ya Kaskazini. Kule kule Afrika ya Kashazini kulitokea Mtakatifu Agustine, Mtakatifu Cyprian, Mtakatifu Athanasio na Mtakatifu Tertullian. Walakini Wakristo wa Afrika ya Kashazini walidharau wajibu wao mkuu mmoja tu; nao ulikuwa ni kuwaleta Waislamu kwa Kristo. Matokeo yake yalikuwa kwamba Waislamu walishambulia Afrika ya Kashazini na kufutilia mbali Ukristo mpaka karne hii! Mpaka sasa Afrika ya Kashazini iko chini ya dini ya Kiislamu, na Wakristo watangazao Injili kule wanaita sehemu hiyo, "sehemu ya watu wasiookolewa!"

Ebu sote tufundishwe na Historia hii.

Wakati wa Matengenezo ya Kanisa, matakwa ya Huss, Luther na Calvin yalipatana na matakwa ya watu wa Ulaya, yaani kutupilia mbali nira ya Papa ambayo ilisonga na kuzolotisha siasa na uchumi. Hali kadhalika hata leo hii, matakwa ya Kanisa la Siri ya kuhubiri Injili kwa Wakomunisti na wafungwa wao yanapatana na matakwa ya watu huru wapendao kuendelea kuishi kwa uhuru kamili.

Hakuna serikali wala nguvu ya siasa yo yote inayoweza kupindua ukomunisti. Wakomunisti wanazo silaha za nuklia. Hivyo kuwashambulia kwa njia ya vita ni kuamsha vita kuu duniani inayoweza kuangamiza mamilioni ya watu. Isitoshe, watawala wengi wa nchi za Magharibi wameoshwa akili zao wala hawawezi kupinga watawala wa kikomunisti. Mara nyingi wamesema vile. Hawa wangeridhika kuona ulevi, wizi, ugonjwa wa kansa na kifua kikuu vinatoweka, lakini sio ukomunisti ambao umekwisha kuangamiza watu wengi mno kuliko yale yote yakiwekwa pamoja.

Mwandishi wa Kirusi, Bwana Ilya Ehrenburg, alisema kwamba kama Stalin asingefanya kazi nyingineyo yote isipokuwa kuandika orodha ya mateka wake wasio na hatia aliowaua na kuwatesa, muda wote wa maisha yake usingetosha.

Siku ya kuadhimisha mwaka wa ishirini wa Chama cha Kikomunisti, Bwana Kruschev alisema, "Stalin aliangamiza maelfu ya Wakomunisti waaminifu wasio na hatia.—Wajumbe mia moja thelathini na tisa waliochaguliwa katika Mkutano Mkuu wa kumi na saba, tisaini na wanane, (wakiwa sabini kwa mia), baadaye walishikwa na kupigwa risasi."

Basi, kama Stalin alifanya vile kwa Wakomunisti wenzake, sasa fikiri alivyowafanyia Wakristo!

Kruschev alikanusha na kulaumu matendo ya Stalin,

ambavyo naye aliendelea kutenda yale yale. Tangu mwaka 1959, nusu ya makanisa ya Urusi yaliyokuwa bado yamefunguliwa, yalifungwa kabisa.

Kule Uchina pana mawimbi mapya ya ushenzi mbaya kuliko ule wa enzi za Stalin. Hakuna uhuru wa kuabudu wala wa kanisa kule! Mpaka sasa kule Urusi na Rumania, Wakristo waendelea kukamatwa. Hata sasa tumepokea habari kwamba Wakristo wengi mno wameshikwa.

Kwa njia ya vitisho na udanganyifu, nchi zile zenye watu zaidi ya mia moja milioni, zalea watoto kwa kuwafunza kuchukia hasa Ukristo.

Katika nchi ya Urusi ni jambo la kawaida kuwaona askari wamesimama milangoni pa makanisa wakiwapiga watoto wanaojaribu kuingia. Watoto huzuiwa kabisa na kutupwa nje. Kwa njia hiyo, viongozi wahalifu wa Kanisa la Kikristo katika nchi za Magharibi wanatayarishwa. Hiyo ndiyo njia ya kuwatayarisha viongozi waovu watakaoangusha Kanisa la Kikristo katika ulimwengu.

Pana nguvu moja tu peke yake iwezayo kupindua Ukomunisti. Ni nguvu ile ile moja iliyofanya Ukristo utawale katika giza la ushenzi mkuu wa Dola ya Warumi. Ni nguvu ile ile iliyosalimisha Ukristo kutokana na ukatili wa kishenzi wa Teuton na Vikings. Ni nguvu ile ile iliyopindua uwezo wa umwagaji wa damu wa Baraza Kuu la kuhukumu wazushi wa dini. Nguvu ile ni nguvu ya Injili ambayo yahubiriwa na Kanisa la Siri katika nchi zote za Kikomunisti.

Kuhifadhi na kuendeleza Kanisa silo swali la umoja na mateso tu ya ndugu Wakristo. Maana yake ni kufa au kuishi kwa ajili ya nchi yako na Kanisa lako. Kuhifadhi na kuendeleza Kanisa siyo tu matakwa ya Wakristo, bali sharti uwe wajibu wa kila serikali huru.

Kanisa la Siri limekwisha kuleta kwa Kristo baadhi

ya watawala Wakomunisti. Bwana Gheorghiu Dej,Waziri Mkuu wa Rumania alifariki baada ya kumwamini Kristo na kuungama dhambi zake, akawa mtu mwenye maisha mapya. Katika nchi nyingi za Kikomunisti wamo watawala wa serikali ambao ni Wakristo wa Siri. Neno kama hili laweza kuenea zaidi. Na hivyo tutaweza kutumaini badiliko kuu katika mwenendo wa serikali ya Kikomunisti. Mabadiliko haya siyo kama yale ya Tito na Gomulka ambao waliendelea kuwa watawala wa nguvu na wakatili waovu, lakini mabadiliko haya ni yale ya kuugeukia Ukristo na Uhuru.

Hii ndiyo nafasi peke yake maalum ya kutenda jambo kama hili.

Mara nyingi Wakomunisti ni waaminifu katika imani yao, sawa na vile Wakristo walivyo waaminifu katika imani yao. Lakini hata Wakomunisti nao wanapita katika wakati wa hatari kuu.

Wakomunisti walikuwa wakiamini kwamba Ukomunisti ungeleta upendo wa kindugu kati ya mataifa. Lakini sasa wanaona kinyume, kwani hata nchi zile za Kikomunisti zagombana zenyewe kwa zenyewe kama vile mbwa watoleanavyo meno.

Tena Wakomunisti walikuwa wanaamini kwamba Ukomunisti utabadili dunia hii iwe kama mbingu, kinyume cha ile mbingu ya Biblia wanayoita udanganyifu mtupu. Bali sasa watu wao wana njaa kali. Hata ngano wanaagiza kutoka katika nchi za watu wale wanaowaita makabaila au makapitalisti!

Wakomunisti waliamini na kuwatumaini sana viongozi na watawala wao. Lakini sasa wamekwisha kusoma katika magazeti yao wenyewe kwamba Stalin alikuwa mwuaji mkuu, na Kruschev alikuwa baradhuli. Mambo yaya haya yametukia kwa mashujaa wa taifa lao kama Rakosi, Gero, Anna Pauker, Rankovici na wengineo.

Wakomunisti hawaamini tena kwamba viongozi wao ni watu wasiokosa.

Mioyo mingi ya Wakomunisti ina ukiwa wa ajabu. Ukiwa huu waweza kujazwa na Yesu Kristo tu. Kwa asili moyo wa binadamu huelekea kumhitaji Mungu. Pana ukiwa wa kiroho maishani mwa kila binadamu mpaka Yesu Kristo tu aujaze. Neno hili li kweli hata kwa Wakomunisti. Lakini Injili ina nguvu ya upendo unaoweza kuwafikia hata wao. Mimi nilikwisha kuona neno hili likitukia. Tena ninafahamu wazi kwamba yawezekana kutendeka.

Wakristo wale waliodhulumiwa na kuteswa na Wakomunisti walikwisha kusahau na kusamehe yote yale yaliyotendeka kwao na kwa jamaa zao. Nao wanajitahidi kwa bidii zao zote ili Wakomunisti wavuke katika hatari na kupata kumwona Kristo. Hivyo wanahitaji msaada wetu kwa ajili ya kazi yao hii.

Wala siyo kwa ajili ya kazi hii peke yake, maana Upendo wa Kikristo ni kwa ulimwengu wote, wala haubagui.

Yesu alisema kwamba jua la Mungu huangazia watu wote, wema na waovu. Hata Upendo wa Kikristo ni hali kadhalika.

Wale viongozi wa Kikristo katika nchi za Magharibi wanaofanya urafiki na Wakomunisti wanajitetea kwa kutumia mafunzo ya Bwana Yesu kwamba ni lazima tuwapende hata adui zetu. Lakini wanasahau ukweli kwamba kamwe Yesu Kristo hakufundisha kuwa lazima tuwapende adui zetu *tu*, na kusahau ndugu zetu.

Hawa wanaonyesha upendo wao kwa kuwanywesha na kuwalisha watu wale ambao mikono yao imejaa damu ya Wakristo, badala ya kuwapa Habari Njema ya Kristo. Walakini watu wale wateswao na Wakomunisti wanasahauliwa wala hawapendwi!

Katika muda wa miaka saba, Makanisa ya Kiroma

na Kievangeli yaliyo Ujerumani ya Magharibi yalitoa Shilingi 875,000,000 kusaidia wenye shida ya njaa. Tena Wakristo wa Amerika walitoa zaidi.

Ndiyo, pana watu wengi wenye njaa. Lakini sidhani kuwa pana watu walio na njaa na wenye kuhitaji msaada kama huo kuliko Wakristo wateswao na kuuawa na Wakomunisti. Kama Makanisa ya Ujerumani, Uingereza, America na nchi za Scandinavia yanachanga fedha za msaada wa njaa, fedha hizi lazima zipelekwe kwa kila mtu mwenye kuhitaji. *Lakini kwanza zingekwenda kwa Wakristo wateswao, pamoja na jamaa zao.* Je, ni kweli ndivyo hivyo inavyofanyika?

Mimi mwenyewe nilikombolewa kwa fidia iliyolipwa na vyama vya Kikristo. Tendo hili lathibitisha kuwa Wakristo wanaweza kukombolewa. Walakini huenda ni mimi tu peke yangu niliyepata kukombolewa kwa fidia kutoka katika nchi yangu. Na ukweli wa fidia ya ukombozi wangu washtaki vyama vya Kikristo katika nchi za Magharibi kwa kutojali kutimiza wajibu wao katika mambo mengi.

Wale Wakristo wa kwanza walijiuliza kama lile Kanisa jipya lilikuwa la Wayahudi tu, au hata watu wa mataifa mengine vile vile? Swali lao lilipata jibu kamili. Kwa namna nyingine, matatizo yale yale yametokea tena katika karne ya ishirini. Ukristo sio wa nchi za Magharibi peke yake Wala Yesu Kristo siye wa America, Uingereza wala nchi nyingine za kidemokrasi. Na wakati Yesu aliposulibiwa msalabani, mkono wake mmoja ulinyoshwa kuelekea Magharibi, na mwingine Mashariki. Yeye alitaka awe Mfalme wa Wayahudi na watu wa mataifa mengine pia - awe mfalme wa Wakomunisti vile vile, wala sio ulimwengu wa Magharibi tu.

Yesu mwenyewe alisema, "Enendeni ulimwenguni *mwote* na kuhubiri Injili kwa *kila* kiumbe."

Kristo mwenyewe alitoa damu yake kwa ajili ya

wote, na wote wasikie na kuamini Injili.

Jambo moja linalotutia moyo kuhubiri Injili katika nchi za Kikomunisti ni kwanba pana watu wanaokuwa Wakristo walio na upendo na wivu. Sikupata kumwona Mkristo Mrusi mwenye uvuguvugu katika imani. Wakomunisti wanaweza kuwa wanafunzi wa Kristo walio maalum na wa pekee.

Kristo anawapenda Wakomunisti, na anataka sana kuwafungua kutoka katika ukomunisti, kama vile anavyowafungua watu wengine kutoka dhambini. Shabaha hii siyo inayochukuliwa na viongozi wa makanisa ya Magharibi, bali waonekana kuridhika na kutojishughulisha na ukomunisti. Na kwa hali ile wanapendelea dhambi na kusaidia kufaulu kwa ukomunisti, wakipinga wokovu wa Wakomunisti na wafungwa wao.

## Niliyoyaona Baada ya Kufunguliwa Kwangu

Nilipofunguliwa kutoka gerezani, nilimkuta mke wangu akiningojea, ndipo tukaishi pamoja tena. Mara moja mke wangu aliniuliza mpango niliokusudia kutimiza baadaye. Ndipo nilimjibu, "Mpango ulio dhahiri mbele yangu ni kuwa mtawa wa kiroho." Naye alijibu kwamba hilo ndilo lilikuwa wazo lake hata yeye.

Katika ujana wangu, nilikuwa na uwezo wa pekee. Lakini mle gerezani, hasa muda ule niliofungwa peke yangu chumbani, nilibadilika kuwa mtu mwenye kutafakari na kutazamia mno. Ile dhoruba kali iliyokuwa moyoni mwangu ilibadilika kuwa shwari. Sikuhanghaishwa wala kujali ukomunisti. Sikuutambua tena hata kidogo. Maana nilikuwa nimekumbatiwa na Bwana Arusi wa mbinguni. Niliwaombea wale wote waliotutesa, tena niliwapenda kwa moyo wangu wote.

Tumaini la kufunguliwa kwangu lilikuwa jembamba kama unywele. Kama ingewezekana nifunguliwe, kila mara nilikuwa nikiwazia jambo la kufanya. Kila mara nilipokuwa katika bahari ya mafikara hivyo, wazo moja

lilikuja, nalo lilikuwa kujitenga mahali fulani jangwani ili kuendelea kuwa na ushirika na Bwana Arusi wa mbinguni.

Mungu ni "Kweli." Biblia ni "kweli kuhusu Kweli." Elimu ya mambo ya Mungu ni "kweli kuhusu kweli, kuhusu Kweli." Mafundisho ya dini ni "kweli kuhusu kweli, kuhusu kweli, kuhusu Kweli." Hivyo Wakristo wengi hukaa katika hizi kweli nyingi zihusuzo"Kweli," wala hawana "Kweli."

Sisi gerezani kwa kuwa tulikuwa na njaa, tulipigwa na kuleweshwa na madawa aina aina, tulisahau elimu ya mambo ya Mungu na Biblia. Hivyo tulikuwa tumesahau "kweli kuhusu Kweli," na kwa jinsi hiyo tuliishi katika "Kweli." Kwa maana imeandikwa, "Mwana wa Adamu atakuja wakati msioudhani na siku msiyoijua." Sisi hatukuweza kufikiri tena. Hivyo wakati wa giza kuu ya mateso yetu Mwana wa Adamu alikuja kwetu, akiangaza kuta za gereza na kuzifanya zimeremete kama almasi hata kujaza vyumba vyetu kwa nuru safi. Kwa namna nyingine, mateso toka miilini mwetu yalifukuziwa mbali. Bali roho zetu zilifurahi katika Bwana. Wala tusingekubali kupoteza furaha yetu ile kwa sababu ya tumaini la kuingia Ikulu kule mbinguni.

Kupingana na mtu au kitu cho chote ni jambo ambalo sikuliwaza akilini mwangu. Sikutaka kupigana vita hata kama ni ya haki kiasi gani. Nia yangu ilikuwa kujenga maisha hai yaliyo safi kwa ajili ya Kristo. Nilifunguliwa kutoka gerezani nikiwa na tumaini hili moyoni mwangu.

Lakini tangu siku ile ya kufunguliwa kwangu, nilipambana na mandhari mbaya ya ukomunisti ambao haukulingana na aina yo yote ya mateso niliyoyapata gerezani. Viongozi wa Makanisa, mapasta, hata maaskofu niliokutana nao, kila mmoja aliungama kwamba alikuwa mpeleka habari na msaliti wa kundi lake kwa askari Wakomunisti. Mimi niliwauliza kama walikuwa

tayari kuacha kazi hiyo, hata kama itawalazimu kufungwa. Majibu yao wote yalikuwa, "Sivyo!" Walijitetea kuwa hawakusema vile kwa sababu ya hofu, lakini kwa ajili ya mambo mapya yaliyotukia kuhusu makanisa, ya kwamba wasipofanya vile yatafungwa.

Katika kila mji kulikuwa na Naibu wa Serikali wa kutawala dini, Mkomunisti, askari polisi wa siri. Huyu alikuwa na madaraka wakati wo wote kumwita pasta na kumwuliza nani wahudhuriao ibada na kushiriki Meza ya Bwana kila mara, au ni nani walio na wivu wa dini yao, nani ahubiriye watu hata wakaamini, au watu huungama nini, na mengineyo.

Kama pasta asipojibu, basi anafukuzwa na kufutwa kazi, ndipo mtu mwingine huchaguliwa kushika nafasi yake. Asipopatikana mtu mwingine wa kushika nafasi yake (neno lililotukia kwa nadra), yule ofisa hulifunga kanisa lile.

Hivyo wachungaji wengi walitoa habari kwa askari polisi. Baadhi ya wachungaji hawa walifanya vile pasipo kutaka, hata walificha mambo mengi. Lakini wengine ilikuwa kawaida yao, wala dhamiri zao hazikuwashtaki. Hata hivyo baadhi ya wachungaji wa makanisa walikuwa na hamu sana kupeleka habari, nao walisema mengi hata wasiyoulizwa.

Watoto wa wafungwa Wakristo nao waliungama vile walivyolazimishwa kutoa habari za jamaa zile zilizowakaribisha na kuwafadhili. La sivyo, walitishwa kufukuzwa shuleni.

Siku moja nilikwenda katika kanisa moja ya Kibaptisti iliyokuwa chini ya bendera Nyekundu ya Kikomunisti. Katika kanisa hii, Wakomunisti walikuwa wamechagua viongozi wa kanisa zima.

Ndipo nilitambua kwamba yale makanisa ya wazi katika nchi za Kikomunisti yalikuwa na viongozi waliochaguliwa na chama cha Kikomunisti. Mara moja nili-

kumbuka kwamba nilikuwa nikiona "machukizo ya uharibifu yakiwa mahali Patakatifu sana," kama alivyosema Bwana Yesu.

Kweli mara nyingi walikwisha tokea mapasta wema na wahubiri wabaya. Sasa kwa mara ya kwanza katika Historia ya Kanisa, Baraza la Kamati Kuu linalochagua viongozi wa kanisa ni la watu wasioamini Mungu, ambao wanatangaza wazi kuwa wananuia kufutilia mbali Ukristo. Je, watu wa namna hiyo wataongoza Kanisa kutimiza shabaha gani? Ni dhahiri, shabaha ni kufutilia mbali Ukristo.

Mkomunisti Lenin aliandika:

"Kila wazo la dini, kila wazo lihusulo Mungu, hata kama ni wazo la mchezo tu juu ya Mungu, ni upotovu wa hatari kuu mno isiyosemeka, tena ni maambukizo ya kuchukiza mno. Dhambi milioni nyingi, ufisadi, maasi ya kupigana na maambukizo ya maradhi ya mwili, havina madhara kama hila ya mawazo ya kiroho juu ya Mungu."

Vyama vyote vya Kikomunisti katika Urusi vyafuata mawazo ya Lenin. Kwao dini ni mbaya kuliko magonjwa kama kansa, kifua kikuu na kisonono. Ajabu kuu! Kwani watu hawa hawa ati ndio wanakata shauri na kuchagua viongozi wa kanisa! Waongozi wa makanisa nao hushirikiana na watu hawa!

Nimekwisha kuona vijana wengi wakitiwa sumu ya ukafiri – kutomwamini Mungu, hali Makanisa hayapingi na kupambana na jambo hili. Hakuna kanisa yo yote katika mji mkuu Bucharest ambayo yaweza kuongoza mikutano ya vijana, au hata Sunday School. Watoto wa Wakristo wanalelewa katika mafunzo ya chuki.

Nilipoyaona mambo haya yote, nilichukia Ukomunisti kuliko nilivyouchukia wakati Wakomunisti walipokuwa wakinitesa gerezani.

Chuki yangu haikutokana na vile walivyonitesa, bali ilitokana na uovu mkuu utendwao juu ya utukufu wa Mungu, kwa Jina la Kristo, pamoja na roho nyingi wanazotawala.

Wakulima wengi toka kote nchini walifika kuniona, wakisimulia vile mashamba ya ushirika yalivyoendeshwa. Sasa walikuwa watumwa wa njaa ya kila mara katika mashamba yao wenyewe. Hawakuwa na mikate wala maziwa na matunda ya kutosha. Neno kama hili ni ajabu kutokea katika nchi ambayo ina rutuba sawa na Kanaan ya zamani!

Ndugu wengi waliungama vile utawala wa Kikomunisti ulivyowabadili kuwa wezi na waongo. Wakati wa njaa sharti waibe mazao yaliyokuwa yao, lakini yamekuwa mali ya mashamba ya ushirika. Ndipo lazima waseme uwongo kusudi wasigundulike!

Wafanya kazi viwandani walieleza vile wanyonywavyo nguvu zao hata kuliko ambavyo makabaila wasingedhani kufanya. Tena wafanyakazi hawana haki ya kulalamika licha ya kugoma.

Walimu na wenye ujuzi lazima wafundishe kinyume cha imani yao, kwamba hakuna Mungu.

Uzima na mawazo ya theluthi moja ya binadamu ulimwenguni vimekwisha kuharibiwa na kudanganyika.

Vile vile wasichana wengi walieleza namna walivyokemewa na kutishwa katika chama Cha Vijana Wakomunisti, kwamba walishirikiana na kubusu vijana Wakristo. Nao hupewa majina ya vijana wanaoweza kushirikiana na kubusu.

Kila neno lilikuwa uwongo na uovu mkuu mno.

Ndipo nilikutana na mashujaa wa Kanisa la Siri, wale wenzangu wa zamani ambao baadhi hawakukamatwa, na baadhi walifungwa na kufunguliwa baadaye, nao

wakaendelea tena na huduma yao ile ile. Walinikaribisha kusudi tuendelee tena na vita yetu. Nilipata kuhudhuria mikutano yao ya siri, nasi tuliimba tukitumia vitabu vya nyimbo zilizoandikwa kwa mkono.

Pale pale nilimkumbuka Mtakatifu Anthony Mkuu aliyekuwa amekaa jangwani miaka thelathini. Hivi alikuwa amejitenga na mambo ya ulimwengu kusudi apate kuishi maisha ya kufunga na kuomba. Lakini aliposikia habari ya ugomvi na mabishano makali kati ya Mtakatifu Athanasio na Arius juu ya Uungu wa Kristo, mara moja aliacha maisha yake ya kujitenga, ndipo akaenda Alexandria, Misri, ili kusaidia na kutetea kweli ipate kufaulu.

Vile vile nilimkumbuka Mtakatifu Bernard de Clairvaux, mtawa aliyekuwa amejitenga milimani. Lakini alisikia matendo ya kipumbavu ya Vita Takatifu (Crusades), jinsi Wakristo walivyoua Waarabu, Wayahudi na ndugu zao wengi waliokuwa wafuasi wa imani nyingine kusudi wakomboe kaburi tupu la Yesu. Mara moja aliacha nyumba ya Utawa na kuanza kuhubiri akipinga vita ya Crusades.

Hali kadhalika, hata mimi nilikata shauri kufanya yote ambayo Wakristo wote wanafanya, kufuata mfano wa Kristo, Mtume Paulo na Watakatifu wengineo. Nilikata shauri kutupilia mbali wazo la kustarehe na kuanza vita tena.

Je, vita hii itakuwa ya namna gani?

Wakristo wengi gerezani walikuwa wakionbea adui zao na kuwashuhudia vizuri sana. Shauku kuu ya roho zetu ilikuwa kwamba waokolewe, nasi tulishangilia kila mara jambo kama hili lilipotukia.

Lakini mimi nilichukia utaratibu mbaya wa Kikomunisti. Hivyo nilitamani mno kuimarisha Kanisa la Siri, ambalo ndiyo nguvu pekee iwezayo kupindua udhalimu mbaya huu kwa kutumia uwezo wa Injili. Sikufikiria

nchi ya Rumania tu, bali ulimwengu wote wa Kikomunisti.

Walakini nilikuta hali ya kutohusika na huduma ya namna hii katia nchi za Magharibi.

Magazeti ya dunia nzima yalipinga hukumu ya kifungo iliyotolewa na Wakomunisti kwa waandishi wawili wa Kikomunisti, Siniavski na Daniel. Lakini hakuna lo lote linaloandikwa kupinga, wala makanisa hayapingi wakati Wakristo wanapofungwa gerezani kwa sababu ya imani yao.

Nani anayejali habari za ndugu Kuzyck aliyehukumiwa kufungwa ati kwa sababu ya kueneza "sumu", yaani vitabu vya Kikristo? Vitabu hivi vilikuwa vya maombi vilivyoandikwa na Torrey akiingiza sehemu za Biblia!

Je, ni nani ajuaye habari za ndugu Prokofiev aliyehukumiwa kifungo kwa sababu ya kueneza mahubiri yaliyoandikwa? Ni nani aliye na habari za Myahudi Mkristo, Grunvald aliyehukumiwa kwa kosa lile lile katika Urusi, ambaye tena Wakomunisti walichukua mtoto wake maisha? Mimi nafahamu nilivyojisikia wakati nilipochukuliwa kutoka kwa mwanangu Mihai. Hivi nateseka pamoja na Ndugu zangu Grunvald, Ivanenko, Granny Shevchuk, Taisya Tkachenko, Ekaterina Vekazina, George Vekazin na wengine wengi mno. Wote hawa ni watakatifu na mashujaa wa imani katika karne ya ishirini. Nainama kubusu minyororo yao kama vile Wakristo wa kwanza walivyobusu minyororo ya wafungwa wenzao wakati wakiongozwa kutupwa katika matundu ya wanyama wakali.

Baadhi ya viongozi wa Makanisa ya Magharibi hawajali watu hawa. Hata majina ya wafia dini na wateswao hayaonekani katika orodha ya maombi yao ya kila siku. Wakati watu hawa walipokuwa wakihukumiwa na kuteswa, Viongozi wa Makanisa ya Kirusi waliowa-

kana na kuwasaliti walikuwa wakipokelewa kwa heshima katika mikutano kule New Delhi na Geneva. Kule, viongozi hawa walimhakikishia kila mtu kwamba Urusi pana uhuru wa dini na kuabudu.

Kiongozi wa Umoja wa Makanisa alimbusu Askofu Mkuu wa Kirusi, Nikodim, baada ya kutoa uthibitisho kama huo. Ndipo wote pamoja walikula karamu kuu katika jina la Umoja wa Makanisa! Kumbe, watakatifu gerezani wanalishwa maboga na matumbo machafu yasiyooshwa, kama vile nilivyokula gerezani kwa ajili ya Jina la Yesu!

Mambo yasingeliendelea vivi hivi. Kanisa la Siri lilikata shauri niondoke nchini kama ingewezekana, kusudi niwafahamishe Wakristo wote ulimwenguni mambo yanayotukia katika nchi za Kikomunisti.

Mimi nimekwisha kukata shauri kushutumu "ukomunisti," ingawa nawapenda "Wakomunisti." Wala sioni haki kuhubiri Injili pasipo kushutumu na kulaumu ukomunisti.

Baadhi ya watu huniambia, "Hubiri Injili halisi tu!" Neno hili lanikumbusha vile nilivyoambiwa na polisi wa siri wa Kikomunisti. Nao vile vile waliniambia nihubiri Kristo, lakini nisitaje ukomunisti. Ndivyo ilivyo kwamba watu wale wanaopenda "Injili halisi" wanaongozwa na roho kama wale polisi wa siri?

Jambo la kwanza, hiyo "Injili halisi" yenyewe siijui! Je, mahubiri ya Yohana Mtakatifu yalikuwa halisi? Mbona yeye hakusema tu, "Tubuni, kwa maana Ufalme wa Mungu umekaribia." Bali alisema tena, "Wewe Herode u mbaya!" Hata alikatwa kichwa kwa ajili hiyo, maana mahubiri yake hayakuwa ya kupulizia upande mmoja.

Yesu naye hakuhubiri ujumbe "halisi" pale mlimani, lakini hata alilaumu na kusema, "Ole wenu Waandi-

shi na Mafarisayo, wanafiki — enyi uzao wa nyoka!"

Ni kwa ajili ya hayo mahubiri "yasiyo safi" kwamba alisulibiwa. Mafarisayo wasingelighafirishwa na Mahubiri ya Mlimani.

Wakati wa kuhubiri lazima dhambi itajwe kwa jina lake. Ukomunisti ndiyo dhambi ya hatari kuu sana leo ulimwenguni. Na Injili ile isiyoshutumu na kulaumu ukomunisti siyo Injili halisi. Kanisa la Siri laushutumu ukomunisti, likijitoa uhai wake na uhuru. Hata sisi hapa Magharibi na penginepo haitupasi kuwa kimya.

Mimi mwenyewe nimekata shauri kushutumu ukomunisti, lakini siyo kwa njia ile watumiayo wale wajulikanao kama "wapinga-ukomunisti." Hitler alikuwa mpinga-ukomunisti, walakini alikuwa mdhalimu. Sisi twachukia dhambi, bali twampenda mwenye dhambi.

## Kwa Nini Nateseka Zaidi Katika Nchi Za Magharibi

Ninateseka sana katika nchi za Magharibi kuliko nilivyoteseka katika nchi za Kikomunisti. Asili ya mateso yangu ni kupata uchu mwingi kwa ajili ya wema wa Kanisa la Siri linalomhubiri Kristo katika nchi za Kikomunisti.

Katika kambi za Kikomunisti, Mwana wa Adamu pamoja na watu wake hawana mahali pa kulaza vichwa vyao. Kule Wakristo hawajengi majumba yao ya kuishi. Kujenga nyumba mpya inaweza kuwa sababu ya kukamatwa na kufungwa kusudi Wakomunisti wachukue nyumba ile. Kule huna sababu ya kumzika baba yako wala kuaga jamaa yako kabla ya kumfuata Yesu. Nani basi, baba, mama, au dada yako? Kwa namna fulani wafanana na Yesu. Kwako, mama na ndugu zako ni wale wanaotimiza mapenzi ya Mungu! Kuhusu maisha ya jamaa, haiwezekani kukaa pamoja. Kwani mara nyingi hutukia kwamba, bibi arusi humkana bwana arusi, mwana huwakana wazazi, na wake huwakana waume zao! Kwa sasa zaidi umebaki ujamaa wa kiroho tu.

Kwa vingine, Kanisa la Siri ni maskini na lenye kuteseka mno, lakini halina Wakristo wanyonge wenye uvuguvugu.

Mkutano wa ibada katika Kanisa la Siri ni kama vile ilivyokuwa katika Kanisa la kwanza miaka elfu moja mia tisa iliyopita. Mhubiri hajui elimu yo yote ya Biblia. Wala hajui kanuni za kuhubiri na hatua zake, ni kama vile Petro alivyokuwa. Kila mwalimu mkuu wa mahubiri angempa Petro sifuri kwa ajili ya mahubiri ya siku ya Pentekoste. Hali kadhalika, katika nchi za Kikomunisti aya za Biblia hazijulikani, maana Biblia ni haba sana kule. Isitoshe, huenda mhubiri ameishi gerezani miaka mingi bila kuwa na Biblia.

Wakati Wakristo hawa wanapoonyesha imani yao katika Mungu Baba, huwa na maana kuu kwa sababu pana tamasha ifuatanayo na imani yao. Kila siku gerezani wanamwomba Mwenyezi Mungu awaruzuku kwa mkate, lakini badala ya mkate hupata maboga na matumbo machafu ajabu! Hata hivyo wanamwamini Mungu kwamba yu Baba mwenye upendo. Wao ni kama Ayub aliyesema hata kama Mungu angemchinja, yeye atazidi kumwamini tu. Tena ni kama Yesu aliyemwita Mungu "Baba" hata saa ile aliyojiona ameachwa.

Mtu ye yote aliyekwisha tambua uzuri wa kiroho wa Kanisa la Siri, hawezi kuridhishwa tena na ukiwa wa baadhi ya makanisa ya nchi za Magharibi.

Ninateseka zaidi katika nchiza Magharibi kuliko vile nilivyoteseka katika nchi za Kikomunisti. Maana kwa macho yangu naona ustaarabu wa Magharibi ukifa.

Bwana Oswald Spengler aliandika katika kitabu chake KUANGUKA KWA MAGHARIBI:

"Unakufa! Nakuona unazo dalili maalum za kuoza! Ninaweza kuthibitisha kwamba utajiri wako mwingi, ufukara wako mkuu, ukabila wako, ujamaa wako, vita vyako, mapinduzi yako, ukafiri wako, misiba yako, dharau

yako, ufisadi wako, talaka zako, mipango yote ya uzazi, yote haya yakufanya uchuruzike damu na kufa akilini. Kwani mambo yaya haya ndiyo yaliyokuwa dalili za kufa kwa dola za zamani kama Makedonia, Uyunani na Rumi!"

Habari hizi ziliandikwa katika mwaka 1926, lakini tangu pale nusu ya nchi za Ulaya mpaka Cuba zimekwisha kupoteza demokrasi na ustaarabu wake. Isitoshe, nchi nyingine za Magharibi zimelala usingizi.

Lakini pana jeshi lisilosinzia, nalo ni jeshi la Kikomunisti. Ingawaje katika sehemu za Mashariki udanganyifu wa Wakomunisti hauna nguvu kali, lakini ukomunisti umeenea zaidi, tena unazidi kuwa sumu mbaya katika sehemu za Magharibi vile vile. Lile wafanyalo Wakomunisti wa Magharibi ni kukanusha tu bahari za mateso na ukatili mbaya utendekao katika nchi za Kikomunisti. Wakomunisti huzidi kutangaza imani yao pote kwa wivu mkuu bila kuchoka. Matangazo yao huenda po pote katika majumba yote ya starehe, katika Vyuo vikuu na vidogo, miongoni mwa wanaelimu, katika Makanisa na kati ya watu fukara. Sisi Wakristo twaonekana kuamini matangazo yao kwa moyo wote kuwa ni ya kweli. Kumbe wao wanaamini uwongo ule kwa mioyo yao yote. Na wakati huo huo walimu wakuu wa mambo ya Mungu wanajadiliana upuzi.

Mambo haya kwa jumla yananikumbusha kisa kimoja wakati majeshi ya Mahomet II yalipouhusuru na kuuzunguka mji wa Constantinople mwaka 1493. Neno kuu la wakati ule lilikuwa kukata shauri kama nchi zile za Balkans zingedumu chini ya Ukristo, au kuwa chini ya dola ya Kiislamu. Na katika mji ule ule uliokuwa umezungukwa na maadui, baraza moja la kanisa lilijadiliana matatizo haya:-

1. Je, macho ya Bikira Mtakatifu yalikuwa ya rangi gani?

2. Je, Malaika ni wanaume au wanawake?

3. Je, kama inzi akitumbukia katika maji Matakatifu, naye atakuwa safi, au atakuwa ameyatia yale maji unajisi?

Matatizo haya yaweza kuwa ni hadithi tu ya wakati ule. Lakini chunguza kwa makini magazeti ya Makanisa katika siku za leo. Bila shaka utagundua kuwa maswali kama haya ndiyo hujadiliwa. Vitisho vya Ukomunisti na mateso ya Kanisa la Siri hayajadiliwi kamwe.

Pana majadiliano yasiyokoma kuhusu habari ya Mungu, kawaida za dini na mambo yasiyo lazima.

Baadhi ya Watu walikuwa wakijiburudisha katika chumba cha starehe. Mmoja wao aliuliza swali:

"Tuseme ulikuwa ukisafiri katika meli fulani, nayo izame, nawe kwa bahati uokoke mpaka kisiwa fulani hali imewezekana kuchukua kitabu kimoja toka maktaba ya meli. Je, utachukua kitabu gani?"

Mtu mmoja alijibu, "Biblia!" Mwingine alisema, "Shakespear!" Lakini mwandishi mmoja alitoa jibu la haki. "Mimi nitachagua kitabu cha kunifunza jinsi ya kuunda mashua na kurudi nchi kavu. Huko nitakuwa huru kusoma kila kitabu nipendacho."

Kudumisha uhuru wa madhehebu na mafundisho ya dini, pamoja na kusikitika mno kwa ajili ya sehemu ambazo zimepoteza uhuru huo kwa sababu ya mateso ya ukomunisti, ni jambo muhimu kuliko kukazania majadiliano ya dini.

Yesu alisema, "Kweli huweka huru." Lakini hali kadhalika ni "uhuru peke yake tu unaoweza kuleta kweli." Hivyo badala ya kugombania mambo yasiyo na maana, ingekuwa busara kushirikiana kupigania uhuru kwa kupinga udhalimu wa ukomunisti.

Ninateseka, tena nazidi kuteseka kwa ajili ya mateso yaongezekayo katika Kanisa lililo ndani ya Ngome

ya Chuma. Ninaweza kuyaona mateso haya kwa sababu nilikwisha kuyapitia.

Mwezi June, mwaka 1966, magazeti mawili ya Kirusi: *Izvestia na Derevenkais Jizn* yalishtaki Kanisa la Kibaptisti la Kirusi kwamba lilifundisha wafuasi wake kutambika watoto kama kafara ya ondoleo la dhambi. Hili ni shtaka la zamani waliloshtakiwa Wayahudi wakati wa mauaji ya watu wa dini.

Lakini mimi nafahamu maana yake. Mwaka 1959 nilikuwa katika gereza ya Cluj kule Rumania pamoja na mfungwa Lazarovici aliyekuwa ameshtakiwa kwamba aliua msichana. Bwana huyu alikuwa mwenye umri wa miaka thelathini tu, bali alionekana mzee mkongwe vile nywele zake zilivyobadilika kuwa nyeupe kwa ajili ya mateso ya siku moja tu. Makucha yake yote yaling'olewa kusudi akili kosa ambalo hakutenda. Baada ya miaka mingi ya mateso, ilitangazwa kwamba hakuwa na hatia, halafu akaachiliwa. Hata hivyo, kwake uhuru ulikuwa bure, maana alikuwa amepondeka vibaya.

Baadhi ya watu husoma habari hizi katika magazeti na kucheka vile Warusi wanavyowashtaki Wabaptisti kipumbavu hivyo. Lakini mimi naelewa wazi maana ya mashtaka haya kwa washtakiwa.

Je, yuko wapi Askofu Mkuu Yermogen wa Kaluga, kule Urusi, pamoja na Maaskofu wengine saba? Watu hawa walipinga ushirikiano na utawala wa Kikomunisti. Tendo lao hili lilikuwa kinyume cha vile walivyotenda wananchi Alexei na Askofu Mkuu Nikodim ambao hutumiwa na Wakomunisti. Kama mimi gerezani nisingeona kwa macho yangu vifo vya maaskofu waliopinga Wakomunisti katika nchi ya Rumania, kamwe nisingejishughulisha na hawa maaskofu wa Mungu.

Mimi natetemeshwa na mateso ya watu wateswao katika kambi za Kikomunisti. Pia natetemeka kila nifiki-

ripo maangamio ya milele ya watesi wao. *Vile vile natetemeka kwa sababu ya Wakristo wa Magharibi wasiosaidia ndugu zao wanaoteswa.*

Katika moyo wangu, hata mimi vile vile ningependa kustawisha shamba langu badala ya kujishughulisha na vita hii kuu. Ningependa sana kupumzika na kutulia mahali fulani. Lakini hili haliwezekani! Maana Ukomunisti waingia kwa nguvu mno! Wakati Wakomunisti waliposhambulia Tibet, walikomesha watu wale waliopendelea sana mambo ya kiroho. Lakini katika nchi yetu Rumania, walikomesha hata wale waliokuwa wamejitenga na mabo ya dunia (watawa). Makanisa na majumba ya watawa yalivunjwa, yakaachwa machache ya lazima ili kuhadaa wageni na watalii. Hivyo utulivu na kustarehe ninakotamani, lingekuwa jambo la kujiepusha na ukweli, neno ambalo lingekuwa hatari kwa roho yangu vile vile.

Ni lazima niongoze vita hii kuu ingawaje ni hatari mno kwa maisha yangu mwenyewe. Kama nitapotea, jueni wazi kuwa Wakomunisti watakuwa wameniiba. Waliniiba barabarani mwaka 1948 wakanifunga gerezani kwa jina la uwongo. Anna Pauker, Waziri Mkuu wa nchi yetu wakati ule, alimwambia Balozi wa Swideni, Sir Patrick von Reuterswaerde, "Naam, Wurmbrand sasa anazunguka barabarani mjini Copenhagen," (mji mkuu wa Denmark).

Walakini Mheshimiwa Balozi alikuwa na barua yangu mfukoni mwake; barua niliyokuwa nimefaulu kutorosha kwa siri toka gerezani. Hivyo alijua wazi kuwa alikuwa akiambiwa uwongo mtupu. Si ajabu, neno hili laweza kutukia tena!

Na kama nitauawa, mwuaji atakuwa amepangwa na Wakomunisti. Hakuna mtu mwingine aliye na nia ya kuniua isipokuwa Wakomunisti. Hata kama mtasikia kashifa mbaya kwangu, kama vile wizi, uzinifu, kuasi serikali, owongo au neno jingine lo lote lile, utakuwa ni mpango

wa kutimiza vitisho vya polisi wa siri, kusema, "Tutakuharibia jina."

Ujumbe wa kuaminika hasa ulifika kwamba Wakomunisti wa Rumania walikata shauri kuniua baada ya taarifa na ushuhuda nilioutoa katika Baraza la Senate la Amerika. Watajaribu kuniua, au kunikashifu vibaya. Watajaribu hata kutoa rushwa na kuwatisha vibaya mno rafiki zangu walio Rumania. Kweli wanazo njia nyingi za kunipata wakinuia.

*Walakini siwezi kunyamaza!* Basi, kazi yenu ni kuyapima na kuyachunguza maneno yote nisemayo. Hata pengine mwafikiri kwamba kwa kuwa nimekwisha kuyapitia yote yale, huenda ni uchungu wa mateso. Basi fikirieni uovu wa nguvu ya ukomunisti uwafanyao raia zake wapate kuchukia hivyo! Ni nguvu gani ile iwafanyayo watu wa Ujerumani ya Mashariki kupenya ngome ya vyuma na kuvusha mtoto kwa tingatinga, kwa kujitoa hata kama ni kupigwa risasi jamaa nzima?

Kweli Ulaya ya Magharibi imo usingizini, nayo yahitaji kuamshwa.

"Mfa maji hakosi kulalama." Watu wengi wanapoteseka huwalaumu wenzao na kuwasukumiza makosa. Kumpata mtu wa kulaumu hutuliza na kupunguza mzigo. Walakini, mimi siwezi kufanya vile.

Wala sitalaumu au kusukumiza makosa kwa viongozi wa nchi za Magharibi ambao wanashirikiana na Wakomunisti. Ubaya hauletwi na watu hawa. Bali ubaya huu ni wa tangu zamani. Hata viongozi hawa nao ni mateka wa dhambi hii nzee. Wao hawakubuni machafuko haya kanisani, bali wameyakuta.

Baada ya kukaa katika sehemu ya Magharibi ya dunia, nimetembelea Seminari nyingi. Niliwahi kusikiliza hotuba kadha kuhusu asili ya kengere kanisani, historia ya kawaida za ibada, sheria na kanuni za kanisa amba-

zo hata hazitumiki, hata juu ya adabu kanisani ambazo hazionekani sasa. Nilipata kuona wanafunzi wa mambo ya Mungu katika Seminari wakijifunza kwamba habari zile za Biblia kuhusu kuumbwa kwa ulimwengu, habari za Adamu, Gharika, na miujiza ya Musa, sizo za kweli hata kidogo Tena walijifunza kuwa unabii wote uliandikwa baada ya kutimizwa. Tena walijifunza kwamba kuzaa kwa Bikira Mariamu na kufufuka kwa Yesu ni uwongo mtupu. Zaidi tena walijifunza kuwa Mitume siyo kweli, na vile vile kwamba kile Kitabu cha Ufunuo kiliandikwa na mwehu, lakini kwa vingine, Biblia ni Kitabu Kitakatifu. (Mambo haya yote yakiweka Kitabu hiki Kitakatifu katika mashtaka ya kuwa na uwongo mwingi kuliko gazeti la Kikomunisti!)

Mafunzo na elimu ya jinsi hii ndiyo viongozi wa sasa wa makanisa walijifunza walipokuwa katikaSeminari! Na hiyo ndiyo dunia yao! Je, itawezekanaje wamwamini Bwana ambaye asemwa mambo mengi maovu vile! Je, yawezekanaje viongozi wa kanisa wawe waaminifu katika kanisa ambalo lafundisha wazi kwamba Mungu amekufa!

Hawa ni viongozi wa kanisa la serikali tu, wala siyo viongozi wa Kanisa la Bwana Arusi Kristo. Hawa ni viongozi wa kanisa ambalo washiriki wake wengi wamekwisha kumsaliti Bwana wao. Nao wakati wamwonapo mtu wa Kanisa la Siri, mtu ateswaye, kwao anaonekana kiumbe kigeni ajabu!

Zaidi tena, siyo haki kuwahukumu watu kwa ajili ya tendo moja ovu. Tukifanya vile tutakuwa kama Mafarisayo waliomwona Yesu kuwa mbaya kwa sababu hakufuata wala kutii sheria zao za siku ya Sabato. Neno hili liliwafumba macho wasiweze kuona neno lo lote jingine jema katika Kristo.

Hali kadhalika, viongozi wa Makanisa walio na tabia tofauti kwa Wakomunisti yawezekana kwa nia zao safi

nana Kristo. Lakini ukomunisti unapinga lengo hili vikali. Wakomunisti ni wapinga dini kwa asili yao. Wao huamini kuwa mtu akifa hubadilika kuwa chumvi chumvi na madini ya ardhini tu, na huo ndio mwisho wake, wala hakuna jambo jingine zaidi. Shabaha ya Wakomunisti ni kutaka kuona maisha yote ya binadamu yakiwa kama mdudu, mnyama, au kitu cho chote kile.

Wakomunisti wanafahamu wingi au jamii. Neno lao kuu ni kama lile la pepo mchafu katika Agano Jipya wakati Yesu alipomwuliza jina lake, alisema, "Tu wengi!" Wakomunisti huvunjilia mbali karama kuu mno ambayo Mungu alimtunukia binadamu, yaani *nafsi*. Hata mtu mmoja alipata kukamatwa kwa sababu askari walikuta nyumbani kwake kitabu kilichoandikwa na Alfred Adler, kiitwacho INDIVIDUAL PSYCHOLOGY (Elimu ya Mambo ya Roho ya Ufahamu ya Binadamu Mmoja). Askari walipiga kelele, "Lo, mmoja mmoja! Kila mara mmoja! Kwa nini isiwe wengi au jamii?"

Yesu anatutaka sisi tuwe nafsi. Kwa hiyo hapana uhusiano wo wote kati yetu na ukomunisti. Wakomunisti pia wanafahamu hili. Wakati mmoja Gazeti lao liitwalo *Nauka i Religia* (Sayansi na Dini) liliandika hivi:

"Dini ni kinyume cha Ukomunisti. Ni adui yake mkuu —. Hivyo kiini cha shabaha ya Chama cha Kikomunisti ni kupiga Dini dharuba kali na kuifisha —. Ni upingaji wa kubuni jamii ya makafiri wanaomkana Mungu kusudi kuwafungua watu kutoka katika utumwa wa dini."

Je, ni hakika kweli Ukristo unaweza kudumu na kuwa na ushirika na Ukomunisti? Wakomunisti wenyewe wanajibu swali hili vizuri sana, wanasema, "Ukomunisti ni dharuba kali la kufisha dini."

SURA YA TANO

# Kanisa La Siri, Sehemu ya 11.

Kwa sasa nitarudia mazungumzo kuhusu Kanisa la Siri. Kanisa hili latenda kazi katika hali ya dhiki kuu. Kumkana Mungu ndiyo dini ya kawaida katika nchi za Kikomunisti. Wakomunisti wanatoa uhuru kidogo kwa wazee kuamini, bali watoto na vijana *wanapingwa kabisa kuamini*. Kila njia ya mawasiliano kama redio, televisheni, senema, vitabu, magazeti na majumba ya michezo, vyote vina shabaha moja tu, nayo ni kufutilia mbali imani ya Mungu.

Kanisa la Siri halina njia yo yote ya kupinga nguvu kuu hii ya utawala huu wa nguvu. Wale mapasta wa siri kule Urusi hawana elimu yo yote ya mambo ya Mungu. Ni pasta ambao hawajapata kuisoma Biblia yote.

Sikiliza basi masimulizi haya kuhusu vile mapasta kadha walivyopata kuwekewa mikono. Siku moja nilikutana na kijana Mrusi aliyekuwa pasta wa siri. Mimi nilimwuliza mtu aliyemtia mikono kuwa pasta.

Kijana yule alijibu, "Sisi hatukuwa na Askofu wa kanuni ili kututia mikono. Yule Askofu wa serikali hawezi kumtia mikono mtu ye yote asiyekubaliwa na Chama cha Kikomunisti. Hivyo sisi vijana kumi Wakristo tulikwenda katika kaburi la Askofu mfia dini (aliyeuawa). Wawili wetu walishika jiwe la kaburi. Ndipo wale wengine wanane walisimama katika mduara kutuzunguka, na sote pamoja tulimwomba Roho Mtakatifu wa Mungu kutuwekea mikono. Nasi twaamini, na tuna hakika kuwa tuliwekewa mikono na Kristo mwenyewe, tena kwa mikono yake ile iliyotobolewa."

Kwangu mimi kuwekewa mikono kwa vijana hawa ni halali mbele za Mungu! Watu waliowekewa mikono jinsi hiyo, na bila kuwa na mafunzo yo yote ya Neno la Mungu ndio wanaoendesha huduma ya kazi ya Kristo.

Hivi ni sawa na Kanisa la karne ya kwanza. Je, ni Seminari gani walizosoma wale waliopindua dunia kwa ajili ya Kristo? Je, wote walikuwa wakielewa kusoma? Tena walipata wapi Biblia zao? Jawabu lake ni kwamba Mungu alizungumza kwao.

Sisi watu wa Kanisa la Siri hatuma kathidro, wala hata majengo ya makanisa. Je, ni kweli jengo lo lote la kathidro au kanisa lina ubora kuliko ule wa anga la mbingu tulilokuwa tukitazama wakati wa mikutano yetu mistuni? Zile sauti za ndege zilikuwa badala ya vinanda. Yale manukato ya maua yalikuwa badala ya ubani. Na mavazi yale machafu ya wafungwa mateka walioteswa yalizidi majoho ya ukasisi. Mishumaa yetu ilikuwa mwezi na nyota, ambayo iliwashwa na malaika waliotuhudumia.

*Mimi sina maneno ya kutosha kueleza ubora wa Kanisa hili.*

Kila mara baada ya ibada za siri hivyo, Wakristo hushikwa na kutupwa gerezani. Mle gerezani Wakristo huvaa minyororo kwa furaha, kama vile bibi arusi kwa furaha avaavyo lulu ya thamani apewayo na mpendwa wake, bwana arusi. Hivyo Wakristo hupata faraja kwa kuwa mikononi mwa Kristo, wala hawawezi kubadilisha furaha yao kwa kitu kinginecho. Mimi nimepata kuona Wakristo wenye furaha katika Biblia, katika Kanisa la Siri, na katika gereza.

Kweli Kanisa la Siri huteseka, lakini linao marafiki wengi miongoni mwa askari polisi wa siri, hata miongoni mwa wakuu wa serikali. Wakati mwingine hawa waamini wa siri hulilinda hili Kanisa la Siri.

Hivi karibuni magazeti ya Kirusi yalilalamika kwa ajili ya kuongezeka kwa idadi ya "waamini wa siri." Magazeti haya yalisema kwamba watu hawa ni idadi isiyohesabika ya wanaume na wanawake wafanyao kazi za madaraka katika serikali ya kikomunisti, katika Idara ya Habari na Uenezaji, na mahali pengine. Watu hawa kwa nje ni Wakomunisti, bali kwa ndani ni waamini wa siri na washiriki wa Kanisa la Siri.

Magazeti haya ya Kikomunisti yaliendelea kusimulia kisa cha kijana mwanamke aliyekuwa mtumishi katika Idara ya Kueneza Habari. Kila baada ya kazi, huyu mwanamke alirudi nyumbani kumsubiri mumewe naye atoke kazini. Ndipo wote waliwakusanya vijana toka vyumba vingine na kuwafundisha Biblia, halafu kuomba pamoja nao.

*Mambo yaya haya yanatendeka pote katika ulimwengu wa Kikomunisti.* Maelfu ya "waamini wa siri" wamejazana katika nchi za Kikomunisti. Watu hawa waona ni busara wasihudhurie ibada katika makanisa ya maonyesho yahubiriyo Injili iliyozimuliwa kwa uzushi, ambavyo tena watachunguzwa vibaya na polisi wa siri. Lakini badala yake wanashikilia kazi zao za madaraka serikalini, na kwa kimya tena kwa bidii humshuhudia Kristo kwa siri.

Kanisa la Siri lina washiriki waaminifu maelfu mengi po pote. Ndugu hawa kwa siri hukutanika katika vyumba vya ardhini au juu kabisa na katika vyumba vya kupanga.

Nchini Urusi, hutakuta mtu akibishana na mwenzake juu ya ubatizo wa watoto wachanga au watu wazima. Wala hutakuta watu wakibishana kuhusu kutoweza kukosa kwa Papa. Wala tena hutaona watu wakibishana juu ya siku ya kuabudu Mungu. Zaidi tena hawawezi kutafsiri unabii au kubishana juu yake. Walakini kila mara nashangaa vile wawezavyo kuwajibu vyema wale makafiri wakanao hakuna Mungu.

Majibu yao huwa wazi na rahisi sana. Kwa mfano:

"Kama umekaribishwa karamuni palipo na kila aina ya chakula, je utaamini kwamba hakuna mtu aliyepika na kuandaa vyakula vile? Je, utasema kuwa chakula chote cha karamu ile kimejitayarisha na kujipika chenyewe tu, au utasema nguvu ya asili ndiyo imekitayarisha?

"Kila mara twala mahindi, machungwa, ndizi, embe, nyanya, nazi, miwa, maziwa, karanga, njugu, mapapai. Je, nani kamtayarishia binadamu maakuli haya yote? Kweli maakuli haya yote hayakutayarishwa, bali yametokea vivi hivi tu, au yametayarishwa na nguvu za asili? Asili haijimudu kitu! Na kama wasema hakuna Mungu, je wawezaje kufafanua vile asili ilivyofaulu kutayarisha maakuli yetu yote?"

Vile vile waamini hawa wa siri wanaweza kuhakikisha kwamba pana uzima wa milele. Nilikwisha sikia mmoja wao akihojiana na mtu akanaye kwamba hakuna Mungu.

"Tusema ungeweza kuzungumza na mimba ya mwanamke mja mzito. Ndipo umwambie mtoto wa ndani kwamba maisha yake aliyo nayo ni mafupi, nayo hufuatwa na maisha kamili, tena marefu. Je, wafikiri yule mtoto tumboni angejibu nini?

"Bila shaka angejibu kama vile ninyi mkanao kwamba hakuna Mungu mnavyotujibu kila mara tuwaambiapo habari za mbinguni na jehanamu. Ile mimba nayo huenda ingesema kwamba maisha katika tumbo la mama ni murua, na mambo mengineyo yote ni ujinga wa kidini.

"Walakini, kama mimba ile ingefikiri kidogo, ingeanza kujihoji yenyewe. 'Naam, hapa mikono inaota! Kwa sasa siihitaji. Maana hata siwezi kuinyosha. Lakini mbona yaota? Huenda ni kwa ajili ya maisha yangu ya baadaye, nami nitaitumia kazini! Hapa tena miguu inaota! Lakini sasa naikunja kifuani tu. Lakini kwa nini

inaota! Huenda maisha katika ulimwengu mpana yafuata, nami nitahitaji kutembea! Hapa tena macho yanaota! Lakini humu tumboni nazungukwa na giza kuu, wala siyahitaji kwa sasa. Lakini kwa nini napata macho? Huenda ulimwengu ule ujao ni wa nuru na rangi mbalimbali!'

"Hivyo, kama mimba ingeweza kutafakari kidogo juu ya maendeleo yake, mtoto yule angefahamu habari za maisha ya nje ya tumbo la mama yake hata bila kuyaona.

"Nasi hali kadhalika. Wakati tuwapo wachanga bado, tuna nguvu, lakini bila busara ya kutumia nguvu ile barabara. Lakini baada ya miaka tunapokwisha kukua katika maarifa na hekima, jeneza la kutuchukua kaburini hutungoja. Je, pana lazima gani kuongezeka katika hekima na maarifa maadamu vitu hivi haviwezi kutumika tena? Kwa nini mimba tumboni huota mikono, miguu na macho? *Ni kwa ajili ya maisha ya baadaye.* Na ndivyo ilivyo hata kwetu sisi. Tuna roho, tena twakua katika maarifa na hekima kwa ajili ya maisha ya baadaye. Tunatayarishwa kuhudumu katika hali bora ifuatayo baada ya kifo."

Imani ya ukomunisti yasema kwamba Yesu hakuwapo. Walakini waamini katika Kanisa la Siri hujibu neno hili upesi mno. Hawa huwauliza Wakomunisti:

"Je, ni gazeti gani ulilo nalo mfukoni? Nalo ni *Pravada* (Baraza) ya leo au ya jana? Ebu nione tafadhali. Kumbe! Ni gazeti la Aprili 1970! Na hii miaka 1970 ilianza kuhesabiwa tangu lini? Je, mwahesabu miaka hii toka kuwapo kwa mtu msemaye hakuwapo wala hakutenda lo lote? Lakini mwahesabu miaka tangu kuzaliwa kwa mtu huyo! Hii ni ajabu kuu!

"Ni kweli kwamba majira na miaka vilikuwapo hata kabla ya kuja kwake. Lakini alipokuja binadamu waliona kwamba kila kitu kilichokuwa kabla yake kilibatilishwa, na ya kwamba muda maalumu ulianza pale pale. Hivyo gazeti lako la Kikomunisti lathibitisha na kushuhudia

wazi kwamba Yesu siye hadithi ya kubuni au uzushi. Alizaliwa hapa duniani."

Mapasta wengi katika nchi za Magharibi hudhania kwamba watu wote walio kanisani husadiki kabisa ukweli wa imani ya Kikristo. Sivyo kabisa! Ni mara haba sana kusikia mahubiri ya kuthubutisha ukweli wa imani yetu ya Kikristo. Walakini katika nchi za Kikomunisti, watu ambao hawakujifunza mambo kama hayo, huwapa waamini wao msingi imara wa imani.

Siyo rahisi kuona kikomo cha Kanisa la Serikali, wala mwanzo wa Kanisa la Siri. Makanisa haya mawili yanaingiliana. *Maana hata mapasta wa makanisa ya maonyesho huendesha vile vile huduma ya siri badala ya vile walivyoagizwa na Wakomunisti.*

Lile Kanisa la serikali, kanisa linaloshirikiana na Wakomunisti, lina historia ndefu na ya kale.

Kanisa hili lilianza mara baada ya Mapinduzi ya Kisoshalisti katika nchi ya Urusi, likiitwa "Kanisa Hai" lililoongozwa na kuhani aliyeitwa Sergius.

Kuhani Sergius alitangaza mjini Moscow, "Shabaha ya 'Kanisa Hai' siyo kujenga tena kanisa, bali kulikomesha na kufutilia mbali dini yo yote."

Kanisa kupanga mpango kama huu ni jambo la kushangaza mno! Mpaka sasa wamekwisha tokea akina Sergius wengi sana katika kila nchi.

Miongoni mwa Wakotoliki wa Hungary, palikuwa na Padri Balogh. Yeye na baadhi ya mapasta waKiprostanti walisaidia Wakomunisti kuiteka na kuitawala nchi yote.

Vile vile Wakomunisti walitawala nchi ya Rumania baada ya kusaidiwa na pasta wa Kanisa la Orthodox aliyeitwa Burducea. Pasta Burducea alibadilika kuwa Mkomunisti hata kuliko Wakomunisti wenyewe. Siku moja ya kuthibitisha utawala wa Kikomunisti nchini Ru-

mania, Burducea akitabasamu mno, alisimama kando ya Waziri Mkuu wa Kirusi, Bwana Vishinski, akatangaza, "Serikali hii itabadili dunia kuwa kama peponi, wala hamtahitaji tena dunia ya mbinguni."

Kuhusu Askofu Mkuu Nikodim wa Urusi, yeye ajulikana wazi wazi kwamba ni msaliti wa Wakristo. Hata Mkuu wa Polisi wa siri, Meja Deriabin alisema wazi kuwa Askofu Mkuu Nikodim alikuwa mfanya kazi wao.

Hali ya jinsi hii imeenea karibu kila dhehebu. Uongozi wa sasa wa Kanisa la Kibaptisti la Rumania ni wa kulazimisha kwa nguvu tu. Hata kule Urusi, uongozi wa Kibaptisti na wa kulazimisha kwa nguvu vile vile. Raisi wa kanisa moja la Rumania, Bwana Tachici aliniambia mwenyewe kwamba alikuwa mtoa habari kwa polisi wa siri wa Kikomunisti tangu siku ile waliyotawala.

Baada ya kufunga maelfu ya makanisa, na badala ya kufunga kila kanisa, Wakomunisti kwa hila walikata shauri kuyaruhusu makanisa machache yaendelee, yakiwa kifaa maalumu cha kuchunguzia, kutawala, na hatimaye kuangamiza Wakristo na Ukristo. Makanisa haya yaliruhusiwa kuendelea kama zana za Kikomunisti za kutawala Wakristo na kuhadaa wageni wanaotembelea nchi yao, kwamba pana uhuru wa dini.

Hata mimi vile vile niliwahi kupewa kanisa mojawapo la hayo, bali kwa masharti kwamba, nikiwa kama pasta, lazima nitoe taarifa na habari za Wakristo wangu kwa polisi wa siri. Baadhi ya watu wengine waliozoea "uwongo mweusi na mweupe" hawataelewa jambo hili. Lakini Kanisa la Siri halikubali yale makanisa ya maonyesho yanayotawaliwa kuwa badala ya Kanisa maalum linalotangaza Injili kwa "kila kiumbe" – hata watoto na vijana vile vile.

Ingawa ni vile, lakini pana uzima kamili wa kiroho katika makanisa yale ya serikali, licha ya wale viongozi waovu. (Nina hofu huenda hali ya namna hii yapatika-

na hata katika makanisa ya nchi za Magharibi. Wakristo mara nyingi huwa waaminifu, siyo kwa sababu ya kuwa na viongozi wema, bali hata viongozi wakiwa waovu.)

Katika Kanisa la Orthodox, kawaida ya sala haikubadilishwa, hivyo hulisha roho za washiriki wa kanisa hili, ingawaje mahubiri hujipendekeza kwa Wakomunisti. Wafuasi wa Makanisa ya Kiluteri, Presbataria na menginevo ya Kiprostanti hutumia nyimbo zile zile za zamani. Hata mahubiri ya mapasta hawa wasaliti nayo huwa na Maandiko Matakatifu vile vile. Lakini watu huweza wakaokolewa kwa nguvu ya maneno ya watu hawa wafahamikao kuwa ni wasaliti, ingawa habari za kuokoka kwao hutolewa tena kwa polisi wa siri. Waamini hawa huficha imani yao waliyopewa na mahubiri yaliyopotoka ya wasaliti hawa. Huu ni mwujiza mkuu wa Mungu ambao umeandikwa katika kitabu cha Mambo ya Walawi 11:37.

"Na kipande cho chote cha mzoga (kufuata sheria za Musa, mzoga ni chukizo) kikiwa kimeangukia mbegu za kupandwa zitakazopandwa, zitakuwa safi."

Itafaa tusema wazi na haki kwamba viongozi wote wa makanisa ya serikali sio watu wa Wakomunisti. Baadhi ya washiriki wa Kanisa la Siri ni watu wenye nguvu katika makanisa haya ya serikali, na wengi wa hawa wanapenda kujificha pasipo kujitambulisha wazi mahali walipo. Nao wanatambua wazi kuwa Ukristo siyo raha, bali ni imani ipiganayo.

Wakati Wakomunisti walipofika kufunga nyumba ya Watawa ya Vladimireshti nchini Rumania, kama vile walivyofanya Urusi, walipambana na taabu ngumu. Hata baadhi ya Wakomunisti walipoteza maisha yao kwa ajili ya uovu wa kujaribu kupinga dini.

Lakini idadi ya makanisa ya serikali yazidi kupungua mno. Sidhani katika nchi yote ya Urusi idadi yafikia hata elfu sita. (Katika U.S.A. kuna jumla ya makanisa zaidi ya 300,000, ambavyo idadi ya watu ni sawa na Urusi.)

Hata hivyo kule Urusi, makanisa haya yaliyoruhusiwa ni vyumba vidogo tu, wala siyo "kanisa" kama vile tujuavyo jengo la kanisa. Wakati wageni wafikapo mjini Moscow, huona kanisa iliyojaa watu; na wageni hawa hushangaa kuona uhuru wa kuabudu ulioko Urusi. Ndipo huandika katika magazeti, "Makanisa hujaa watu!" Kumbe, hili ndilo kanisa moja tu peke yake la Kiprostanti lililoko mjini Moscow! Na wageni hawa hawafahamu wala kuona msiba huu mkubwa wa kuwa na kanisa moja tu la Kiprostanti kwa watu milioni saba wa mji wa Moscow!

Ni jambo la kushangaza sana kwamba hata yale makanisa ya chumba kimoja kimoja yako mbali kiasi cha kutoweza kufikiwa na zaidi ya themanini kwa mia ya watu wa Urusi. Hivyo jeshi hili la watu sharti lisahauliwe, au lifikiwe kwa njia za mahubiri ya Injili yaendeshwayo na Kanisa la Siri. Hakuna njia nyingine!

Kadiri Ukomunisti unavyoendelea katika nchi, ndivyo Kanisa linavyohitajika kuwa la siri. Maana baada ya makanisa halali kufungwa, badala yake huzuka vikao na vyama vya kupinga dini.

## Jinsi Kanisa La Siri Linavyotumia Vitabu Vya Watu Wakanao Hakuna Mungu

Kanisa la Siri lafahamu jinsi ya kutumia vitabu hivi. Kwanza, lajilisha kwa kutumia vitabu vya watu wasemao hakuna Mungu, kama vile Eliya alivyolishwa na kunguru. Wakomunisti kwa wivu mkuu wanajitahidi kwa akili na busara nyingi kudhihaki na kusahihisha aya za Biblia.

Wakomunisti walichapisha vitabu viwili vilivyoitwa BIBLIA YA MZAHA, na BIBLIA YA WAAMINI NA WASIOAMINI. Katika vitabu hivi walijitahidi kuonyesha jinsi aya za Biblia zilivyo za kijinga. Na ili kufanya vile, walinakilisha aya nyingi mno kutoka katika Biblia. Sisi tulishangilia mno neno hili! Yale masahihisho na

dhihaka yao yalikuwa ya kipumbavu ajabu hata hakuna mtu aliyeyajali. Lakini vitabu hivi vilichapishwa nakala milioni nyingi zikiwa zimejaa aya nyingi mno za Biblia, ingawaje wao walizidhihaki.

Hapo kale wazushi wa dini walipokuwa wanahukumiwa na Baraza Kuu, walipelekwa kwenye matanuru ya moto katika misafara hali wamevikwa mavasi ya dhihaka kuu, yamechorwa moto wa jehanamu. Hawa walioitwa wazushi, mbona walikuwa watakatifu! Aya za Biblia hudumu kuwa za kweli daima hata kama Shetani atazinakili au kuzidondoa na kuzitumia.

Viwanda vya Kikomunisti vya kuchapa vitabu vilishangila mno kupokea barua nyingi za maombi ya kuchapa vitabu vile vya aya za Biblia pamoja na dhihaka za Wakomunisti. Wao hawakufahamu kuwa barua hizi zilitoka kwa Washiriki wa Kanisa la Siri ambao hawakuwa na njia nyingine ya kupata Maandiko. Sisi tulifahamu sana namna ya kuvitumia vitabu hivi.

Vile vile tulifahamu namna ya kutumia mikutano ya makafiri wamkanao Mungu na kusema hakuna Mungu, ili kushuhudia imani yetu.

Siku moja Profesa Mkomunisti alionyesha na kusema hadharani kwamba Yesu alikuwa mtu wa mazingaombwe tu. Yule Profesa alikuwa na gudulia la maji mbele yake. Ndipo alitia dawa nyekudnu, na maji yote yakawa mekundu.

"Mwaona! Huu ndio mwujiza wote! Yesu alikuwa amehcha dawa katika nguo zake kama hivi, ndipo akajifanya kugeuza maji kuwa divai kwa njia ya ajabu. Lakini mimi naweza kufanya zaidi yake. Naweza kugeuza divai hii iwe maji tena."

Profesa yule alisema, akitia dawa nyeupe katika maji ili kuyageuza meupe. Nayo yalikuwa meupe. Baadaye aliongeza dawa nyekundu, na maji yakageuka kuwa mekundu tena.

Pale pale Mkristo mmoja alisimama akasema, "Ndiyo, ndugu Profesa, umetustaajabisha kwa haya yote uwezayo kufanya. Lakini tungekuomba ufanye neno moja zaidi, nalo ni kunywa kidogo hiyo divai yako."

Yule Profesa alijibu, "Siwezi! Maana dawa hii ni sumu!"

Ndipo Mkristo alijibu, " Hii ndiyo tofauti kuu kati yako na Yesu. Yesu na divai yake ametupatia furaha kuu miaka hii elfu mbili, maadam wewe watupa sumu kwa divai yako!"

Kiasi cha kumalizika kwa majadiliano haya, Mkristo alijiona anatupwa gerezani. Lakini tukio hili la ushindi mkuu wa kweli tupu lilienea pote, likiimarisha imani ya waamini.

Sisi tu dhaifu kama Daudi mdogo. Walakini tuna nguvu zaidi ya Goliathi wa makafiri, maana Mungu yu upande wetu. Vile vile, kweli ni yetu.

Wakati fulani mwalimu wa Kikomunisti alikuwa akihutubia juu ya elimu ya kumkana Mungu. Wafanyakazi wote wa kiwanda kimoja walilazimishwa kuhudhuria, na miongni mwao walikuwamo Wakristo wengi. Wote walikaa kimya wakisikiliza ile hotuba ya kukufuru na kumsuta Mungu, na kwamba kumwamini Kristo ni ujinga mtupu. Yule mhutubiaji aliendelea kusema kwamba hakuna ulimwengu wa kiroho, hakuna Mungu, hakuna Kristo, hakuna uzima wa milele, na kwamba binadamu hana roho, bali ni sawa na mnyama, au mti au jiwe tu. Alisisitiza mno kwamba mtu hana roho, bali ni kama kitu tu.

Ndipo Mkristo mmoja alisimama akaomba aruhusiwe kusema neno. Naye alikubaliwa. Yule Mkristo alinyaanyua kiti chake cha kukunja akakitupa chini. Alitulia kitambo akikiangalia kile kiti. Baada ya hayo alimwendea mhutubiaji na kumwezeka kofi la uso. Yule mhutubiaji alihamaki vibaya na kujawa hasira. Uso ulimgeuka rangi na kuwa mwekundu kwa ajili ya ghadhabu!

Bwana yule alipiga kelele akiwaita Wakomunisti wenzake wamkamate huyu Mkristo. Bwana Mhutubiaji alidai kwa nguvu, "Mbona umenipiga? Ni sababu gani?"

Mkristo alijibu kwa utulivu. "Sasa hivi umejidhihirisha kuwa mwongo mkuu. Punde hivi umesema binadamu ni kitu kama jiwe, mti, au kiti. Niliponyanyua na kutupa kiti changu chini hakikukasirika kwa sababu ni kitu halisi. Mbona wewe nilipokuchapa kofi hukuwa kama kiti kile, bali umeghadhabika na kukasirika mpaka kugombana vibaya. Kitu halisi hakiwezi kukasirika. Lakini wewe ulikasirika mbona? Hivyo ndugu Profesa, umekosea mno. Binadamu siyo kitu, bali ni zaidi ya kitu. Binadamu ana roho. Sisi tunazo roho."

Kwa namna nyingi, Wakristo wa kawaida wa Kanisa la Siri waliweza kudhihirisha wazi uwongo wa Wakomunisti wamkanao Mungu.

Nilipokuwa gerezani, ofisa wa siasa alinikemea kwa ukali, "Utaendelea kushikilia ujinga wa dini yako mpaka lini?"

Mimi nilimjibu, "Nilikwisha kuona watu wengi wamkanao Mungu wanapokuwa katika saa ya kufa, hulia kwamba hawana Mungu, nao humlilia Kristo. Je, wewe waweza kukumbuka lini ulimwona Mkristo katika saa yake ya kufa akijuta kwa nini alikuwa Mkristo, ndipo akamwita Marx au Lenini kumwokoa kutoka katika imani yake?"

Yule ofisa alicheka na kusema, "Hilo ni jibu la busara sana."

Halafu niliendelea, "Kama fundi ajengaye madaraja akimaliza kujenga daraja fulani, haridhiki kuwa ni imara kwa kumwona paka akivuka mpaka ng'ambo ya pili. Bali atahitaji kuona gari zito likivuka hadi ng'ambo, ndipo atahakikisha kwamba alijenga daraja imara.

"Wakati unapomkana Mungu, hali kila jambo lako li-

nafanikiwa vyema, huko siko kuthibitisha ukweli wa ukafiri wa kumkataa Mungu. Maana wakati wa mateso pana majuto makali, na ukafiri wa kumkataa Mungu hausaidii kitu."

Wakati ule ule nilitumia kitabu cha Lenini ili kumhakikishia vile Lenin mwenyewe alivyokuwa akiomba wakati wa shida, hali akiwa Mkomunisti na Waziri Mkuu wa Urusi!

Sisi tumetulizana, na twaendelea kutulia tukingojea matukio ya mambo yanayotokea. Ni Wakomunisti tu wasiotulizana, ambao kila mara huanzisha mipango ya kupinga dini. Kwa ghasia yao hii wanathibitisha usemi wa Mtakatifu Agustini kwamba, "Moyo wenye mahanghaiko hauwezi kutulia mpaka umepumzishwa na Yesu."

## KWA NINI WAKOMUNISTI WAWEZA KUOKOLEWA

Kama Wakristo walio huru wakisaidia Kanisa la Siri, mioyo ya Wakomunisti wengi itaokolewa; hivyo dunia nzima itabadilika. Wataokolewa kwa sababu siyo kawaida mtu kuwa Mkomunisti. Hata mbwa naye apenda awe na mfupa wake pakee. Na kila Mkomunisti atamani sana kuwa na kitu kilicho mali yake mwenyewe bi-nafsi. Mioyo ya Wakomunisti wengi yapinga matendo yao wafanyayo, na ule upuzi waambiwao kuamini.

Naam, ukatili hauna mfano! Watu hawakuumbwa wawe wakatili hivyo, wala hawawezi kuendelea na ukatili kama huo. Neno hili lilionekana wakati wa kuanguka kwa enzi za Nazi. Maana baadhi ya watawala walijinyonga, na wengine walijuta na kutubu maovu yao.

Pana sababu maalum ya ulevi mwingi hivyo katika nchi za Kikomunisti. (Hata imetangazwa katika redio kwamba Urusi yataka kukomesha ulevi ambao wazuia maendeleo ya nchi). Pana shauku kali ya maisha mema na bora ambayo ukomunisti hauwezi kuwapa. Mrusi wa kawaida ni mtu mwema sana, tena mwenye moyo wa ukarimu. Ukomunisti ni wa juu tu na wenye upurukushani mwi-

ngi. Hivyo Mkomunisti huhitaji maisha safi na bora. Na kwa vile hawezi kuyapata mahali penginepo, basi huyatafuta katika ulevi. Anaonyesha katika ulevi wake matisho ya ukatili na udangayifu wa maisha atakayoishi. Kwa muda mfupi, pombe humfanya huru, kama vile Kweli imfanyavyo mtu huru akisha ifahamu.

Siku moja katika enzi za Kirusi mjini Bucharest, nililazimika kuingia katika duka la mvinyo. Mke wangu naye aliandamana nami mpaka dukani. Tulipoingia tulimwona Ofisa wa Kirusi akiwa na bunduki mikononi, akitisha kila mtu na kudai mvinyo zaidi. Mwenye duka alikuwa amekataa kumwuzia pombe zaidi baada ya kumwona amelewa mno. Watu wote waliokuwa mle dukani walikuwa wamefadhaika mno kwa hofu. Ndipo mimi nilimwendea mwenye duka, kwani tulifahamiana, nikamsihi ampe yule Ofisa pombe, nikimhakikishia kwamba nitakaa naye kumtuliza. Chupa moja moja zililetwa katika meza yetu iliyokuwa na bilauri tatu. Ofisa huyu alijaza bilauri zote tatu na kuzinywa moja baada ya nyingine. Mimi na mke wangu hatukunywa. Ingawaje Ofisa huyu alikuwa amelewa, lakini akili yake ilifanya kazi. Nilimwambia habari za Kristo, naye akasikiliza kwa makini sana.

Mwisho wa yote alisema, "Wewe umekwisha kuniambia u nani, sasa sikiliza nikueleze mimi ni nani. Mimi ni mmoja wa mapasta wa Kanisa la Orthodox niliyekuwa wa kwanza kukana imani yangu wakati mateso makuu ya Stalin yalipoingia. Nilisafiri toka kijiji mpaka kijiji nikihutubia kwamba hakuna Mungu, tena kuwa nilidanganyika nilipokuwa pasta. Niliwaambia mimi ni mdanganyifu pamoja na mapasta wenzangu. Wakomunisti walinisifu sana katika tendo hili hata wakanifanya ofisa wa polisi wa siri. Na adhabu niliyopokea kutoka kwa Mungu ni kuwaua Wakristo baada ya kuwatesa vibaya. Sasa ninakunywa mno hivi kusudi nisahau maovu yale yote niliyoyatenda! Lakini haisadii kamwe!"

Wakomunisti wengi hujiua. Hata watu wakuu kama

watunga mashairi Essenin na Maiakovsk walijiua vile vile. Ndivyo alivyojiua mwandikaji mashuhuri, Fadeev. Bwana Fadeev baada tu ya kuandika kitabu chake FURAHA, akieleza kwamba 'furaha' hupatikana kutokana na kuhudumia ukomunisti pasipo kukoma. Yeye mwenyewe alifurahia kazi yake mpaka akajipiga risasi na kufa. Maana roho yake haikuweza kuvumilia uwongo mkuu kama ule. Mabwana Joffe na Tomkin, viongozi wakuu wa Kikomunisti na wapigania ukomunisti hodari, hawakustahimili kuona vile ukomunisti usivyodhihirika kuwa kitu kamili cha kutegemea. Nao pia walijiua!

Wakomunisti ni wenye huzuni. Hawana furaha hata kidogo. Hata ndivyo walivyo watawala wao wa nguvu. Stalin mwenyewe alikuwa mwenye huzuni ajabu! Baada ya kuwaua wakuu na viongozi wenzake wazee, yeye mwenyewe alibakia katika hofu na mashaka makuu ya kupewa sumu au kupigwa risasi. Nyumba yake ilikuwa na vyumba vinane vya kulala vilivyokuwa vikifungwa kama sefu katika kanzi (bank). Usiku wo wote hapakuwa na mtu aliyefahamu Stalin alilala chumba kipi. Hakuweza kula chakula mpaka mpishi amekionja mbele yake. Kwa hiyo ukomunisti haumpi mtu awaye yote furaha, hata wale watawala wake wa nguvu, nao hawana furaha. Wanamhitaji Kristo.

Tukiushinda ukomunisti, tutakuwa tumewafungua mateka wa Wakomunisti na Wakomunisti wenyewe.

Hivyo Kanisa la Siri lawakilisha mahitaji ya ndugu zetu waliofungwa na kutekwa utumwani. Lisaidieni!

Hali dhahiri ya maendeleo ya Kanisa la Siri itategemea ari na imani yake.

Mchungaji mmoja wa kanisa aliyejibandika jina la "George", aeleza kisa kimoja katika kitabu chake kuhusu Kanisa la Siri.

Ofisa mmoja wa Jeshi la Kirusi katika Hungary ali-

mwita pasta fulani aonane naye furaghani. Ofisa yule alikuwa kijana shupavu, mwenye kupenda kujionyesha vile alivyo hodari na mshindi katika kila jambo. Wote wawili walipoingia katika chumba cha kukutania, yule ofisa kijana alishtua kichwa kuelekea msalaba mdogo ulioning'inia ukutani.

"Unafahamu, kitu kile ni uwongo mtupu?" Ofisa alisema kwa nguvu akimtazama pasta. "Tena ni kijiti cha hila tu ambacho ninyi mapasta mwatumia kupumbaza watu maskini na kuwalainisha kusudi matajiri wazidi kuwafanya wajinga.Sasa, kwa kuwa ni sisi wawili tu hapa, kana kwamba Yesu Kristo siye Mwana wa Mungu!"

Pasta alitabasamu kidogo. Ndipo alianza kusema, "Lakini, maskini, kijana mwanangu! Mimi naamini kwa moyo wangu Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu. Na hili ni kweli kabisa!"

"Sipendi unifanyie hila ya namna hiyo mimi," yule ofisa aliunguruma. "Mimi sichezi! Na wala usinichezee!"

Pale pale ofisa yule alichomoa bastola yake na kuielekeza kichwani pa pasta.

"Usipokana sasa hivi mbele yangu kwamba huo ni uwongo mtupu, nitafyatua risasi!" Ofisa aliamrisha hali macho yamemtoka pima.

"Mimi sitaweza kusema hivyo, maana siyo kweli. Hakika, Bwana wetu Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu kabisa!" Pasta alisisitiza bila hofu ya bastola ambayo ingetoboa kichwa chake kwa nukta tu.

Jibu hili lilimfanya ofisa kutupa chini bastola yake na kumwangukia pasta, mwana wa Mungu, kifuani, hali machozi yakimtiririka njia mbili.

"Ni kweli! Ni kweli!" Alilia yule ofisa mwanajeshi. "Sasa ninaamini! Lakini mwanzoni sikuelewa kwa nini watu waliweza kufa kwa ajili ya imani hii mpaka nilipoi-

gundua na kuipata mimi mwenyewe. Asante sana! Umenitia nguvu katika imani yangu. Sa mimi vile vile nawewa kufa kwa ajili ya Kristo. Umenionyesha njia!"

Pana visa vingi vya namna hiyo ninavyofahamu. Wakati Warusi walipoingia nchini Rumania, askari wawili wa Kirusi waliingia kanisani wakiwa na bunduki tayari mikononi.

"Sisi hatuamini imani yenu hii! Wale wasiotaka kuikana, sasa hivi watapigwa risasi! Wale wanaoikana, wajitenge upande wa kulia!" Askari walitoa amri kwa ukali.

Baadhi ya watu walijitenga kulia. Nao walifukuzwa nje mbio na kuamrishwa kwenda nyumbani. Walikimbia kuyasalimisha maisha yao. Baada ya hawa kwenda zao, wale askari Warusi waliwakumbatia Wakristo waliobaki kanisani, wakisema, "Ndugu! Hata sisi tu Wakristo! Lakini tulitaka tushirikiane na wale tu walio tayari kufa kwa ajili ya imanai hii!"

Watu wa jinsi hiyo wanapigania Injili ya Kristo katika nchi yetu. Wala siyo kwamba wanapigania Injili tu, bali wanapigania uhuru vile vile.

Wakristo wengi wa nchi za Magharibi hutumia saa nyingi kusikiliza muziki wa kidunia. Katika nyumba zetu watu waweza kusikia sauti kali sana za muziki vile vile, Lakini shabaha yake ni kutaka watu nje wasiweze kusikia mazungumzo ya Injili na maombi hata wakatushtaki kwa polisi wa siri. Mbona watu hawa hufurahi kupindukia kila wakutanapo na Mkristo wa juhudi sana toka nchi za Magharibi!

Mimi niandikaye habari hizi ni mtu hafifu tu. Lakini ni sauti ya wale ndugu zetu wasioweza kupaza sauti zao. Kwa niaba yao ninaomba ipatikane juhudi kuu katika imani, na namna ya kupambana na matatizo yahusuyo Ukristo. Katika jina lao naomba dua na msaada wa matendo kwa ajili ya kanisa aminifu litesekalo, yaani Kanisa la Siri lililo katika nchi za Kikomunisti.

Tutawaleta Wakomunisti kwa Yesu, kwanza, kwa sababu Mungu yuko upande wetu. Tutawaleta Wakomunisti kwa Yesu, pili, kwa sababu ujumbe wetu walingana na matakwa halisi ya mioyo yao.

Wakomunisti waliofungwa gerezani wakati wa utawala wa Nazi waliungama kwangu kuwa wakati wa shida walikuwa wakiomba. Nimekwisha kuona maofisa Wakomunisti wakitaja maneno "Yesu! Yesu!" wakati wa kufa kwao.

Tutafaulu kwa sababu jadi ya utamaduni wa watu wetu yatusaidia. Warusi wanaweza kukomesha maandiko yote ya sasa ya Kikristo! Lakini vipo vitabu vya Tolstoi na Dostoievschi, Wakomunisti wenzao, na watu huvisoma na kupata mwanga wa Kristo. Hata kule Ujerumani ya Mashariki pana vitabu vya Goethe, na nchini Poland kuna vitabu vya Szienkiewicz. Mwandikaji mkuu wa vitabu nchini Rumani alikuwa Sadoveanu, na Wakomunisti wamechapisha kitabu chake kiitwacho *Maisha ya Watakatifu* kwa jina la *Hekaya za Watakatifu*. Hata kwa jina hili, mifano ya maisha ya Watakatifu yasisimua mno.

Wala tena Wakomunisti hawawezi kutupilia mbali historia ya uchoraji na kazi za sanaa za akina Raphael, Michelangelo na Leonardo da Vinci. Picha zao zataja habari za Kristo.

Kila ninapozungumza na Mkomunisti habari za Kristo, yale mahitaji makuu ya kiroho yaliyo moyoni mwake, huwa msaada kwangu. Shida yake kuu siyo kujibu hoja zangu. Lakini shida kuu huwa namna awezavyo kunyamazisha sauti ya dhamiri yake inayonisaidia.

Nimekwisha kuona maprofesa wengi wakiomba Mungu awasaidie kabla ya kutoa hotuba ya kumkana Mungu. Ninafahamu Wakomunisti wengi wanaokwenda mbali kuhudhuria mikutano kwa siri. Lakini wakigunduliwa na kuhojiwa, hudanganya na kukana kuwa hawakwenda katika mikutano ya siri. Watu wale baadaye hujuta na kulia kwa

sababu ya kutopata ujasiri .wa kupigania imani yao ile inayowalazimisha kwenda mikutanoni.

Lakini mara mtu apatapo imani, hata ikiwa duni kiasi gani, imani hiyo hukua na kuendelea. Twajua hakika kuwa itaendelea hata kufaulu, kwa sababu sisi watu wa Kanisa la Siri mara nyingi tulikwisha kuona imani ya namna hiyo ikifaulu.

Yesu Kristo anawapenda Wakomunisti. Hivyo yawezekana, tena ni lazima waletwe kwa Kristo. Ni Kanisa la Siri tu lililo katika nchi za Kikomunisti liwezalo kumleta Mkomunisti kwa Kristo. Mkristo ye yote anayetaka kutosheleza shauku ya Kristo ya Wokovu wa kila roho ya binadamu, sharti asaidie Kanisa la Siri katika kazi zake. Yesu alisema "kufundisha mataifa yote." Hakusema kuwaacha Warusi. Uaminifu wetu kwa Mungu na Amri hii Kuu vyatulazimisha kuingia katika nchi za Kikomunisti ambazo ni theluthi ya ulimwengu wote. Twaweza tu kuwafikia kama tukifanya kazi bega kwa bega na Kanisa la Siri lililoko huko.

## MAKUNDI MATATU YALIYO KANISA LA SIRI

### Kwanza: Mapasta na Mashemasi Ambao Wakomunisti Wamefukuza Katika Kazi ya Mungu.

Yako makundi matatu yaliyo Kanisa la Siri. Kundi la kwanza ni maelfu na maelfu ya Mapsta na Mashemasi wa zamani ambao walifukuzwa katika kazi ya Mungu na Wakomunisti kwa sababu walikataa kuchanganya Injili ya Kristo na uzushi. Wengi wa Mapasta na Mashemasi hawa wamefungwa na kuteswa muda mrefu kwa ajili ya imani yao. Nao baada ya kufunguliwa wamerudia kazi yao tena, kwa siri wakihidumu katika Kanisa la Siri.

Ingawa Wakomunisti walifunga makanisa yao au kuchagua waongozi wapya, Mapasta hawa sasa wanamtumikia Mungu katika Kanisa la Siri wakifaulu zaidi kuliko vile walivyokuwa wakitumika. Hawa huongoza mikutano,

ibada, na maombi ya siri katika maghala, vyumba vya ardhini, au juu, mistuni, mashambani, au po pote pale waamini wakutanikapo kwa faragha. Watu hawa ni wafia dini walio hai ambao hawataacha kuhudumu ingawa huwagharimu mateso makali na kufungwa gerezani mara nyingi.

Pili: Kanisa Isiyo ya Kawaida.

Kundi la pili la Kanisa la Siri ni jeshi kubwa la wanaume na wanawake wasio mashemasi wala mapasta, bali Wakristo waliojitoa kwa moyo. Sharti ifahamike wazi kwamba kule Urusi na Uchina, hakuna Wakristo wa majina, wala walio nusu-nusu au wenye nia mbili. Ujira wa mtu kuwa Mkristo ni mkubwa mno, hivyo mtu awaye Mkristo, ni Mkristo kweli kweli. Jambo kubwa la kukumbuka ni kwamba mara nyingi mateso huwafanya Wakristo wawe na nguvu, wenye ushuhuda, tena wanaookoa roho za watu. Hivyo mateso ya Wakomunisti nayo yamewasha moto na kuamsha Wakristo kuwa na bidii, tena waliojitoa kabisa kuliko wale walio katika nchi huru. Ndugu hawa hawaelewi vile mtu awezavyo kuwa Mkristo halafu asipende kuokoa kila roho aionayo.

Hata gazeti moja la Jeshi la Kirusi liitwalo Nyota Nyekundu (Red Star), lilishambulia Wakristo likisema, "Wale wamwabuduo Kristo wana wivu mkuu nao hupenda kumvamia kila mtu kwa makucha yao."

Walakini maisha safi ya ndugu hawa yamewapatia upendo na heshima vijijini. Katika kila kijiji au mji, Wakristo ndio wenyeji wanaopendwa zaidi. Wakati mama mmoja auguapo hata kutoweza kutunza wanawe, mama Mkristo hujitolea kuwatunza watoto wale. Pengine mtu ashindwapo kujitafutia kuni akiwa mgonjwa au mzee sana, Wakristo hujitolea kumkatia kuni. Kweli ndugu hawa wanaishi kama Ukristo ulivyo, yaani wanaishi Kikristo halisi. Hivyo kila wanapomshuhudia Kristo, watu wote huwasikiliza na kuamini, sababu huwa wamemwona Kristo katika maisha ya ndugu hawa.

Kwa kuwa mtu mwingine asiyeruhusiwa kwa cheti hawezi kusema neno kanisani, hivyo ndugu wenye moto wa kiroho hushuhudia na kuokoa roho po pote katika nchi za Kikomunisti. Ndugu hawa wanashuhudia vijijini, masokoni, visimani, barabarani na kila mahali wanapokwenda. Hata magazeti ya Kikomunisti yanaamini wauza nyama Wakristo hutumbukiza vijitabu vya Injili katika vifurushi vya nyama wafungiavyo wanunuzi.

Yajulikana wazi kwamba Wakristo wenye madaraka katika viwanda vya kuchapa vitabu hurudi kazini usiku wa manane ili kuchapisha vijitabu vya Injili, ndipo hufunga na kuchomoka mapema kabla ya mapambazuko. Magazeti mengi ya Kikomunisti yakubali kwamba watoto mjini Moscow hupata vijitabu vya Injili toka mahali fulani, nao hunakili sehemu zake kwa mikono na kutumbukiza katika makoti ya walimu wao chumbani, shuleni.

Hivyo jeshi kubwa la wanaume na wanawake wa kawaida tu wasio na cheo cho chote kanisani lafanya kazi kuu kwa nguvu, nao hufaulu kuokoa roho katika nchi za Kikomunisti.

Hata kule Cuba ambako Wakomunisti walitesa mapasta na kuwafunga gerezani, halafu badala yao wakawekwa mapasta wengine, vile vile "Kanisa la Siri" linaendesha kazi ya kushuhudia na kuokoa roho.

Hawa mamilioni ya Waamini halisi waliojidhabihu wametakaswa kwa moto ule wa mateso ambayo Wakomunisti walidhani yatawaangamiza.

Tatu: Mapasta na Mashemasi Wasiokubali Kuzuiwa Wala Kunyamazishwa.

Kikundi cha tatu na cha mwisho cha Kanisa la Siri ni kundi kubwa la Mapasta na Wahudumu waaminifu walio katika kanisa zilizohalalishwa, lakini kanisa zilizozuiwa na kunyamazishwa. Kanisa la Siri halikutengwa kabisa kutoka katika kanisa halali. Katika nchi

nyingi za Kikomunisti kama Yugoslavia, Poland na Hungary, mapasta wengi wa makanisa yaliyoruhusiwa hufanya kazi katika Kanisa la Siri vile vile. Katika nchi nyingine, kanisa zote mbili zimeunganika. Mapasta hawa hawana ruhusa kuhubiri Kristo katika vyumba vyao viitwavyo kanisa. Wala hawaruhusiwi kuongoza mikutano ya watoto au vijana. Tena wasio Wakristo wanaogopa hawafiki. Isitoshe, hawa Mapasta hawaruhusiwi kuwatembelea Waamini wao na kuomba nao nyumbani mwao. Kila upande wamezungukwa ngome ya Ukomunisti ambayo hufanya makanisa yao yasiwe na maana yo yote.

Mara nyingi Mapasta hawa hawajali utawala ule wa Kikomunisti ambao unadhihaki "uhuru wa kuabudu," bali kwa ujasiri kujitoa kafara kwa kuhudumu kwa siri hata kuvuka vizuizi vile. Mapasta hawa huwahudumia watoto na vijana. Nao kwa siri hukutanika na kuomba katika miji ya Wakristo wao. Kwa siri hupokea na kueneza vitabu vya Injili kwa roho zenye njaa. Hutoa maisha yao pasipo kujali sheria na vizuizi vile, bali hushuhudia na kuhubiri Injili kwa watu wote, kwa kuwa kwa nje wanaonekana hawana hatia mbele ya serikali, basi hujitoa kabisa kueneza Neno la Mungu.

Wengi wa ndugu hawa waligunduliwa kule Urusi siku za karibuni, nao walishikwa na kufungwa kifungo kirefu. Hawa ndio kikundi cha tatu na muhimu, cha Kanisa la Siri.

Wahudumu wa awali waliofukuzwa na kuteswa na Wakomunisti, Mapasta walioruhusiwa ambao hufanya kazi zaidi ya ile waliyoagizwa kufanya, wote hawa ni watumishi wa Kanisa la Siri. Na Kanisa la Siri litaendelea mpaka Ukomunisti utakaposhindwa kabisa. Katika baadhi ya nchi, kikundi kimoja hufanya kazi zaidi kuliko vingine, lakini vikundi vyote vitabu vipo; vyote vikimtumikia Kristo kwa kujitoa maisha.

Mtu mmoja aliyetembelea nchi za Kikomunisti akipeleleza habari za dini, aliporudi kwao aliandika kwamba hakupata kuona Kanisa la Siri.

Hivi ni sawa na mtu akitembelea sehemu fulani ya nchi ambayo watu wake hawajui kusoma wala kuandika, ndipo mtu yule arudi kwao na kutoa taarifa akisema: "Nilipeleleza vizuri sana, hata niliwauliza kama wote wanazungumza kwa ufasaha na mtungo safi wa usemi. Walinijibu kwamba wao hawazungumzi hivyo."

Neno kama hili siyo kweli hata kidogo. Maana watu hao bila shaka wanao usemi wao wa kawaida ulio katika mtungo na ufasaha safi. Bali wao husema tu hata pasipo kufikiri au kufahamu kuwa wanatumia usemi wenye ufasaha na mtungo safi.

Hali kadhalika, wale Wakristo wa kwanza nao hawakufahamu kwamba walikuwa Wakristo. Kama mtu angewauliza habari za dini yao, bila shaka wangemjibu kwamba wao ni Wayahudi, Waisraeli, waamini wa Yesu Masihi, ndugu, watakatifu, watoto wa Mungu n.k. Jina "Wakristo" lilibuniwa na watu wengine baadaye katika mji wa Antiokia.

Wala hakuna mfuasi ye yote wa Luther aliyefahamu kwamba alikuwa Mluteri. Kwanza, Luther mwenyewe alipinga sana jina hili.

"Kanisa la Siri" ni jina ambalo limebuniwa na Wakomunisti pamoja na watu wa Magharibi wapelelezao hali ya dini katika nchi za Mashariki, hasa kuhusu umoja huu ulioanzishwa. Wala washiriki wa hili Kanisa la Siri hawauiti umoja wao huu hivyo. Wao wanajiita Wakristo, waamini, na watoto wa Mungu. Lakini kwa siri wanahudumu, wanakutanika, wanaeneza Injili katika mikutano ya siri ambayo pengine huhudhuriwa na wageni wale wakanushao kwamba hawaoni Kanisa la Siri.

Hili ni jina litoshalo kabisa ambalo latumiwa na ma-

adui, pamoja na watu wengine wa mbali watazamao kwa upendo huduma zote za umoja huu wa siri.

Mtu anaweza kutembea kote katika nchi za Magharibi bila kuona mitego ya upelelezi ya Kikomunisti. Hii haina maana kwamba Wakomunisti hawafanyi upelelezi kule! Hasha! Wao siyo wajinga kiasi cha kujionyesha wazi wazi hivyo kwa wasafiri wadadisi, wala vifaa vyao vya kupelelezea havionekani.

Katika sura ifuatayo, minedondoa maneno kutoka katika magazeti maalum ya Kikomunisti kusudi kuhakikisha ya kuwa hili Kanisa la Siri, jasiri, laendelea kukua.

SURA YA SITA

# Magazeti Ya Kikomunisti Yashuhudia

Nimekwisha kusimulia jinsi tunavyoshughulika kueneza Injili ya Kristo kwa siri katika jeshi la Kirusi, na kote nchini Romania, iliyo chini ya Wakomunisti.

Nimewasihi ili mkamhubiri Kristo miongoni mwa Wakomunisti na mateka wao, yaani watu wale wanaoteswa nao.

Je, maneno ya wito wangu yako wazi? Je, maneno haya kweli yawezekana kutendeka? Je, ni ya kweli na yakini?

Kweli kuna Kanisa la Siri nchini Urusi? Je, yawezekana kazi hiyo ya siri ifanyike kule?

Twaweza kujibu maswali haya kutokana na habari za leo zinazoandikwa magazetini. Majibu kamili yatapatikana katika magazeti ya Kikomunisti yenyewe.

Warusi walikwisha kuadhimisha na kusherehekea miaka hamsini ya utawala wa Kirusi. Walakini, ushindi wao ni ushinde! Ukristo umeshinda, na wala siyo Ukomunisti. Magazeti ya Kirusi ambayo umoja wetu huyapekua sana yamejaa habari za Kanisa la Siri. Kwa mara ya kwanza, Kanisa la Siri limethubutu kufanya kazi wazi wazi hata kiasi cha kuogofya Wakomunisti. Na habari tupatayo kutoka mahali pengi yadhihirisha ukweli wa taarifa hii katika magazeti ya Kikomunisti.

Neno kuu la kukumbuka ni kuwa Kanisa la Siri lafanana kama gogo zito lielealo majini – sehemu yake ku-

bwa ikiwa imezana majini, na sehemu ndogo tu ikitokeza kwa nje.

Hivyo kurasa hizi chache zifuatazo, nimekusanya habari maalum kutoka katika magazeti ya Kikomunisti.

### Sehemu Ya Gogo Itokezayo Juu Ya Maji

Tarehe 7, Novemba, mwaka 1966, katika sehemu ya Suhumi kule Caucasus, Kanisa la Siri lilifanya mkutano mkubwa nje wazi. Waamini wengi toka miji mingine mingi walihudhuria. Wakati wito wa kuamini ulipotolewa, vijana arobaini na saba walimwamini Kristo, ndipo walibatizwa pale pale katika Bahari Nyeusi (Black Sea), sawa na nyakati za kale kama vile Biblia isemavyo.

Hapakuwa na muda wa mafundisho ya Katekisimu kabla ya ubatizo. Baada ya miaka hamsini ya utawala wa nguvu wa Kikomunisti, bila Biblia, wala kitabu cho chote cha Kikristo, wala Seminari yo yote; hivyo mapasta na wahudumu wote wa Kanisa la Siri hawana elimu ya Theoloji.

Lakini, kama twakumbuka, hata Filipo naye hakuwa na elimu ya Theoloji, wala mitume wengine pia. Bali towashi alipomwuliza Filipo baada ya kuzungumza naye kama muda wa saa moja: "Tazama, maji ni haya, ni nini kinachonizuia nisibatizwe?"

Filipo alisema, "Ukiamini kwa moyo wako wote inawezekana." Hivyo Filipo na towashi walitelemka wote majini, towashi akabatizwa.

Ile Bahari Nyeusi (Black Sea) ina maji mengi ya kutosha ili Kanisa ya Siri iweze kuendesha kawaida ya Biblia.

*Uchitelskaia Gazete (Gazeti la Walimu)* lililotolewa tarehe 23Agosti 1966 lilieleza habari kwamba, katika mji Rostov-on-Don, Wabaptisti walikataa kuandikisha kanisa yao kufuatana na sheria. Pia walikataa kuwatii waongozi

wao waliochaguliwa na Wakomunisti. Vile vile walifanya maandamano barabarani.

Maandamano haya yalifanyika siku ya tarehe moja Mei. Kila tarehe 1 Mei huwa siku kuu ambayo Wakomunisti huandamana, nao hulazimisha kila mtu ahudhurie. Lakini siku hii kwa mara ya kwanza nchini Urusi, jeshi kubwa la Kanisa la Siri lilionekana likiandamana barabarani. Kama vile Yesu alivyokuwa akifanya miujiza yake siku ya Sabato, akiidharau, ndivyo hata Kanisa la Siri linavyochagua sherehe na siku kuu za Wakomunisti ili kudhoofisha sheria za Kikomunisti.

Waamini elfu moja na mia tano walikuwapo. Kilichowavuta ulikuwa ni upendo wa Mungu tu. Walifahamu wazi kwamba kwa kufanya vile walihatarisha uhuru wao. Pia walijua dhahiri kuwa mateso, njaa na kifungo viliwangoja gerezani.

Kila Mwamini nchini Urusi anajua "Hati ya Siri" iliyaondikwa na Wakristo wa Injili katika mji wa Barnaul. Hata ile yaeleza habari za dada Hmara wa kijijini Kulunda, ambaye alipokea habari kuwa mumewe alifia gerezani. Sasa Dada Hmara alikuwa mjane mwenye watoto wanne wachanga. Na wakati alipopokea maiti ya mumewe, aliweza kuona makovu ya pingu mikononi. Viganja, vidole na nyayo vilikuwa vimeunguzwa vibaya. Sehemu ya chini ya tumbo ilikuwa imekatwa katwa kwa kisu. Mguu wa kuume ulikuwa umevimba, na miguu yote ilikuwa na makovu ya mapigo. Mwili mzima ulijaa makovu yaliyotokana na mapigo mabaya.

Kila Mwamini aliyeandamana barabarani Rostov-on-Don alifahamu kwamba hata yeye mambo yaya haya yangeweza kumpata. Walakini, walikuja na kuandamana.

Vile vile walifahamu kwamba huyu mfia dini ambaye alitoa maisha yake kwa ajili ya Mungu, miezi mitatu baada ya kuamini kwake alizikwa hadharani, wakiwapo Wa-

kristo wengi walionyanyua makaratasi yenye maandishi kama haya:

"Kwangu Mimi Kuishi ni Kristo na Kufa ni Faida!"

"Msiwaogope Wale Wanaoua Mwili, Lakini Wasiweze kuua Roho!"

"Niliwaona Chini ya Madhabahu Wale Waliokufa Kwa Ajili ya Neno la Mungu!"

Mfano huu wa mfia dini uliwasha mioyo ya wale wote waliohudhuria mkutano wa Rostov-on-Don. Wote walikusanyika barabarani kuzunguka kijumba kidogo. Watu wengine walijazana pote, wengine juu ya mapaa ya nyumba, baadhi walipanda mitini kama Zakayo wa zamani. Watu themanini walimwamini Yesu pale pale, wengi wakiwa vijana. Katika jumla ile, watu ishirini na watatu walikuwa wa Chama cha Vijana wa Kikomunisti (Komsomols).

Wakristo walitembea barabarani mpaka mtoni Don ambako ibada ya ubatizo ilifanyika.

Ghafula, motokaa za vikosi vya polisi Wakomunisti zilifika, na askari wakazunguka kingo zote za mto! Nia yao ilikuwa kuwakamata ndugu viongozi wa ibada na mkutano. (Maana isingewezekana wakamate watu wote elfu moja na mia tano.) Mara moja Wakristo walipiga magoti kuomba, wakimwomba Mungu awalinde watu wake kusudi mkutano wa siku ile ufaulu. Ndipo ndugu Wakristo wanaume kwa wanawake walishikana mikono bega kwa bega wakijenga mduara na ngome ya kuwalinda viongozi wao wasikamatwe. Hali ilikuwa mbaya kweli!

*Uchitelskaia Gazeta* – gazeti hili lilieleza kuwa kanisa lisilo halali la Kipabtisti linao mtambo wa siri wa kuchapa vitabu katika mji wa Rostov. (Kule Urusi, neno "Baptisti" launga makanisa yote ya Ki-Evanjeli na Pentekoste). Mtambo huo wachapisha vitabu na vijitabu vya kuwafundisha vijana kusimama na kupigania imani yao. Kimojawapo cha vitabu hivi vya siri chawaeleza wazazi Wakristo jinsi ilivyo busara kuwapeleka watoto

wao kuhudhuria mazishi ya Wakristo waliouawa kusudi wasihanghaishwe na hali kama hiyo. Vile vile wazazi wanashauriwa kuwapa watoto wao Elimu ya Kikristo ili kuzuia madhara ya elimu ya uzushi wa kumkana Mungu ifundishwayo katika shule za Kikomunisti.

Gazeti hili la Walimu lazidi kuuliza: "Kwa nini walimu kwa woga wanajichanganya na jamaa ambao watoto wao wamepumbazishwa na dini?"

Gazeti lili hili lasimulia kisa kilichotukia wakati wa kusikiliza kesi ya wahubiri waliobatiza watu kwa siri.

"Waamini vijana walioitwa kortini kutoa ushahidi, walidharau korti ya Kikomunisti. Walionekana wenye hasira na wenda wazimu wa dini. Hata wasichana na wanawake vijana watazamaji waliwatazama washtakiwa kwa kuwastahi mno, hali wakikodolea macho ya kuwabeza Wakomunisti wamkanao Mungu."

Washiriki wa Kanisa la Siri wamejitoa maisha yao kupigwa na kufungwa gerezani kwa kudai uhuru zaidi mbele ya Makao Makuu ya Chama cha Kikomunisti nchini Urusi.

Tunayo hati au maandiko ya siri ya Kamati isiyo halali ya makanisa ya Ki-Evanjeli na Kibaptisti nchini Urusi. Hati hii yapinga "Umoja wa Kibaptisti", yaani makanisa yanayotawaliwa na Wakomunisti, yakiongozwa na mjasusi Karev, ambaye alisifu utu mwema wa Wakomunisti kwa sababu ya mauaji makuu ya Wakristo, akitukuza uhuru ulioko kule. (Maisha Urusi Leo - Soviet Life Today, No. 6, 1963). Hati hii nayo imesafirishwa kwa siri hadi nchi za Magharibi.

Ndani ya hati hii pana maelezo ya maandamano ya kishujaa yaliyofanyika mjini Moscow penyewe. Ifuatayo chini ni sehemu ya tafsiri ya hati hii:

"Habari ya Haraka!"

"Wapendwa Ndugu na Dada, Baraka iwe kwenu na

neema itokayo kwa Mungu, Baba na Yesu Kristo, Bwana wetu.

"Twaharakisha kuwafahamisha kwamba ule ujumbe wa Makansia ya Kikristo ya Ki-Evanjeli na Kibaptisti, watu wapatao mia tano waliosafiri mpaka mjini Moscow tarehe 19 Mei, mwaka 1966, umepenya mpaka penye kiini cha nguvu ya Kikomunisti. Watu wote wamefika jumba la Kamati Kuu ya Chama cha Kikomunisti cha Jamhuri ya Urusi ya Kisiosholisti, wakipeleka maombi yao yasikilizwe.

"Karatasi yetu ya maombi tulimpa Katibu Mkuu, Brezhnev."

Hati ile ile ilizidi kueleza kwamba watu hawa mia tano walisimama kutwa nzima mbele ya jumba hili kuu. Haya yalikuwa maandamano ya kwanza mjini Moscow kupinga Ukomunisti wazi wazi. Maandamano haya yalitayarishwa na wajumbe wa Kanisa la Siri.

Kulipokuwa jioni, karatasi nyingine ya maombi ilipelekwa kwa Brezhnev ikitoa malalamiko kwamba komredi mmoja, Strozanov, alikataa kuwakilisha maombi yao ya kwanza kwa Katibu Mkuu, Brezhnev, na tena kwamba aliwatisha vibaya.

Ujumbe ule wa watu mia tano ulikaa barabarani usiku kucha. Watu wengi wakiwa katika motakaa walifika pale kuwatupia matope na takataka, wakiwatukana. Ingawa mvua ilinyesha, na walitendewa yote haya, lakini walikaa mbele ya jumba la Chama cha Kikomunisti usiku kucha.

Keshoye, ujumbe ule ulishauriwa kuingia ndani ili kuonana na maofisa wa vyeo vya chini wa Kikomunisti. Wote kwa umoja walikataa shauri hili kwa kujua kwamba "Wakristo wo wote waingiao ofisi za maofisa Wakomunisti, hupigwa vibaya maana hapana shahidi mwingine.

Hivyo ujumbe huu ulidai uitwe na Brezhnev, Katibu Mkuu, mwenyewe."

Ndipo kitendo kisichoepukwa kilitukia! Alasiri, saa nane kasa robo, magari ya abiria ishirini na manane yalifika. Pale pale mapigo ya kakatili kwa Waamini yalianza.

"Mara sisi sote tulifanya mduara mkubwa tukiwa tumeshikana mikono, na kuimba wimbo:

*Siku Njema Maishani Mwetu ni Siku Ambazo Tunaweza Kuchukua Msalaba.*

Papo hapo askari polisi wa siri walianza kutupiga sote wakubwa kwa wadogo." Waliwashika mmoja mmoja na kuanza kuwapiga usoni, vichwani na kuwabwaga barabarani penye lami ngumu. Baadhi waliburutwa kwa nywele za vichwa vyao hadi kutupwa katika magari. Baadhi ya wengine waliotoka walipigwa mpaka kuzirai. Baada ya kujaza magari yote, Wakristo wale walipelekwa mahali pasipojulikana. Walakini nyimbo za Injili walizoimba hawa ndugu Wakristo zilisikilika zikitoka katika magari ya polisi wa siri. Mambo haya yote yalitendeka wazi machoni pa makundi makubwa ya watu!

Na sasa tukio malidadi kabisa linafuata, Baada ya ya wale ndugu mia tano kukamatwa na kuteswa isivyo kanuni, Ndugu G. Bins, pamoja na Ndugu Horev, Wachungaji kamili wa kundi la Kristo, walikuwa bado na ujasiri mkuu kwenda katika jumba la Makao Makuu ya Kamati Kuu ya Kikomunisti. Ndugu hawa walifanya kama vile Yesu alivyoanza kuhubiri baada ya kukamatwa kwa Yohana Mbatizaji, akisema, "Tubuni, maana ufalme wa Mbinguni umekaribia."

Ndugu Bins na Horev walifika kuuliza habari za Ujumbe ule wa watu mia tano, na kuomba wafunguliwe. Hata ndugu hawa nao walitoweka, yaani walifungwa gerezani!

Ndipo baadaye habari zilienea kuwa walikuwa katika gereza la Lefortovskaia.

Je, Wakristo hawa wa Kanisa la Siri walikuwa woga? Hasha! Mara moja ndugu wengine walijitoa maisha yao na kutupilia mbali uhuru wao kwa kutoa hati nyingine. Ndugu hawa walisimulia visa vyote vilivyotukia, wakikaza, *"maana mmepewa kwa ajili ya Kristo, siyo kumwamini tu, ila na kuteswa kwa ajili yake."* Waefeso 1:29. Waliwajuburu ndugu, "mtu asifadhaishwe na dhiki hizi, maana ninyi wenyewe mnajua kuwa twawekewa kizo." Wathesaloniki 3:3. Vile vile walitumia maneno ya Waebrania 12:2, wakiwaita Wakristo, "....tukimtazama Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu; ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu..."

Kanisa la Siri limekwisha pinga wazi mjini Rostov, Moscow na kote nchini Urusi. Kanisa la Siri limepinga wazi uzushi wa kumkana Mungu, ambayo ni sumu mbaya kwa watoto na vijana. Ndugu hawa wanapigana kupinga sumu ya Kikomunisti pamoja na viongozi wapotovu wa makanisa halali, ambayo gazeti la Kirusi liitwalo "Pravda Ukrain" la tarehe 4 Oktoba 1966 lilieleza:

"Katika siku zetu, Shetani anatawala kwa nguvu, na 'kanisa' linakubali mashauri yote yaliyo kinyume cha amri za Mungu."

Gazeti *Pravda Vostoka* lilieleza kesi ya Ndugu Alexei Neverov, Boris Garmashov, na Axen Zubov ambao walikusanya vikundi vya watu kusikiliza vipindi vya mahubiri ya Injili kwa redio kutoka America. Walichukua mahubiri kwa mashine za kunasia sauti, halafu wakayaeneza pote.

Ndugu hawa vile vile walishtakiwa kwa makosa ya kuendesha mikutano ya Injili kwa siri, wakijibandika majina kama "watembezi" au "stadi" wa kujadili neno fulani. Hivyo ndivyo Kanisa la Siri lifanyavyo kazi,

yaani ni sawa na lile Kanisa la Mwanzo lilivyofanya kazi mapangoni na mashimoni kule Rumi.

Gazeti *Sovietscaia Moldavia* la tarehe 15 Septemba 1966, vile vile lalalamika kwamba, Kanisa la Siri hunakilisha vijitabu kwa mashine. Halafu hukutanika pamoja katika majumba ya mikutano, ambavyo ni kinyume cha sheria, tena huzunguka huko na huko wakimshuhudia Kristo.

Gazeti lili hili lasimulia kisa kimoja kilichotukia katika gari moshi toka Reni kwenda Chisinau. Wavulana watatu na wasichana wanne waliimba nyimbo za Kikristo mle garini, kusema, "Tuutoe ujana wetu wakf kwa ajili ya Kristo."

Mwandishi wa habari hii alisema vile alivyochukizwa mno kuona Wakristo hawa wakihubiri po pote, "mabarabarani, magarini, penye vituo vya wasafiri, hata katika vyuo vya taifa." Hali kadhalika, hili ni Kanisa la Siri likitenda kazi nchini Urusi leo hii.

Katika korti fulani ilikuwa ikisikilizwa kesi ya Wakristo walioimba nyimbo za Injili hadharani. Baada ya hukumu kutolewa, wale waliohukumiwa walipiga magoti wakasema, "Mungu, tunatoa maisha yetu na kuyaweka mikononi mwako. Tunakushukuru Bwana, kwa kuturuhusu kuteseka kwa ajili ya imani hii."

Mle mle kortini, umati wa watu ukiongozwa na Madan, "mwenda wazimu wa dini," uliimba wimbo ule ule ambao ndugu zao waliimba wakashtakiwa na kuhukumiwa kifungo.

Tarehe mosi, mwezi Mei, Mwaka 1966, Wakristo wa vijiji viwili, Copceag na Zaharovka, walifanya mkutano msituni, kwa sababu hawakuwa na kanisa.

Zaidi tena walikutanika mara nyingi wakijifanya kwamba walisherehekea siku kuu ya kuzaliwa kwa mmoja wao. (Jamaa nyingi za Wakristo zenye watu wanne, au watano, ziliweza kuwa na siku kuu zaidi ya

thelathini kwa mwaka, zikiwa kama kinga ya mikutano ya siri.)

Magereza, au mateso haviwezi kuwatisha Wakristo wa Kanisa la Siri. Ni sawa na vile Kanisa la Kwanza lilivyojengwa na kuimarishwa na mateso.

Gazeti *Pravda Ukrain* la tarehe 4 Oktoba, mwaka 1966, lilimtaja Ndugu Prokofiev, mmojawapo wa viongozi wa Kanisa la Siri nchini Urusi, kuwa alikwisha kufungwa gerezani mara tatu. Lakini kila akifunguliwa huanza tena kufundisha Mafunzo ya Jumapili kwa siri. Sasa amekamatwa tena.

Ndugu Prokofiev aliandika hati ya siri kusema, "Kanisa linapotii sheria za kibanadamu, (yaani sheria za kikomunisti), linapoteza baraka zake zote kutoka kwa Mungu."

Wakati usikiapo kwamba ndugu fulani amehukumiwa kufungwa gerezani nchini Urusi, usifikirie hali ya magereza ya nchi za Magharibi. Kule Urusi na katika nchi za Kikomunisti, gereza maana yake ni *kufa, njaa, mateso, na kuoshwa akili!*

Gazeti liitwalo *Nauka i Religia* (Sayansi na Dini) Namba 9, la mwaka 1966, lilisema kwamba Wakristo huchomeka vijitabu vya Injili katika magazeti na vitabu vingine vya Kikomunisti. Jalada laweza kuwa la kitabu cha Kikomunisti, kumbe ndani pamewekwa vijitabu vya Injili na Biblia.

Vile vile gazeti liitwalo *Kazakstankaia Pravda* la tarehe 30 June, 1966, lilisema kuwa Wakristo huimba nyimbo ambazo sauti yake ni ya "Nyimbo za Taifa za Kikomunisti," lakini maneno yakimtukuza Kristo.

Barua moja ya siri iliyoandikwa mjini Kulanda kule Siberia, Wakristo walisema kuwa kanisa halali la Kibaptisti "limeharibu kanisa na watumishi wa kweli ulimwenguni; sawa na vile Makuhani, Waandishi na Mafariyaso walivyomsalitiYesu Kristo mbele ya Pilato."

Lakini, Kanisa la Siri, aminifu, linaendelea kufanya kazi.

Kanisa hili ambalo ni bibi arusi wa Kristo, laendelea kumhudumia! Hata Wakomunisti wenyewe wanaamini kuwa nasema kweli kwamba Kanisa la Siri lawaleta kwa Kristo. Maana kweli inawezekana kuwaokoa Wakomunisti!

Gezeti liitwalo *Bakinskii Robocii* (Kazi za Baku) la tarehe 27 Aprili, mwaka 1966, lilichapisha tena barua ya msichana kijana, Tania Ciugunova, mwanachama wa Chama cha Vijana Wakomunisti, ambaye alimwamini Kristo. Barua ile ilikamatwa na Watawala Wakomunisti, nayo ilisema hivi:

*"Mpendwa Shangazi Nadia,*

*"Ninakutumia baraka toka kwa Bwana wetu mpendwa. Shangazi Nadia, mbona Bwana ananipenda mimi sana! Sisi binadamu si kitu mbele zake. Shangazi Nadia, naamini kwamba unafahamu maana ya maneno haya: "Wapendeni adui zenu, wabarikini wanaowalaani, watendeeni mema wale wanaowachukia, na waombeeni wale wanaowadharau...!*

Mara tu baada ya barua hii kukamatwa, kakaye mvulana, Peter Serebrennikov, ambaye ndiye alimhubiri Tania Injili mpaka akaamini, alitupwa gerezani pamoja na vijana wengine Wakomunisti. Gazeti moja la Kikomunisti liliandika baadhi ya mahubiri ya Peter kusema:

"Lazima tumwamini Mwokozi wetu kama vile walivyofanya Wakristo wa kwanza. Sisi kanuni yetu kuu ni Biblia; wala hatutambui kanuni nyingine yo yote. Ni sharti tuharakishe mno kuokoa watu toka dhambini, hasa vijana."

Na wakati Peter alipoambiwa kwamba, sheria za Kikomunisti zakataza mtu asimwambie kijana ye yote habari za Kristo, yeye alijibu, "Sisi tunayo sheria moja tu, nayo ni Biblia." Hili ndilo jibu pekee la kawaida

katika sehemu yo yote ile iliyo chini ya utawala wa nguvu wa watu wanaomkana Mungu.

Gazeti hili hili laonyesha picha ya ajabu kwa kusema, "Vijana wavulana kwa wasichana huimba nyimbo za kiroho. Tena hupokea ubatizo na kukaza mafundisho maovu yenye udanganyifu wa kuwapenda adui!"

Gazeti hili laendelea kueleza kuwa wavulana na wasichana wengi walio wanachama wa Chama cha Vijana Wakomunisti ni Wakristo halisi! Habari ile ile yaendelea, na mwishoni inatoa masuto makali: "Mbona shule za Kikomunisti hazina nguvu! Mbona zachusha, wala hazitoi nuru ... hata mapasta wanaweza kunyakuwa wanafunzi toka puani mwa waelimishaji wao wazembe!"

Gazeti liitwalo *Kazakstankaia Pravda* la tarehe 30 June, mwaka 1966 liligutushwa ajabu ilipogundulika kwamba mwanafunzi wa kwanza darasani, tena mwenye tuzo za juu kuliko wote alikuwa Mkristo mvulana.

Halafu gazeti *Kirgizskaia Pravda* la tarehe 17 Januari 1966 lilidondoa maandiko ya siri ya akina Mama yasemayo:

"Ebu na tuunganike kwa nguvu kuomba na kuweka wakf kwa Mungu maisha ya watoto wetu tangu wakati wanapokuwa wakibebwa katika susu. Tujitahidi kadiri tuwezavyo ili kuwaokoa watoto kutokana na vishawishi vya dunia!"

Ni kweli nguvu hizi zimefaulu sana. Maana hata magazeti ya Kikomunisti yanashuhudia! Ukristo umeendelea mbele katika vijana.

Katika gazeti moja kutoka mjini Celiabinsk, Urusi, ilielezwa vile Nina, msichana, tena mwanachama wa Chama cha Vijana Wakomunisti alivyopata kuwa Mkristo. Nina alipata kuwa Mkristo kwa kuhudhuria mkutano wa siri.

Gazeti *Sovietskaia Justitia.* Namba 9 la mwaka 1966, lasimulia hivi kuhusu Mkutano wa Siri wa namna hiyo hiyo!

"Mkutano hufanywa usiku wa manane. Huwa wamejificha, tena wenye woga hata kutishwa na vivuli vyao wenyewe. Wanaume walitoka sehemu mbali mbali. Ndugu walijaza chumba cha giza ambacho dari yake ilikuwa chini zaidi. Walikuwa wengi mno chumbani hata nafasi ya kupiga magoti haikupatikana. Kwa ajili ya kukosa hewa, hata koroboi yao ilizimika. Wengi wao walianza kutiririka jasho. Na mtu mmoja, mmojawapo wa watumishi wa Bwana alikaa barabarani kuangalia askari polisi."

Lakini Nina alisema kwamba alipokelewa vi suri kwa kukumbatiwa na kutunzwa vyema. "Walikuwa na mwanga wa imani kuu katika Mungu, kama mwanga huu nilio nao mimi sasa hivi. Mungu anatutunza salama ajabu! Waacheni wale vijana Wakomunisti wanaonifahamu wanipitie kimya tu hata bila kunisalimu! Wacha wanianga-lie kwa dharau wakiniita 'Mbaptisti' kama wanipigao. Wacha wafanye vile wapendavyo! Wala hata mimi siwataki tena!"

Hivyo, vijana wengi Wakomunisti hujitoa kumtumikia Kristo mpaka mwisho, kama vile Nina alivyojitoa.

Majibu wayatoayo Wakristo wa Kanisa la Siri kila wanapoletwa katika Korti za Wakomunisti, huwa ya kiroho na matakatifu. Hakimu mmoja kortini alimhoji Mkristo msichana, "Kwa nini mwavuta watu kuingia dhehebu lenu lililopigwa marufuku?

Yule dada alijibu, "Shabaha yetu ni kuuleta *ulimwengu wote* kwa Kristo."

"Mbona dini yenu yapingana na sayansi!" Jaji mmoja alishutumu vikali kortini wakati wa kusikiliza kesi ya msichana mmoja aliyekuwa mwanafunzi.

Yule msichana mshtakiwa alijibu kwa utulivu, na kwa busara alifafanua majibu yake!

"Je, Mheshimiwa Jaji! Wewe unafahamu sayansi vyema kuliko Wataalamu Einstein na Newton? Wao walikuwa Wakristo. Jina la Einstein lajulikana kote ulimwenguni. Nimejifunza habari za Einstein katika madarasa ya juu. Na Mtaalam huyu Einstein aliandika: 'Kama tukisafisha unabii wa dini ya Kiyahudi na Ukristo kwa njia ya mafundisho ya Yesu, kwa kutenga mbali shughuli za kikuhani, tutaweza kupata dini ambayo yaweza kuokoa ulimwengu wote kutoka katika maovu. Wajibu mtakatifu wa kila mtu ni kujitahidi awezavyo ili dini hii ipate kushinda.'

"Mheshimiwa Jaji! Kumbuka habari za Mtaalamu wetu mkuu Pavlov! Je, vitabu vyetu havisemi kwamba alikuwa Mkristo?

"Hata Karl Marx naye aliandika katika Utangulizi wa kitabu chake *Das Kapital* kwamba: 'Ukristo wa Kiprostanti ndiyo dini ya kweli iwezayo kutengeneza upya tabia za watu zilizoharibiwa na dhambi.'

"Mimi mwenyewe nilikuwa na tabia iliyoharibiwa na dhambi. Lakini Marx amenifundisha kuwa Mkristo, kusudi nitengeneze upya tabia yangu iliyoharibika. Yawezekanaje basi, ninyi wafuasi wa Marx mnihukumu kwa tendo hili?"

Ni rahisi kutokana na majibu hayo kutambua kwa nini Jaji yule alinyamaza kimya pasipo kumjibu yule msichana mdogo.

Katika mashtaka mengine ya jinsi hiyo kwamba Ukristo wapingana na sayansi, kijana Mkristo alijibu vizuri sana kortini.'

"Mheshimiwa Jaji! Nina hakika kwamba wewe si mtaalamu mkuu kama Mtaalamu wa sayansi aitwaye Simpson, aliyegundua dawa ya kutia mtu usingizi (chloroform), pamoja na dawa nyinginezo. Lakini alipoulizwa ni kitu gani kikuu mno kuliko vyote alivyokwisha kugundua, alijibu, 'Siyo dawa ya kutia usingizi, (chlo-

roform)! Ugunduzi wangu mkuu mno ni kutambua kwamba mimi ni mwenye dhambi ambaye naweza kuokolewa na neema ya Mungu!"

Maisha, kujitoa kafara, na damu ile waimwagayo Wakristo kwa ajili ya imani yao, ni hoja kamili za kutetea Ukristo zilizomo katika Kanisa la Siri. Hayo yote yaunda "ushirika mtakatifu wa watu wale walio na alama za mateso," kama vile alivyosema Albert Schwetzer, mmissionari katika nchi ya Afrika. Ushirika wa namna hiyo alikuwa nao Yesu, mtu wa mateso mengi. Hata Kanisa la Siri nalo lashirikishwa na kifungo cha upendo wa Mwokozi wake. Kifungo kile cha upendo chawaunga pamoja washiriki wote wa Kanisa la Siri, wala hapana mtu duniani awezaye kuwashinda.

Barua moja iliyosafirishwa kwa njia ya siri kutoka katika Kanisa la Siri ilisema:

*"Hatuombi Mungu kusudi tuwe Wakristo bora zaidi, bali twaomba tuwe namna ile ya Wakristo ambao Mungu anataka tuwe, yaani Wakristo tufananao na Kristo. Maana yake ni kuwa, tuwe Wakristo tulio tayari kuchukua Msalaba kwa ajili ya utukufu wa Mungu."*

Kwa kuwa na "busara kama nyoka", kama vile mafundisho ya Yesu yasemavyo, Wakristo wakamatwapo hawasemi viongozi wao, hata wakifikishwa kortini, hawawasemi.

Gezeti *Pravda Vostoka* (Ukweli wa Mashariki) la tarehe 15 Januari, 1966 laeleza vile mshtakiwa, Maria Sevciuk alivyojibu kortini wakati alipoulizwa mtu aliyemhubiri habari za Kristo: "Mungu ndiye aliyenivuta kuingia kundini mwake."

Mtu mwingine alipomwuliza, "Ni nani kiongozi wenu?" Maria alijibu, "Hatuna kiongozi mwanadamu."

Watoto Wakristo walipoulizwa, "Ni nani aliyewa-

fundisha kushiriki Ukristo na kuvua tai nyekundu za Kikomunisti?"

Mara wao walijbu, "Tulifanya sisi wenyewe kwa hiari yetu. Hatukufundishwa na mtu ye yote."

Ingawaje mahali pengine matendo ya Kanisa la Siri yanatokeza wazi wazi, lakini katika sehemu zingine Wakristo hujibatiza wenyewe kusudi viongozi wao wasikamatwe. Katika sehemu hizo, ubatizo hufanyika mtoni, na wote wale wanaojibatiza huvaa vinyago usoni kusudi wasipigwe picha za nyuso zao.

Gazeti *Uchitelskaia Gazeta* la tarehe 30, Januari, 1964 lasimulia kisa cha mhutubiaji mmoja juu ya hotuba ya uzushi wa kumkana Mungu katika kijiji cha Voronin, wilaya ya Volnecino-Korskii, kule Urusi. Baada ya hotuba ile, gazeti lasema, "Wakristo walimsaili hadharani kuhusu mafundisho yake, naye hakuweza kuwajibu."

Wakristo wale walimwuliza, "Ninyi Wakomunisti mwapata wapi msingi wa mafunzo ya maadili mnayotangaza, maadam hamtii amri, 'usiibe', wala 'usiue?" Wale Wakristo walimthibitishia yule mhutubiaji kwamba mambo hayo yanatoka katika Biblia ambayo Wakomunisti hupinga. Hotuba yote ile ilivurugika baada ya mhutubiaji kuchanganyikiwa mambo. Hivyo Wakristo walipata Ushindi mkuu.

## Mateso Ya Kanisa La Siri Yazidi Kuongezeka

Sasa Wakristo wa Kanisa la Siri wanateseka zaidi kuliko walivyopata kuteseka hapo mwanzo. Dini zote zinateswa vibaya nchini Urusi. Ni jambo linalovunja mioyo ya Wakristo kusikia vile Wayahudi wanavyoteswa katika nchi za Kikomunisti. Lakini shabaha kuu ya mateso hayo ni Kanisa la Siri. Magazeti ya Kikomunisti hutoa tarifa ya ukamataji mkuu wa Wakristo, pamoja na mashtaka mengi mengi.

Katika sehemu moja, Wakristo themanini na wawili

walifungwa katika gereza ya wenda wazimu. Baada ya siku chache, kiasi cha watu ishirini na wanne walikufa kutokana na maombi marefu mno! Je, tangu lini maombi marefu yakaua mtu? Unaweza kufikiria na kukisia mateso yao?

Teso kuu mno watendewalo kwa lazima ni kunyang'anywa watoto wao, na kuwanyima ruhusa kuwatembelea maisha yao yote. Hili hutokea baada ya kugundulika kwamba wazazi wamewafundisha watoto wao habari za Kristo.

Urusi ilitia sahihi hati ya azimio la Umoja wa Mataifa, "lipingalo ubaguzi katika elimu," hati ambayo yaweka masharti: "Wazazi sharti wahakikishe kuwa watoto wao wanapata mafundisho ya dini wanayopenda wenyewe."

Msaliti Karev, kiongozi wa kanisa halali la Kibaptisti nchini Urusi alitangaza kuwa uhuru kama huo kwa wazazi wapatikana tele kule Urusi, na wadanganyifu humwamini! Sasa sikiliza vile magazeti ya Kirusi yasemavyo.

Gazeti *Sowjetskais Russia* la tarehe 4 June 1963, lasimulia kisa cha Mbaptisti, Makrinkowa, mwenye watoto sita alivyonyang'anywa watoto wake kwa sababu aliwafundisha imani ya Kikristo, na kuwakataza kuvaa ile tai nyekundu ya Kikomunisti.

Wakati hukumu ilipopitishwa, Mama huyu alisema, "Nateseka kwa ajili ya imani." Bibi huyu alilazimishwa kulipa gharama zote za kutunza wale watoto wake alionyang'anywa. Kwa sasa wanalishwa sumu ya uzushi wa kumkana Mungu. Enyi Mama mlio Wakristo, fikirini mateso na maombolezo ya huyu Mama mwenzenu!

Gazeti *Ucitelskaia Gazeta* lasimulia mambo yaliyowapata Ignatii Mullin na mkewe. Jaji aliwalazimisha waikane imani yao, akisema, "Chagueni kati ya Mungu na binti yenu. Je, mwachagua Mungu?"

Mzee Ignatii, baba mzazi wa msichana yule yule alijibu, "Mimi sitakana imani yangu."

Paulo Mtume alisema, "Mambo yote hutenda kazi pamoja kwa wema—." Mimi kwa macho yangu nimekwisha kuona watoto waliolelewa wakiwa Wakristo halafu wakatengwa na wazazi na kuingizwa katika shule za Kikomunisti. Badala ya kulogwa na sumu ya kikomunisti, ile imani ya watoto hawa waliyofunzwa na wazazi wao Wakristo huambukiza watoto wengine na kuenea shule nzima.

Biblia yasema kwamba ye yote apendaye watoto wake kuliko Yesu, hamfai. Maneno haya yana maana kuu katika nchi za Kikomunisti.

Je, umekwisha kujaribu kutengwa na watoto wako hata pasipo ruhusa kuwatembelea, kiasi cha mwezi mmoja tu? Kama ndivyo, basi wafahamu mateso ya ndugu zetu nchini Urusi.

Haitakuwa haki kueleza habari za Kanisa la Siri la Kiprostanti peke yake pasipo kutaja hata madhehebu mengine vile vile.

Kanisa la Kale (Orthodox) nchini Urusi limebadilika kabisa kutokana na kawaida yake ya kanuni zake. Mamilioni ya Wakristo wake wametupwa gerezani nao. Mle gerezani hawakuwa na tasbihi, wala misalaba, wala sanamu za Watakatifu, wala uvumba na mishumaa. Wakristo walitupwa gerezani pasipo kuhani au padri. Makuhani na mapadri walitupwa gerezani pasipo majoho, mikate, divai, au mafuta matakatifu, wala vitabu vya sala. Nao waligundua kwamba waliweza kufika mbele za Mungu moja kwa moja katika maombi bila kuhitaji vitu hivyo. Walianza kumwomba Mungu, na Mungu aliwamwagia Roho Mtakatifu. Huu ulikuwa uamsho halisi wa kiroho katika Kanisa hili la Kale la Orthodoksi.

Hivyo ni wazi kuwa katika Urusi na nchi nyingine za Kikomunisti pana Kanisa la Siri la Kiorthodoksi,

ambalo ni sawa na kanisa la Injili, tena liko karibu kabisa na Mungu. Lililobakia katika Kanisa hili, ni mazoea tu ya kanuni na kawaida za Kiorthodoksi. Maana Kanisa hili nalo limetoa Wakristo wafia-dini wengi. Nani ajuaye mahali alipo Askofu Mkuu Yermogen wa Kaluga? Yeye alieleza wazi uovu wa kushirikianisha Kanisa na Serikali ya Kikomunisti imkanayo Mungu.

Katika muda wa miaka hamsini ya utawala wa Kikomunisti, magazeti ya Urusi yamejazana na habari za ushindi wa Kanisa la Siri. Kweli kanisa hili lapita katika dhiki kuu, lakini lakua na kudumu katika uaminifu na kweli.

Sisi Wakristo wa Rumania tulipanda mbegu kwa sababu ya kazi yetu ya siri katika jeshi la Kirusi. Ndivyo na Wakristo wengine walivyofanya Urusi na katika nchi nyingine za Kikomunisti. Mbegu zile zimeota na kuzaa matunda.

Ni wazi ulimwengu wa Kikomunisti waweza kumwamini Kristo. Wakomunisti wanaweza kuwa Wakristo. Hata wale mateka wao wanaweza kuwa Wakristo, kama tutaweza kuwasaidia.

Kuendelea kwa Kanisa la Siri nchini Urusi na China, na katika sehemu nyingine za Kikomunisti, ni ushahidi kwamba haya niyasemayo ni haki tupu.

Kwa kutaka kudhihirisha shangwe waliyo nayo ndugu zetu Wakristo watesekao, hapa chini zafuata barua kutoka Urusi. Barua mbili za mwisho zatoka katika gereza la Urusi.

**Jinsi Varia, Msichana Mkomunisti Alivyomwamini Yesu Na Kutoa Ushuhuda Mpaka Akawa Mfungwa Mtumwa.**

Barua tatu za kwanza zatoka kwa Maria, msichana Mkristo aliyemshuhudia Varia mpaka naye akamwamini Yesu.

*Barua ya Kwanza:*

*"—Bado ninaendelea kuishi hapa. Ninapendwa*

*sana. Napendwa hata na mwanachama wa Chama cha Vijana Wakomunisti (Komsomol) niliye naye chumbani gerezani. Siku moja aliniambia, 'Sijui wewe ni binadamu wa namna gani! Watu wengi humu gerezani wanakutukana na kukutesa, bali wewe unawapenda wote!*

*Mimi nilimjibu kwamba Mungu ametufundisha kuwapenda watu wote, hata adui zetu, wala siyo rafiki zetu tu. Mwanzoni msichana huyu alinitesa mno. Lakini nilimwombea kwa bidii sana. Hata siku moja aliponiuliza kama naye ningempenda, mimi nilimkumbatia upesi, ndipo sote tukaanza kulia machozi. Tangu pale, sote twaomba pamoja.*

*Tafadhali sana mkumbukeni msichana huyu katika maombi, jina lake aitwa Varia.*

*Wakati unaposikia mazungumzo ya watu wamkanao Mungu, yawezekana kufikiri kwamba kweli ndivyo walivyo. Lakini maisha ya wengi wao yaonyesha kwamba wanamkana Mungu kwa vinywa vyao tu, bali roho zao zamlilia na kumhitaji mno. Kweli maumivu na kuugua kwa roho husikilikana wazi. Watu hawa wanatafuta kitu fulani cha kujaza ukiwa ule walio nao mioyoni mwao - ukiwa uletwao na hali ya kutokuwa na Mungu.*

*Dadayo katika Kristo,*

*Maria."*

*Barua ya Pili:*

*"Katika barua yangu iliyotangulia nilikueleza habari za Varia, msichana aliyekuwa akimkana Mungu. Sasa naharakisha kukueleza furaha yangu kuu niliyo nayo kuhusu huyu mpendwa wangu. Varia amekwisha kumwamini Yesu Kristo kuwa Mwokozi wake, tena anashuhudia kila mtu wazi wazi.*

*Wakati Varia alipomwamini Kristo na kufahamu*

*furaha kuu ya wokovu, pale pale alihuzunika mno. Kwa sababu alikuwa amepanda na kueneza mawazo kwamba hakuna Mungu. Sasa amekata shauri kufidia tendo kilo!*

*Mimi na Varia tulihudhuria mkutano wa Wakomunisti wamkanao Mungu. Ingawaje nilikuwa nimemwonya anyamaze, lakini maonyo yangu hayakusaidia kitu! Sote tulikwenda kutazama jambo ambalo lingetukia. Baada ya kuimba wimbo wa Kikomunisti ambao Varia mwenyewe hakuimba, aliomba apewe muda wa kusema maneno. Na wakati wake ulipofika, alisimama mbele ya mkutano. Kwa ujasiri mkuu, tena mbele ya watu wote, alishuhudia kuwa Kristo ni Mwokozi wake. Isitoshe aliwaomba rafiki zake wa zamani wamsamehe kwa kuwa macho yake ya kiroho yalikuwa yamefumbwa hata asiweze kutambua kwamba alikuwa akielekea na kuongoza wengine katika maangamio ya milele. Aliwanasihi watu wote kuacha dhambi na kumwamini Kristo.*

*Watu wote walinyamaza kimya, wala hapakuonekana aliyemkata kauli. Baada ya mazungumzo kwa sauti yake ya kupendeza aliimba wimbo wa Kikristo usemao, "Sitahayari kumshuhudia Kristo aliyekufa kusudi kuhifadhi amri zake na msalaba wake."*

*Baadaye Wakomunisti walimchukua Varia wetu. Na leo hii ni tarehe 9 Mei, wala sijui mahali alipo. Walakini, Mungu anao uwezo kumwokoa. Mwombeeni!*

*Ndimi wako,*

*Maria."*

*Barua ya Tatu.*

*"Jana tarehe mbili Agosti nilipokuwa gerezani, nilizungumza na Mpendwa wetu Varia. Moyo wangu unaumia vibaya kila ninapomfikiri. Kweli Varia bado*

*angali kijana mdogo, maana ana umri wa miaka kumi na tisa tu. Vile vile rohoni, bado ni mtoto mchanga katika maisha ya kiroho, sababu, ameamini hivi karibuni. Lakini anampenda Kristo kwa moyo wake wote naye mara moja aliingia katikanjia ngumu.*

*Huyu msichana maskini ana njaa mno! Tulipofahamu kwamba yumo gerezani, mara tulianza kumtumia vifurushi, lakini alipokea vitu vichache tu miongoni mwa vile vilivyotumwa.*

*Nilipomwona jana, alionekana amekonda sana, dhaifu, tena mwenye mapigo mabaya. Lakini macho yake yaling'aa kwa nuru ya amani ya Mungu isiyo ya dunia hii.*

*Naam, ndugu zangu wapendwa, wale ambao hawajapokea amani hii ya Kristo iliyo ya ajabu, hawawezi kufahamu neno hili—. Bali wenye amani hii wana furaha kuu ajabu! Mateso na vipingamizi tulivyowekewa havitunyamazishi sisi tulio katika Kristo.*

*Nilimwuliza Varia kupitia katika ngome ya vyuma, 'Je, Varia, unajuta kwa sababu ya kumwamini Kristo?'*

*Varia alijibu bila kusita, 'Hasha! Sijuti kamwe! Hata leo hii wakinifungua nitakwenda kuwaambia watu habari ya upendo mkuu wa Kristo. Usifikiri kwamba ninateseka hivi. Mimi ninafurahi kwani Yesu ananipenda mno hata kunipa nguvu na furaha ya kuvumilia yote haya kwa ajili ya jina lake.''*

*Tafadhali sana zidini kumwombea. Haijulikani, huenda pengine akapelekwa kule kaskazini, Siberia, kwenye baridi kali. Amenyang'anywa nguo zake zote na kuachiwa zile alizo nazo mwilini tu. Wala Varia hana jamaa, hivyo yatupasa tumkusanyie vitu vya lazima. Nimetunza sehemu ya vitu ulivyonitumia. Na kama Varia atapelekwa kule, basi nitampa.*

*Mimi naamini kuwa Mungu atamwimarisha na kumpa nguvu ya kustahimili mateso yanayomkabili. Mungu amtunze na kumhifadhi vizuri!*

*Wako,*

*Maria."*

*Barua ya Nne: (Toka gerezani).*

*"Mpendwa Maria,*

*Mwishowe hata mimi nimeweza kukuandikia! Tulifika salama hapa——. Kambi yetu iko maili kumi (kilometa kumi na sita) toka mjini. Wala sintaweza kufafanua vile maisha yalivyo. Wayaelewa barabara! Ila napenda kukuandikia mambo yanayonihusu mimi mwenyewe.*

*Ninamshukuru Mungu atunzaye afya yangu na kunipa nguvu za kufanya kazi. Dada fulani na mimi twafanya kazi kiwandani, kwenye mashine. Ni kazi ngumu sana hata afya ya Dada huyu imekuwa mbaya mno! Hivyo huwa ni lazima mimi kufanya hata kazi yake. Naanza kumaliza kipande changu cha siku ndipo ninamsaidia huyu dadangu. Twafanya kazi muda wa saa kumi na mbili, au kumi na tatu kila siku. Chakula chetu ni kama chenu kidogo sana. Lakini maneno haya siyo ninayotaka kukueleza.*

*Moyo wangu wamhimidi Mungu kwa vile alivyokuongoza kunionyesha Njia ya Wokovu. Kwa maana sasa natembea katika Njia hii. Hivyo maisha yangu yana shabaha kuu, tena najua niendako, na ninateseka kwa ajili ya nani. Kila mara nasikia hamu ya kutoa ushuhuda kwa kila mtu kusudi kutangaza ukuu wa shangwe ya wokovu nilio nao moyoni mwangu.*

*Je, Ni nani awezaye kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo? Hakuna mtu wala kitu cho chote. Wala gereza au mateso haviwezi. Mateso*

*haya ambayo Mungu aruhusu yatupate, yanatutia nguvu zaidi katika imani. Moyo wangu umejaa shangwe, maana Neema ya Mungu yafurika.*

*Kule kazini naadhibiwa na kuteswa mara kwa mara, sababu siwezi kunyamaza kumshuhudia kila mtu vile Kristo alivyookoa maisha yangu. Bwana Yesu amenifanya kiumbe kipya, mtu mpya, ambaye alikuwa akielekea jehanamu. Je, kweli naweza kunyamaza kimya baada ya jambo kama hili? Ng'o! Siwezi kunyamaza! Kwa kadiri midomo yangu iwezavyo kuzungumza, nitamshuhudia kila mtu habari ya upendo mkuu wa Mungu.*

*Tulipokuwa tukisafiri kwenda katika kambi, tulikutana na ndugu pamoja na dada wengi katika Kristo. Hushangaza mno kuona vile Roho Mtakatifu anavyokuongoza kuwatambua mara moja, kwamba ni watoto wa Mungu. Hakuna sababu kuzungumza nao kwanza ndipo uwatambue, bali kuwatazama tu kwatosha kukuonyesha kwamba wao ni watoto wa Mungu.*

*Wakati tulipokuwa tukiendelea na safari yetu kwenda katika kambi, mwanamke mmoja alitupa chakula tukiwa katika kituo cha gari la moshi. Bibia huyu baada ya kutupa chakula alisema maneno matatu, 'Mungu yu Hai!'*

*Ilikuwa jioni sana siku ile tulipofika kambini. Nasi tulipelekwa katika vyumba vya gereza la ardhini. Mle tuliwasalimu wale tuliowakuta Amani Kwenu!' Kwa shangwe kuu tulisikia jibu kutoka kila pembe 'Twawapokea kwa Amani!' Pale pale tulijisikia kuingia katika jamaa ya Mungu.*

*Naam, na ndivyo ilivyokuwa. Wengi tulio hapa tunamwamini Kristo kuwa ni Mwokozi wetu. Zaidi ya nusu ya wafungwa ni Wakristo. Miongoni mwetu pana waimbaji wakuu na wahubiri mashuhuri. Jioni, kila*

*baada ya kazi za shokoa, huwa ajabu na furaha kuu kukutanika miguuni pa Yesu kwa nyimbo na maombi, ingawa huwa kwa muda mfupi tu. Ndani ya Kristo pana uhuru po pote.*

*Kusema kweli, hapa mimi nimepata faida kuu ya kujifunza nyimbo za kiroho, tena kila siku naongezeka kukua katika Neno la Mungu. Humu gerezani imekuwa mara yangu ya kwanza kuadhimisha Kumbukumbu ya Kuzaliwa Kristo, ambavyo sasa nina umri wa miaka kumi na tisa. Na wala sitaisahau siku hii tukufu!*

*Mambo yalikuwa hivi siku ile. Ilikuwa lazima tufanye kazi nzito mno kutwa. Lakini baadhi ya ndugu walichomoka hadi mtoni pasipo kugundulika. Kule walichimbua barafu na kutayarisha nafasi ya kubatizia wakati wa usiku, kufuatana na amri ya Neno la Mungu. Mimi na ndugu wengine saba tulibatizwa usiku ule. Mbona ilikuwa shangwe kuu kwangu! Ningefurahi zaidi kama wewe Maria ungekuwapo usiku ule pamoja nami. Bila shaka ningefidia kidogo uovu wangu ule niliokutendea kabla. Lakini Mungu humchagua kila mtu na kumweka mahali pake, na ni sharti tusimame imara mahali pale pale Mungu anapotuweka.*

*Tafadhali nisalimie jamaa yote ya watoto wa Mungu. Naamini Mungu atabariki shughuli zako za kawaida kama alivyonifanyia mimi. Soma Waebrania 12:1-3.*

*Ndugu wote wanakusalimu. Tena wanafurahia imani yako katika Kristo, kwamba hata katika mateso yako yote waendelea kumhimidi, wala hukomi. Ukiwaandikia ndugu wengine, tafadhali wakilisha salamu na shukrani zetu.*

*Wako,*

*Varia."*

*Barua ya Tano: (Toka gerezani)*

*"Mpendwa Maria,*

*Mwishowe nimepata wasaa zaidi kukuandikia tena mistari michache. Ndugu yangu mpendwa, naweza kukuambia kuwa mimi na dadangu fulani tungali hai kwa sababu ya neema ya Mungu tu! Sasa tumo —, Nasi twapelekwa —, na tutakaa huko.*

*Dada, nakushukuru sana vile unavyonitunza kama Mamangu mzazi! Sote tulipokea vitu vile ulivyotutayarishia na kututumia. Zaidi, nakushukuru mno kwa ajili ya tunu yako kuu, yaani ile Biblia. Ninawashukuru ndugu wote ambao mlishirikiana kukusanya vitu hivyo. Tafadhali, fikisha shukrani zangu kwao.*

*Tangu Mungu aliponifunulia siri kuu ya upendo wake mtakatifu, najiona mtu mwenye furaha sana duniani. Mateso haya yanayonipata nayahesabu kuwa neema maalum. Nashukuru kwamba tangu siku ile ya kwanza kuamini, Bwana alinipatia furaha ya kuteseka kwa ajili yake. Niombeeni ili nizidi kuwa mwaminifu kwa Bwana mpaka mwisho.*

*Naomba Mwenyezi Mungu awatunze na kuwaimarisha nyote katika vita hii takatifu.*

*Mimi na Dadangu fulani tunawasalimu kwa busu. Kama tukipelekwa —, pengine tutapata nafasi kukuandikia tena. Msiwe na wasiwasi kwa ajili yetu. Sisi tuna furaha na shangwe kwa sababu thawabu yetu ni kuu mbinguni. Mathayo 5:11-12.*

*Wako,*

*Varia."*

Hiyo ndiyo barua ya mwisho kutoka kwa Varia, msichana Mkomunisti aliyemwamini Kristo, ambaye alihukumiwa kufungwa na kufanya kazi za kitumwa kwa sababu ya ushuhuda wake. Habari zake hazikusikika

tena. Lakini upendo wake wa ajabu, na ushuhuda wake kwa Kristo, vyaonyesha utukufu wa mateso na imani ya Kanisa la Siri katika thuluthi moja ya dunia iliyo chini ya utawala wa Kikomunisti.

SURA YA SABA

# Ujumbe Kutoka Kanisa La Siri

## Ujumbe Ninaowaletea kutoka Kanisa la Siri

Baadhi ya watu waniita "Sauti ya Kanisa la Siri." Lakini mimi mwenyewe najiona sistahili hata kidogo kuwa sauti ya sehemu tukufu ya Mwili wa Kristo.

Ingawa ni hivyo, niliwahi kuongoza Kanisa la Siri katika nchi za Kikomunisti muda wa miaka mingi. Kwa namna ya mwujiza, nimenusurika katika mateso na kifungo cha miaka kumi na minne, miaka miwili nikiwa katika "chumba cha mauti." Vile vile kwa njia ya mwujiza mkuu zaidi, Mungu aliona vyema anitoe gerezani na kuniIeta katika nchi za Magharibi kusudi nizungumze na Kanisa huru.

Hivi sasa mimi ninazungumza kwa niaba ya ndugu zangu ambao wamelala katika makaburi yasiyohesabika. Ninazungumza kwa niaba ya ndugu zangu ambao sasa hivi wakutanika kwa siri mistuni, mashimoni, katika vyumba vya siri, na po pote pale.

Kanisa la Siri nchini Rumania lilikata shauri nitoke kule na kupeleka ujumbe kwa Wakristo huru kote ulimwenguni. Kwa njia ya mwujiza tena, nimewahi kutoka Rumania. Sasa ninatimiza kazi niliyopewa kufanya na wale waliobaki wakitumikishwa, wakitoa maisha yao, wakiteseka na kufa katika nchi za Kikomunisti.

Na huu ndio Ujumbe maalum ninaowaletea kutoka Kanisa la Siri:

"Msifarakane nasi!"

"Msitusahau sisi!"

"Msitufute mawazoni mwenu!"

"Tupatieni zana tunazohitaji! Sisi tutalipa gharama ya kuzitumia!"

Huo ndio Ujumbe niliotumwa kuwaletea. Nazungumza kwa niaba ya Kanisa nyamavu, Kanisa la Siri, kanisa "bubu" ambalo halina sauti ya kusema.

Kikiliza kilio cha ndugu na dada zenu walio katika nchi za Kikomunisti! Wao hawaombi watoroke kule, wala wapate maisha ya raha. Hasha! Wao wanaomba wapewe zana za kuwasaidia kupambana na kuzuia sumu wapewayo watoto wao kutokana na mafunzo ya uzushi wa kumkana Mungu. Wanaomba Biblia za kutumia kusudi kueneza Neno la Mungu.Je, wanawezaje kutangaza Neno la Mungu bila kuwa na Biblia?

Kanisa la Siri lafanana na Daktari aliyekuwa akisafiri kwa gari la moshi siku fulani. Gari lile liligongana na gari jingine, na abiria wengi walilala hoi wamejeruhiwa vibaya,na wengine wakifa. Kwa bahati yule Daktari hakuumia hata kidogo. Ndipo alitembea huko na huko miongoni mwa majeruhi na maiti wale. Ghafula alilia kwa huruma, "Heri ningekuwa na vyombo vyangu! Heri ningekuwa na vifaa vyangu —!"

Kwa vifaa vyake vya udaktari, bila shaka angeokoa maisha ya wengi. Kwa maana alikuwa radhi, tena alikuwa na moyo wa kupenda kusaidia — . Lakini hakuwa na vifaa vyake!

Hii ndiyo hali ya Kanisa la Siri. Kanisa hili liko tayari kujitoa kabisa. Liko radhi kutoa wafia dini! Liko tayari hata kukaa gerezani muda wa miaka mingi. Lakini nia na utayari wake havina faida kama halipati vifaa na zana za kutumia kazini. Hivyo Kanisa la Siri lawasihi ninyi watu wa Kanisa huru likisema: "Tupatieni vifaa - Vitabu vya Injili, Biblia na Vijitabu vya Neno la Mungu, hata msaada wo wote ule, ndipo sisi tutatimiza yabakiyo."

## Jinsi Wakristo Huru Wawezavyo Kusaidia

Kila Mkristo huru aweza kusaidia mara moja kwa njia kama hizi zifuatazo:

Watu hawa wanaomkana Mungu, ni watu wasiotambua chanzo cha uhai wao usioonekana. Wala hawana fahamu ya maajabu yaliyo duniani na katika maisha yao. Wakristo wanaweza kuwasaidia watu hawa kama watatembea katika imani kuu ya ushirika na Mungu wao asiyeonekana. Tena zaidi, Wakristo wanaweza kutusaidia kama wakiishi maisha kamili ya Kikristo na kujitoa kafara. Zaidi, wanaweza kutusaidia kama watapinga wazi wazi kila mara Wakristo wanapoteswa.

Wakristo huru wa nchi za Magharibi wanaweza kutusaidia kwa kuwaombea Wakomunisti ili waokolewe. Maombi haya yaonekana kama ya kijinga, lakini hayana hila. Sisi tuliwaombea Wakomunisti, lakini keshoye walitutesa vibaya zaidi.

Lakini, hata maombi ya Bwana Yesu kwa ajili ya mji wa Yerusalem, yalionekana kama ya kijinga, walakini yalikuwa manyofu. Maana kweli walimsulibisha baada ya sala zake. Hata hivyo, siku chache walipigapiga vifua vyao, na watu elfu tatu waliokolewa siku moja. Kuhusu watu wengine, maombi hayo hayakupotea bure. Maombi yo yote yasiyopokelewa na mtu yule aombewaye, hukurudia tena kwa njia ya baraka, na kuwa laana kwake yule uliyeombea.

Mimi na ndugu wengine tulimwombea Hitler na watu wake kusudi tutimize Neno la Bwana. Mimi nina hakika kwamba maombi yetu yalisaidia risasi za majeshi ya nchi rafiki ili kumshinda Hitler na jeshi lake.

Ni lazima tuwapende adui zetu kama nafsi zetu. Wakomunisti vile vile ni jirani zetu sawa na watu wengine wote.

Wakomunisti ni matokeo ya kutotimiza maneno ya

Kristo: "Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele."

Wakristo bado hatujatoa uzima huu kuwa tele kwa kila mtu. Bali baadhi ya watu wameachwa pembeni. Ndipo wale walioachwa pembeni wameasi na kuanzisha chama cha kikomunisti. Nao kila mara ni mateka wa dhuluma, yaani kutopata haki. Hivyo sasa ni wakali na wakatili mno. Nasi ni sharti tuwapinge. Lakini, Wakristo ni lazima wawapende adui zao hata kama wanapingana nao.

Siyo kwamba sisi sasa hatuna hatia, maana wamekuwa Wakomunisti. La! Tuna hatia kwa sababu ya kutotimiza wajibu na kazi yetu. Kwa sababu hii, ndiyo maana lazima tufidie kwa kuwapenda, tendo ambalo ni tofauti na kuwaombea.

Mimi si mjinga kupita kiasi kuamini kwamba upendo peke yake waweza kutatua tatizo la Wakomunisti. Wala nisingemshauri mtawala ye yote kukomesha fujo ya waasi kwa upendo tu. Ni lazima wawepo askari, mahakimu na magereza kwa ajili ya waasi, na wala siyo mapasta peke yao. Kama waasi na wavunja sheria wasipotubu, basi, sharti wafungwe gerezani. Wala tena sitatumia neno "upendo" katika maana ya Kikristo kubatilisha siasa, uchumi, na utamaduni wa Kikomunisti. Maana hata Wakomunisti wanaonekana ulimwenguni kama kundi la wanyang'anyi na waasi. Wanyang'anyi hunyakua mikoba, tena huiba nchi nzima.

Lakini Pasta na Mkristo mmoja mmoja wanaweza kufanya wawezavyo ili kuwaleta Wakomunisti kwa Kristo pasipo kujali maovu yale yanayotendwa na ukomunisti. Hata wale mateka wao wasio na hatia wanaweza kuletwa kwa Kristo vile vile. Ni lazima Wakristo tuwaombee Wakomunisti na mateka wao tukifahamu neno hili.

**Biblia na Vitabu Vya Injili Vyahitajika Haraka**

Pili, Wakristo huru wanaweza kusaidia kwa kutuma

Biblia na Vitabu vya Injili. Pana njia safi na salama kabisa ya kutuma vitabu hivi mpaka kuingia katika nchi za Kikomunisti. Tangu nitoke kule nimekwisha kutuma vitabu vingi ambavyo vimefika salama. Ni hakika pana njia halisi ya kuvituma, kama ninyi Wakristo huru mtavitoa kuwasaidia ndugu na dada zenu wa Kanisa la Siri. Nilipokuwa bado nchini Rumania, mimi mwenyewe nilipokea Biblia nyingi zilizotumwa kwa njia fulani. Wala hakuna swali kuhusu usafirishaji wake. Neno kuu ni kupatikana tu!

Biblia zahitajika mno! Maelfu ya Wakristo walio Urusi na nchi nyingine za Kikomunisti bado hawajapata kuona Biblia kwa muda wa miaka ishirini mpaka hamsini.

Siku moja watu wawili toka kijiji kimoja walifika nyumbani kwetu. Watu hawa walikuja toka kijijini kwao ili wafanye kazi ya kuparuza barafu wakati wote wa baridi kusudi wapate fedha za kununua hata Biblia kuukuu wapeleke kijijini kwao.

Wakati huo nilikuwa nimepokea Biblia mpya kutoka Amerika. Hivyo niliwapa moja mpya badala ya nzee. Kwanza walionekana kutoniamini! Walitaka kunipa fedha walizopata kwa kuparuza barafu. Lakini nilikataa wala sikupokea kitu kwao. Nao walirudi kwao kijijini.

Baada ya siku chache barua ya shukrani na furaha kuu ilifika kutoka katika kijiji kile, nayo ilikuwa na sahihi thelathini! Biblia ile moja waliikata vizuri katika vipande thelathini, nao huvisoma kwa kubadilishiana wao kwa wao!

Ni jambo la kuhuzunisha mno kumsikia Mrusi akiomba apewe ingawa ukurasa mmoja tu wa Biblia! Ukurasa huu utalisha roho yake, na roho za wenzake. Hawa hufurahia mno kubadilisha mbuzi au ng'ombe na Biblia. Mtu mmoja nimfahamuye aliuza pete yake ya arusi kusudi anunue Agano Jipya iliyojikunjakunja.

Watoto wetu hawajapata kuona kadi ya Krismasi. Na

kama wakipata moja, basi watoto wote kijijini watajikusanya kuitazama, na pale pale mtu mkubwa aweza kusimulia habari za mtoto Yesu na jinsi alivyozaliwa na Bikira. Kwa njia hiyo, hadithi ya Kristo na Wokovu huweza kuelezwa - mambo haya yote yanawezekana kutokana na kadi moja tu ya Krismasi! Tunaweza kutuma Biblia, Injili na karatasi nyingine nyingi. Hii ni njia mojawapo mwezayo kutusaidia.

Tatu, ni lazima tuchape na kutuma maandishi maalum kupingana na sumu ya mafunzo ya uzushi wa kumkana Mungu wapewayo watoto tangu shule za msingi mpaka Vyuo vikuu.

Wakomunisti walikwisha kutayarisha kitabu kiitwacho "Kiongozi cha Amkanaye Mungu." Hii ndiyo Biblia ya kila amkanaye Mungu. Katika shule za msingi watoto hufunzwa aya nyepesi. Na aya ngumu zaidi zafunzwa katika vyuo vya juu kadiri mtoto aendeleavyo. Biblia potovu hizi hufuatana na maendeleo ya mtoto, akipewa sumu njia nzima ya masomo yake.

Ajabu ni kwamba Wakristo kote ulimwenguni hawajachapa kitabu cha kupinga bilbia hii ya Kikomunisti! Wakristo tunaweza, tena ni lazima tuchape na kutuma majibu ya Kikristo kuhusu sumu ya uzushi wapewayo vijana.

Ni lazima kitabu kama hiki kiandikwe na kuchapwa, ndipo kitumwe mara moja, maana Kanisa la Siri halina kitabu cha kuwapa vijana waliopewa sumu ya kitabu kile. Kanisa la Siri litadumu katika hali ya kufungwa mikono mpaka litakapopata kitabu kama hiki kimechapishwa katika lugha mbali mbali.

Vijana wetu walishwao sumu ya uzushi lazima wapate jibu; jibu la Mungu - jibu la Kikristo, jibu letu! Hii tena ni njia mojawapo mwezayo kusaidia, yaani kuandika na kuchapa kitabu cha kujibu kile cha kikomunisti kiitwacho *Kiongozi cha Amkanaye Mungu.*

Jambo la nne tuwezalo kufanya, ni kuwaunga mkono ndugu wetu wa Kanisa la Siri. Yawezekana kuwapa msaada wa fedha kusudi waweze kusafiri huko na huko wakieneza Injili toka mtu hata mtu. Kwa sasa ndugu wengi wamefungwa majumbani mwao na hali ya kukosa fedha za kulipa nauli na chakula wakisafiri.

Hivyo wamezuiwa wala hawawezi kusafiri tangu kijiji hata kijiji, ambavyo wakaaji wanawaita mara kwa mara ili wahudhurie mikutano ya siri. Kwa kutoa kiasi cha Shs. 100 au Shs. 120 kwa mwezi, twaweza kuwafungua watumishi hawa ili waweze kuvihudumia vijiji vile vinavyowaita mara kwa mara. Ndugu hawa watapeleka Neno la Mungu vile vile.

Wale mapasta ambao wamewahi kufungwa gerezani kwa ajili ya imani yao, ni moto moto sana kutangaza Injili ili kuokoa roho zilizopotea. Lakini hawana njia ya kusafiri mpaka vijijini. Bali matoleo kidogo yatawapa njia ya kupeleka ujumbe wa Injili vijijini.

Wakristo wanaume kwa wanawake wanahitaji msaada. Kwa kuwa ni Wakristo, basi kule Urusi hawapati mapato ya kuwatosha waishi, au hata wabakize fedha kidogo tu ili wasafiri kueneza Injili. Huu ni mwujiza, maana matoleo kidogo tu yatawawezesha kusafiri huko na huko wakipeleka Injili.

Baadhi ya mapasta wa kanisa zile zinazoruhusiwa na serikali huongoza mikutano ya siri vile vile. Tendo hili ni la kujitoa kafara. Lakini, nao wanataka msaada wa siri kusudi waendeshe mikutano hiyo. Ile mishahara walipwayo na serikali za Kikomunisti ni kidogo kabisa, wala haiwatoshi waishi. Lakini wana upendo na moyo wa kujitolea hata kuhatarisha uhuru wao kwa kutojali amri za kikomunisti. Bali kwa siri huhubiri Injili kwa watoto na vijana. Kazi hii tu peke yake haitoshi, sharti wawe na njia za kuendeshea huduma hii yenye kuzaa matunda.

Kiasi cha Shs. 100 au Shs. 120 kwa mwezi kitamsaidia mshiriki wa Kanisa la Siri kueneza Injili vizuri. Hii tena ni njia mojawapo mwezayo kusaidia katika huduma yao ya siri.

Njia nyingine yafuata. Ni lazima kutangaza Injili kwa redio katika nchi za Kikomunisti. Kwa kutumia vituo vya redio vilivyo katika nchi huru, twaweza kulisha Kanisa la Siri chakula cha kiroho, maana nalo lahitaji sana Mkate wa Uzima.

Kwa kuwa Wakomunisti hutumia redio kueneza habari zao, watu wengi wanazo redio, nao wanaweza kupokea ujumbe huu. Milango iko wazi ya kutangaza Injili kwa redio katika nchi za Kikomunisti. Kazi kama hii yafaa ipanuliwe sana. Kanisa la Siri sharti lipate chakula cha kiroho kutokana na mahubiri ya redio. Hii ni njia nyingine ya kusaidia Kanisa la Siri lililo katika nchi za Kikomunisti. (Sauti ya Injili, Addis Abbaba, imeanzisha mahubiri katika Kichina kwa ajili ya Wachina wa Peking) *Maneno yaliyo vibomani ni ya mfasiri.*

**Msiba Wa Jamaa Za Wakristo Wateswao**

Sharti tutoe msaada kwa jamaa za Wakristo wateswao. Makumi elfu nyingi ya jamaa zile sasa wanateseka kwa msiba usioelezeka. Mkristo wa Kanisa la Siri akamatwapo na kufungwa, msiba mkuu wa huzuni huwaangukia jamaa. Ni kesi ya jinai kwa mtu ye yote asaidiaye jamaa za Wakristo wafungwa. Neno hili ni hila mbaya ya Wakomunisti ili kuzidisha mateso kwa mama na watoto wabakio.

Wakati Mkristo atupwapo gerezani, mara nyingi huteswa na kufa. Lakini huu huwa mwanzo tu wa msiba. Mke wake na watoto huteswa bila kikoma. Mimi nashuhudia kweli kwamba kama Wakristo huru wasingetutumia msaada mimi na jamaa yangu,bila shaka tusingenusurika kuwaeleza na kuandika habari hizi!

Hivi sasa pametokea ukamataji mkuu mno pamoja na mateso ya Wakristo katika Urusi na kwingineko. Ingawaje Wakristo hawa wanakufa na kupokea thawabu zao mbinguni, lakini jamaa zao wanabakia katika msiba mkuu wa kuogofya. Sisi tunaweza, na ni sharti tuwasaidie. Bila shaka lazima tusaidie hata mataifa mengine yanayokufa kwa njaa kule sehemu za Asia na Afrika vile vile. Walakini, ni akina nani wastahilio kupata msaada wa Wakristo kuliko jamaa za watu wale ambao wanateswa na wamekufa kwa ajili ya Kristo – watu wateswao kwa ajili ya imani yao katika magereza ya Kikomunisti?

Tangu nifunguliwe, chama cha Kiristo cha Ulaya kimekwisha tuma msaada mwingi kwa jamaa za Wakristo wafia dini. Yote yale yaliyokwisha kutendeka ni kidogo mno yakilinganishwa na yale tuwezayo kufanya kutokana na msaada wenu.

Mimi kama mshiriki wa Kanisa la Siri ambaye nimenusurika na kuokoka, nimewaletea ujumbe, maombi na siaha kutoka kwa ndugu zenu niliowaacha huko. Wao ndio walionituma kutangaza ujumbe huu kwa niaba yao. Na kwa njia ya mwujiza nimesalimika mpaka kuutangaza ujumbe huu.

Nimewaeleza hitaji la haraka la kumtangaza Kristo katika ulimwengu wa Wakomunisti. Nimewaambia ilivyo muhimu kuwasaidia jamaa za Wakristo wafia dini upesi iwezekanavyo. Vile vile nimewaonyesha njia dhahiri za kuweza kusaidia Kanisa la Siri liweze kutimiza ujumbe wake wa kutangaza Injili.

Wakati nilipopigwa katika unyayo, ulimi wangu ulilia. Mbona ulimi wangu ulilia? Wenyewe haukupigwa! Lakini

ulilia kwa sababu unyayo na ulimi ni viungo vya mwili ule ule. Hali kadhalika ninyi Wakristo huru m viungo vya Mwili wa Kristo ipigwao sasa katika magereza ya Kikomunisti. Kweli hamsikii maumivu yetu?

Lile Kanisa la Kwanza katika hali yake kamili ya kujitoa kafara na kujitolea, limefufuka tena katika nchi za Kikomunisti.

Wakati Bwana Yesu Kristo alipokuwa akiteseka katika maombi bustanini Gethsemane, Petro, Yakobo na Yohana walikuwa umbali wa kutupa jiwe tu, lakini *walilala usingizi mzito!*

Je, ni kiasi gani cha matoleo au sadaka za Wakristo Kanisani hutolewa kusaidia Kanisa liteswalo? Ebu waulize Pasta na Viongozi wa Kanisa yako wakueleze vile wewe mwenyewe umepata kuwasaidia ndugu na dada zako watesekao katika magereza ya Kikomunisti.

Katika ngome za magereza ya Kikomunisti pana tamasha kuu la kifo cha mashujaa wafao kwa ajili ya Kristo, sawa sawa na Kanisa la Kwanza. Walakini Kanisa huru limesinzia!

Ndugu zetu huko peke yao wanapigana kwa ushujaa mno vita kuu ya karne ya ishirini, sawa kama vile mashujaa wa Kanisa la Kwanza. Walakini Kanisa huru lajisahaulisha vita na maumivu ya ndugu zao, sawa sawa kama vile Petro, Yakobo na Yohana walivyosinzia wakati Bwana wao alipokuwa akiteseka vibaya!

Je, hata nanyi mtalala usingizi mzito wakati huu ambapo ndugu zenu wa Kanisa la Siri kwa kuteswa wanapigana peke yao kwa ajili ya Injili?

Je, hamtasikia kilio chetu!

"Tukumbukeni sisi! Tusaidieni! Msitutupe!"

Sasa basi, huo ndio Ujumbe kutoka kwa ndugu na dada zenu wa Kanisa la Siri ambao wanateseka katika

utumwa wa ukafiri wa Ukomunisti umkanao Mungu.

Wasomaji wanaweza kumwandikia Mwandikaji wa Kitabu hiki kwa anwani hii:

**The Rev. Richard Wurmbrand**
**Inland Publishers**
**P.O. Box 125**
**Mwanza, Tanzania**

Zawadi kwa kazi ya Mungu katika nchi za Kikomunisti, pamoja na misaada ya kusaidia jamaa za wafia dini, vyote vyaweza kutumwa kwa anwani hiyo, kwa kupambanua – "Mchango kwa Ulimwengu wa Kikomunisti" (Fund For the Communist World).

INLAND PUBLISHERS

BOX 125
Mwanza, Tanzania